

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kumi – Tarehe 22 Juni, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):

Taarifa ya mwaka na hesabu zilizokaguliwa za Baraza la Hifadhi na Usimamizi za Mazingira kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 *(The Annual Report and Audited Accounts of National Environment Management Council (NEMC) for Financial Year ended 30th June, 2011).*

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Taarifa ya mwaka na hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka 2008/2009 *(The Annual Report and Accounts of Mzumbe University for the Year 2008/2009).*

Taarifa ya maka na hesabu za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka 2008/2009 *(The Annual Report and Accounts of Open University of Tanzania for the Year 2008/2009).*

MASWALI NA MAJIBU

Na. 96

Utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA aliuliza:-

Ibara ya 23(1) ya sheria ya Gharama za Uchaguzi inataka mgombea kusafirisha wapiga kura kwenda au kutoka katika kituo cha Kupiga Kura na kwamba jukumu la kusafirisha na kuwarudisha wapiga kura ni la Serikali:-

- (a) Je, Serikali inatekeleza wajibu huo?
- (b) Je. Serikali imepata uzoefu gani katika kutekeleza sheria hiyo?
- (c) Je, sheria hiyo ilisaidia kuondoa rushwa katika uchaguzi au iliwakinga baadhi ya wagombea na kuwatisha wengine?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa Rais na wabunge, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilijitahidi kuweka vituo vya kupigia kura karibu na maneno ya wananchi. Hatua hii ilisaidia kuondoa tatizo la wananchi kushindwa kwenda kupiga kura kwa sababu ya umbali wa vituo vya kupigia kura. Aidha, Serikali haikuwahi kupokea malalamiko yoyote kutoka kwa wagombea wa vyama vya siasa kusafirisha wapiga kura kwa sababu ya umbali wa vituo au wananchi kushindwa kufika kwenye maeneo ya vituo vya kupigia kura kwa sababu yoyote. Endapo Serikali ingepokea maombi hayo ingeyafanyia kazi na kutekeleza jukumu hilo kulingana na matakwa ya sheria ya Gharama za Uchaguzi, Ibara ya 23(1).

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ya Gharama za Uchaguzi imeanza kutumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa mwaka 2010. Pamoja na kwamba tathmini ya utekelezaji wa sheria hiyo bado inaendelea, Serikali imejifunza mambo mengi mazuri yaliyosaidia uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kuwa wa amani na utulivu. Uzoefu mzuri tuliopata ni kupungua kwa kiasi kikubwa cha malalamiko ya matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2005. Aidha, ziko dalili kuwa vyama na wadau wengine hawakutekeleza kikamilifu jukumu la kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha waliojiandikisha kujua umuhimu wa kupiga kura. Hali hii ilisababisha wananchi wengi kutoenda kupiga kura.

(c) Mheshimiwa Spika, sheria ya gharama za uchaguzi kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza vitendo vya rushwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Kama nilivyoeleza katika sehemu (b) malalamiko ya matumizi makubwa ya fedha kwenye uchaguzi yamepungua sana mwaka 2010 kuliko ilivyokuwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ya Gharama za Uchaguzi ilitungwa na Bunge lako Tukufu si kwa lengo la kumkinga mtu yeyote au kumtisha mwingine, bali kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu unakuwa huru na wa haki. Aidha, Serikali ipo tayari kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wadau mablimbali kuhusu maboresho ya sheria hiyo. (Makofi)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu aliyojitahidi Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Ibara ya 23 ya sheria ya gharama za uchaguzi nilioulizia swali, ibara ndogo ya (7) ambayo Serikali imeshindwa kutekeleza inahusiana Serikali kutoa usafiri na kusafirisha wapiga kura ni kitu ambacho kimesababisha kwa Jimbo langu, wapiga kura zaidi ya 40 kukosa kwenda kupiga kura kwa sababu ya ugonjwa na maradhi mbalimbali wameshindwa kufika kwenye vituo na pamoja na kwamba Mbunge ninayo gari, nilishindwa kuwasafirisha kutokana na sheria hii.

(i) Je, Serikali inasema nini kwa kutokutekeleza sheria iliyojitungia yenyewe hapa Bungeni?

(ii) Kwa kuwa wapiga kura wa Jamuhuri ya Muungano au Mbunge wa Jamuhuri ya Muungano anatokea pande zote mbili za Muungano na wa kuwa sheria hii ilitungwa na Bunge lako Tukufu na kwa kuwa vyama vya siasa ni vya Kitaifa na sheria hii haikuhusisha Baraza la wawakilishi upande wa Zanzibar ilipotengenezwa na ina makosa kibao.

Je, Mheshimiwa Waziri utaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba sasa kwa kuwa sheria ilitungwa haraka haraka na uzoefu tulioupata utaweza kurekebisha sheria hii kwa kushirikiana na upande mwingine wa Zanzibar ambako hakuna TAKUKURU?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu zilizosababisha baadhi ya watu kutokupiga kura ziko nyingi, lakini siwezi kuzibainisha hapa kwa sababu bado Tume ya Uchaguzi na taasisi nyingine za Serikali kama Msajili wa Vyama vya siasa wanaendelea kufanya tathmini kadhaa ili tujue hasa ni sababu zipi za msingi zilizosababisha upungufu mkubwa wa watu kwenda kupiga kura. Inawezekana moja ya sababu ni hii ambayo anaisema Mheshimiwa Mnyaa. Lakini pia nimekiri kwamba sheria hii imetungwa na tumeitumia mara moja tu, inawezekana ina mapungufu.

Kwa hiyo, mimi nakubaliana na hitimisho la Mheshimiwa Mnyaa na ndiyo maana nimeomba wadau mbalimbali pamoja na Wabunge kwamba hili jambo tumelifanya mwaka mmoja, tumepata uzoefu, sasa upo umuhimu wa wadau mbalimbali wakiwemo akina Mheshimiwa Mnyaa na Waheshimiwa Wabunge wengine kutoa uzoefu wao na mapungufu kadhaa ili ikiwezekana Bunge hili liweze kurekebisha sheria hii kwa mujibu wa uzoefu tulioukata.

Kwa hiyo, hilo linawezekana na ndiyo maana tunakaribisha tathmini hii ifanywe kwa kupitia ninyi Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine. Tupo tayari kupokea maoni mbalimbali ili kufanyia marekebisho sheria hii.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Nikirejea mpango mkakati wa maendeleo wa miaka mitano, Serikali imekuwa ikitoa kauli kwamba mpango ule ni wa kwa kwetu sisi wote kama Watanzania na nikirejea swali la msingi la Mheshimiwa Mnyaa, inaonekana kwamba suala zima la kuhakikisha kwamba tunaona kwamba mambo yote yanakwenda sawasawa hapa nchini kwetu ni jukumu la kila raia wa Tanzania.

Hivi sasa Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba inaonekana ambao wanafanya tathmini ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika suala la baadhi ya wapiga kura wa Tanzania ambao walikuwa na matatizo mbalimbali kushindwa kwenda kupiga kura, inaonekana tathmini inafanywa na Tume.

Ni kwa nini Serikali wakati mwingine haitaki kukubaliana na taarifa ambazo zinakuwa zinatolewa na sisi Wabunge, inaonesha kwamba sisi Wabunge hatuaminiki, tukirejea haswa katika swali la msingi la Mheshimiwa Mnyaa. Kwa nini Serikali haitaki kukubaliana na sisi Wabunge na kukubali maoni yetu ambayo tunakuwa tunatoa? Naomba majibu. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge alilouliza la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge ametaka kuchanganya kidogo miaka mitano akaacha, akaja kwenye tathmini, mara Serikali haitaki sasa anasema Serikali haitaki kupokea tathmini. Nimetoka hapa sasa hivi nimekiri. Mheshimiwa Mnyaa amezungumza hoja na kwa niaba ya Serikali nimeikubali ile hoja kwamba tuko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kufanya hii tathmini kwa hoja hizo. Yaani hoja zitolewe, hoja zikitolewa tunazipokea, lakini Mheshimiwa Mbunge hukutoa hoja kwa hiyo, sijui ni hoja gani tumeikata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushauri toa hoja, tutaiangalia hoja yako, tutajadili, tutaikubali pamoja na wadau wengine. Tume ya Uchaguzi ni chombo cha kuratibu, lakini Waheshimiwa Wabunge mtoe maoni. Nampongeza Mheshimiwa Mnyaa ametoa maoni yake na tumeyachua. Kwa hiyo, Mheshimiwa kama una maoni yeyote Serikali iko wazi, tusilalamike, tuko tayari kupokea maoni. (*Makofi*)

Mahitaji ya Maji-Arumeru Mashariki

MHE. REBECCA M. MNGODO aliuliza:-

Ni kwa nini Serikali wakati mwingine haitaki kukubaliana na taarifa ambazo zinakuwa zinatolewa na sisi Wabunge, inaonesha kwamba sisi Wabunge hatuminiki, tukirejea haswa katika swali la msingi la Mheshimiwa Eng. Mohammed Habib Juma Mnyaa.

Kwa nini Serikali haitaki kukubaliana na sisi Wabunge na kukubali maoni yetu ambayo tunakuwa tunatoa? Naomba majibu.

Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa vijiji vya Sakila, Kikatiti, Mareu, Kingori na Legaruki Wilayani Arumeru, maeneo yenye shida kubwa sana ya maji kwa ajili ya binadamu na mifugo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma za maji safi na salama. Aidha, ni kweli kwamba vijiji vilivyotajwa hapa vina upungufu mkubwa wa maji safi na salama.

Katika kukabiliana na upungufu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru ipo katika mchakato wa kuunda chombo cha usimamizi wa kisheria cha watumiaji maji kitakachoweza kusimamia maji kidogo yanayopatikana ili yatumike kwa utaratibu mzuri utakaowezasha vijiji vilivyotajwa kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha kikatiti kwa sasa kinapata maji kutoka bomba la maji la KIMASAKI lililojengwa na kukamilika mwaka 2005 chini ya uhisani wa *CAFOD* wa nchini Uingereza kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali *CBHCC (Community Based Care Council)* lililopo katika Mji wa Arusha. Aidha, vijiji vya King'ori, Leguruki na Meru vinapata maji toka bomba la Ngarenanyuki/Leguruki/King'ori ambalo lilijengwa

mwaka 1963 ingawa miundombinu yake ni chakavu na inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi milioni 294 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maji kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji katika maeneo yaliyotajwa. Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa visima 6 katika ya visima 10 vilivyokuwa vimepangwa kuchimbwa hali ambayo imepunguza ukubwa wa tatizo la maji katika maeneo hayo. Aidha, Mtaalam Mshauri ajulikanae kwa jina la *Nelson Consultant* amepatikana kwa ajili ya kufanya usanifu wa miradi ya maji Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza juhudi za kuwapatia wananchi maji, Serikali katika mwaka 2011/2012 imetenga fedha shilingi bilioni 1.12 fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na usambazaji wa maji sambamba na kuweka matanki ya maji, kufunga pampu na kusukuma maji, kuweka mfumo wa umeme na kusambaza mabomba.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri napenda kumshukuru sana kwa kukubali kwamba vijiji vya Sakila, Kikatiti, Mareu na Kingori kwamba vina upungufu mkubwa wa maji safi na salama. Namshukuru pia amekubali kwamba vijiji vya Kingori, Leguruki na Mareu vinapata maji kwa bomba ambalo lilijengwa mwaka 1963 ni miaka miwili baada ya uhuru na amekubali kwamba miundombinu yake ni chakavu.

Namshukuru pia kwamba amesema kwamba Mtaalam Mshauri amepatikana ili kufanya usanifu wa miradi ya maji. Sasa ninapenda kuuliza huyo msanifu anaanza kazi lini, kwa sababu mtoto wa kike au mama wa Kimeru ndiye anaepata tabu kuamka mapema asubuhi kwenda kutafuta maji mbali na huyu mtoto wa kike ndipo aende shule. Watoto wengine wameacha shule, wamekatiza masomo yao na wasichana wengine....

SPIKA: Swali ni lipi sasa?

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ninataka kujua huyo mtoto wa kike lini mateso yake yatamwondoka kwa msanifu huyo ni lini anaanza kazi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mngodo kama ifuatavyo:-

Kwanza kumshukuru sana kwa shukurani ambazo amezitoa kwamba na sisi tumeona hivyo kwamba kuna tatizo, labda ni-declare interest ya hawa wako jirani na mimi katika Jimbo langu la Siha ndiyo maana nafahamu kama kuna tatizo.

Kwa hiyo, kama alitaka kunikona pale asingeweza, najua kwamba kuna tatizo pale. Chanzo cha kuaminika kabisa kilichopo pale ni chanzo kile kilichopo katika mto *Usa River* pale, lakini vile vyanzo vingine vya visima vimekuwa na matatizo kwa sababu wakati mwingine tumekuta kwamba vina *floride* yale maji yanayopataikana pale.

Sasa kama nilivyosema hawa *Nelson Consultant* wameshapatikana tayari. Kwa hiyo, kwa maneno mengine ni kwamba kazi inaanza mara moja, kwa hiyo kazi hii itaanza sasa hivi kwa hiyo, aende akafuatilie na mimi nina muahidi kwamba nikitoka hapa nitapita kule kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa maswali mengi ya Wabunge yanauliza mradi wa world bank, vijiji kumi kwa kila Wilaya.

Je, Serikali haioni kwamba kuna matatizo katika mradi huu na kufanya utafiti ili kuona kwamba tatizo ni nini kwa sababu mradi huwo unasuasua na wananchi wanashindwa kupata maji safi na salama kwa ajili ya mradi huwo kuchelewa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

SPIKA: Naomba uhamie kwenye meza nyingine, hiyo mashine huwa haisikiki vizuri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa *world bank* kama tulivyokwisha toa kauli hapa Bungeni, ni kweli ulikuwa umechelewa jinsi ilivyotarajiwa, lakini kwa sasa tumejipanga vizuri. Maana awamu ya kwanza hii, Halmashuri zilizo nyingi tayari zimeshapata hatua ya kuweza kupata washauri, tayari wameshaweka makandarasi wameshachimba visima ni Halmashauri chache ambazo zimesuasua na hizi chache sehemu kubwa ilikuwa ni kwa sababu ya uwezo waliokuwa nao wa utekelezaji wa miradi hii.

Lakini katika awamu inayokuja, tutahakikisha kwamba hizo kasoro ndogo ndogo tunazikamilisha ili Halmashauri zote ziweze kumaliza mradi kama ilivyotarajiwa. (*Makofi*)

Na. 98

Tatizo la maji Mji mdogo wa Lushoto

MHE. HENRY D. SHEKIFU aliuliza:-

Mji mdogo wa Lushoto unakabiliwa na tatizo kubwa la maji na mradi wa kuupatia maji mji huo kutoka chanzo cha maji ya mto Kibohelo umekwishaandaliwa lakini utekelezaji wake unasuasua:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukamilisha mradi huo ili kumaliza tatizo la maji katika mji huo na vitongoji vyake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha huduma za maji zinaimarishwa katika mji mdogo wa Lushoto, Serikali imekamilisha ujenzi wa matanki ya maji ya kupunguza nguvu ya maji Magamba ambayo yamejengwa sambamba na ununuzi wa mabomba inchi 6 na uchimbaji wa mtaro kwa ajili ya kutandaza mabomba kutoka chanzo cha maji hadi kwenye tanki la maji lililopo Maguzoni lenye ujazo wa lita 225,000. Awamu hii imetumia shilingi milioni 383.7.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha ujenzi wa tanki la kuhifadha maji katika Kitongoji cha Kungurui katika Kijiji cha Magamba lenye ujazo wa lita 681 kwa ajili ya usambazaji maji katika mji mdogo wa Lushoto. Awamu hii itahitaji shilingi milioni 340.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2010/2011 zilizotengwa shilingi bilioni 1.6 zikiwemo fedha za wahisani ambao ni Benki ya Dunia, kwa ajili ya miradi ya maji ya vijiji 10. Kiasi cha shilingi milioni 200 zilitolewa na kutumika kukeleza miradi ya maji yaani *Quickwins*.

Kwa sasa mpango uliopo wa kuondoa tatizo la maji katika mji mdogo wa Lushoto na vitongoji vyake ni kupima, kusanifu, kuandaa michoro, kuandaa zabuni na kutayarisha miradi itakayojengwa ili kuhakikisha upatikanaji wa maji Makao Makuu ya Wilaya za Lushoto, Mombo, Korogwe, Songe na Handeni-Kasela.

Ili kutimiza azma hiyo katika mwaka wa 2011/2012 zimetengwa shilingi bilioni 1.9. Aidha, ujenzi wa tanki la *Magamba Coast* lenye ujazo wa lita 135,000, ujenzi wa tanki la Mbula lenye ujazo wa lita 135,000. Ununuzi na utandazaji wa mabomba yenye urefu wa inchi 4 kutoka Magamba hadi Maguzoni utafanyuika katika kipindi hicho. Taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri zinaendelea.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujitahidi kujibu swali hili. Ukiangalia yaliyojibiwa na yale yaliyoko katika hali halisi ni vitu viwili tofauti. Nimwombe Waziri

na Wataalam kama ikiwezekana basi wafike Lushoto wahakiki kile kinachosemwa. Kwa sababu ninaamini kama kilichosemwa humu kingekuwa ni sahihi basi tatizo la maji Lushoto lingepungua sana.

Swali la pili, hilo la kwanza ni ombi aje. Kwa kuwa mradi huu ni kama ulivyosema ulisanifiwa na ni muda mrefu na mradi ulianza na unasuasua, hivi huyu mtaalam mshauri anatafutwa aje afanye nini? Ahsante sana Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nimshukuru kwamba anakubali kwamba maelezo tuliyotoa hapa ndiyo yenyewe, ingawa katika hali halisi Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna tatizo pale. Mbunge anayezungumza hapa ni mtu mkubwa, amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara na amewahi kuwa Mbunge humu ndani wa Lushoto hiyo, anayoizungumza ni Lushoto ambayo nimewahi kwenda, nimeona katika eneo lile. Ni kweli kabisa analosema kwamba kuna matatizo pale. Siwezi kubishana na Mheshimiwa Mbunge ambaye yeye ndiyo anatoka kule yuko *fresh* kuliko mimi, na kwa taarifa ya Kikao hiki pia huyu ni Mjomba wangu. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa kuna mambo mawili hapa yanazungumzwa, ambayo kama hayakuelezwa vizuri yatachanganya watu. Huu mradi wa kwanza ambao tumesema kwamba una bilioni 1.6 huo mradi huo ndiyo ule ambao uko kwenye mambo ya *World Bank* ambao Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ametusaidia kujibu vizuri sana kwamba kumekuwepo na haya matatizo. Huu mradi wa pili unaozungumzwa wa bilioni 1.9 hauko katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Huu mpango unaratibiwa na Mkoa wa Tanga na yule Kiongozi wa Mkoa wa Tanga wa Maji yeye ndiye anasimamia mradi huu. Ndiyo maana nilipotaja hapa sikutaja Lushoto tu. Nimetaja Korogwe na Mombo wote nikawataja kule. Sasa anasema kwamba anatafuta kwa ajili ya nini. Yule aliyepatikana alikuwa ule mradi wa kwanza, ule niliousema pale, ndiyo maana anasema mbona tunazungumza tena habari ya kwamba anatafutwa mtu wa kusanifu na nini. (*Makofi*)

Hii mnayozungumza hapa, ina *complement* tu mpango ule wa kuhakikisha kwamba maji katika mji wa Lushoto yatapatikana. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kwa namna anavyohangaika kuhakikisha watu wake wa Lushoto wanapata maji safi na salama. Kuhusu kwenda kule mimi kama nilivyosema huyu ni Mjomba wangu nitakwenda Lushoto ili nikasaidiane naye kuhakikisha kwamba maji yanapatikana.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Tatizo la Lushoto halina tofauti sana na lile lililopo katika Wilaya ya Kondoa hususani katika Jimbo la Kondoa Kusini. Mradi wa Maji wa Ntomoko wa mwaka 1974 mabomba yake yote yamekwishachakaa. Vijiji 14 vinategemea bomba hilo lakini sasa wanatembea zaidi ya kilomita 20 kwenda kutafuta maji. Mheshimiwa Rais alipokuja wakati wa kampeni aliahidi kwamba tatizo hilo

lingeshughulikiwa kwa haraka. Hadi leo hakuna mpembuzi yakinifu wala msanifu. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu tatizo hili? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante iko sawa kwa sababu wewe siyo mjomba wake na huyu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hili la Ntomoko tunalifahamu, nalijua, hata Baba wa Taifa alishughulika sana na mradi huu. Ni mradi mkubwa, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Nkamia kwamba kuna tatizo pale kwa sababu mabomba yale yamechakaa na mimi mwenyewe nimefika pale nimeona. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane, tukae wote kwa pamoja, tu-*compare notes* kidogo. Siwezi kujibu haraka haraka hapa ili tuone kwamba ni nini ambacho tunaweza tukasaidia pale.

Lakini kufika kwenye hiyo Ntomoko yenyewe anayoizungumza, ni kweli mabomba pale ni chakavu kwa kunahitaji kamsaada pale. (*Makofi*)

Na. 99

Sheria Inayowazuia Wakulima Kulima Kando Kando ya Ziwa Victoria

MHE. ALPHAXARD (K.n.y. LUGOLA) aliuliza:-

Kilimo ndio ajira kubwa inayowapatia kipato wananchi walio wengi vijijini; wapo wakulima katika jimbo la Mwibara wanaolima kando kando ya Ziwa Victoria ambao wamekuwa wakisumbuliwa na kunyanyaswa na kikundi cha usimamizi wa rasilimali ya uvuvi katika Ziwa Victoria kitiwacho *Beach Management Unit (BMU)* kwa visingizio vya uharibifu wa mazingira.

- (a) Je, ni sheria gani inayowazuia wakulima hao kulima kando ya ziwa hilo?
- (b) Je, ni umbali gani kisheria usioruhusiwa kulima kwenye fukwe za ziwa hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni Ziwa Victoria limekabiliwa na ongezeko la shughuli za kijamii na kiuchumi ndani na nje ya ziwa, zinazosababisha ongezeko la uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya ziwa.

Kutokana na umuhimu wa ziwa hilo, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria na mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria (LVEMP I & II) ilianzisha vikundi vya walinzi wa fukwe za ziwa (*Beach Management Unit*) ili kupunguza shughuli zenye madhara kwa ubora na bayoanuai ya ziwa hilo. Vikundi

hivyo husimamia na kudhibiti shughuli za uvuvi haramu na kilimo kando kando ya ziwa kufuatana na sheria zilizopo.

Sheria zinazozuia kulima kando kando ya ziwa ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 Kifungu Na. 57 (1) na (2) na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009, Kifungu Na. 34.

(b)Mheshimiwa Spika, umbali usioruhusiwa kuendesha shughuli za kibinadamu kutoka kwenye fukwe za ziwa ni mita sitini (60) kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Kifungu Na. 57 (1).

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Kifungu Na. 34 kinaridhia Kifungu Na. 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kumpa Waziri mwenye dhamana ya maji uwezo wa kutangaza umbali zaidi ya mita sitini kutoka kwenye kingo za chanzo cha maji endapo ataona kwamba umbali wa mita sitini haukidhi mahitaji ya kuzuia chanzo husika kisichafuliwe au kuharibiwa.

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri, ni kwamba Sheria inatamka kusiwe na shughuli yoyote ya binadamu ndani ya mita 60 kando kando ya Ziwa Victoria na kwa kuwa Watanzania wenzetu walioko Mwanza Mjini, Musoma Mjini na Bukoba Mjini ambao nao wako Ziwa Victoria wana majengo, kuna viwanda na makazi ndani ya mita 60 je, ni lini Serikali itaondoa majengo hayo ili wawe sawa na wengine? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 13(iv) inapiga marufuku mtu yoyote asibaguliwe na mtu yoyote au na mamlaka yoyote katika kutekeleza Sheria.

Je, Serikali inawapa matumaini gani Wana-Mwibara ambao wamebaguliwa na Sheria hii ili na wao wawe sawa na wale ambao wako mjini wako ndani ya mita 60?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maeneo ambayo bado kuna majengo ambayo yako ndani ya mita 60. Sasa sheria hii ilivyoanzishwa mwaka 2009 majengo mengi yalikuwa yamejengwa kabla ya muda huo.

Sasa ni hatua ambazo tutaanza kuchukua wale wote ambao wamejenga ndani ya mita 60 kwa sababu wamevunja sheria ili waweze kuondoa majengo hayo.

Suala la kubaguliwa, mimi nafikiri Sheria si kwamba inabaguliwa. Sheria inamwuhusu mtu yoyote na maudhui ya Sheria hii ni kulinda rasilimali za maji za Ziwa. Kama unavyofahamu miaka yote hii ukiangalia kwamba mito mingi iliyokuwa na maji sasa hivi haina maji.

Sasa tusipoweza kulinda Sheria hii ya mazingira na vyanzo vya maji itafika mahali kwamba tutakuwa hatuna maji ambayo kila mahali tunasema hakuna maji. Kwa

hiyo lazima tusimamie Sheria hii na Sheria haiwezi kuwa baguzi. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba mtu yoyote anafuata Sheria iliyowekwa.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Jina langu Tizeba. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Mimi nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hizi *Beach Management Units* wanachaguana pale kijijini na kwa kweli hawana mafunzo yoyote kuhusu mazingira na kwa kweli maudhui ya kazi yao yanakuwa *mis-interpreted*. Ndiyo maana malalamishi mengi yako *around* juu ya hilo jambo.

Je, Serikali haioni sasa iko haja ya Wizara ya Uvuvi kushirikiana na Wizara ya Maji na Mazingira ili kuendesha mafunzo kwa hivi vikundi ili viweze kutekeleza kazi yake vizuri? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba iko haja ya kuunganisha Wizara za Uvuvi pamoja na Maji pamoja na Mazingira ili kuweza kutoa mafunzo yanayostahiki katika vikundi vya hivi vya *Beach Management Units* ili wafanye kazi zao inavyotakiwa.

Na. 100

Ulinzi katika Hifadhi ya Ngorongoro na Manyara

MHE. MCH. ISRAEL J. NATSE aliuliza:-

Wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Ngorongoro na Manyara huathirika sana na uharibifu unaofanywa na wanyamapori wao binafasi na mali zao:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda usalama wa maisha ya watu wake na fidia kutokana na uharibifu ufanywao na wanyama?
- (b) Je, Halmashauri zinazopakana na Hifadhi hizo zinanufakaje na rasilimali hizo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, kuwa kumekuwa na tatizo la wanyamapori kuharibu mali za wananchi ikiwa ni pamoja kuhatarisha maisha yao.

Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imejenga vituo vinne vya ulinzi vya Endamagha, Oldean, Rhotia, Mbulumbulu na Lositete ambavyo vipo mpakani mwa Hifadhi na Wilaya ya Karatu. Askari waliopo katika vituo hivyo hushiriki katika zoezi la kudhibiti wanyamapori wanaovamia mashamba na makazi ya wananchi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali itaongeza vituo vingine katika maeneo ya Engaruka na Engiresero.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 Kifungu 71 (1) na 71 (2), Serikali hutoa kifuta jasho kwa wananchi walioathirika na wanyamapori kwa kuharibiwa mashamba yao na kifuta machozi kwa ndugu wa marehemu wanaouawa na wanyamapori hao. Viwango hivyo vimeainishwa katika Kanuni zinazosimamia suala hilo ambazo zimeanza kutumika kuanzia mwezi Aprili mwaka huu.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zinazozunguka Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Manyara zinanufaika sana na rasilimali zilizomo katika Hifadhi hizo kwanza kwa kupata ajira kwa wananchi ambao wanawaongoza wageni kwenda hifadhini.

Wananchi ambao wanafanya biashara mbalimbali ikiwepo biashara ya hoteli ndogo ndogo, biashara ya vinyago, na miradi ya ujirani mwema. Kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2011, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetumia zaidi, imetumia shilingi milioni 286 kugharimia miradi ya Maendeleo kupitia utaratibu wa Ujirani mwema.

Hali kadhalika Mamlaka imetumia sh.2.5 kusomesha wanafunzi 3207. Imetumia shilingi milioni 900 kununua chakula na kukisambaza kwa wananchi, na shilingi milioni 280 kununua vyakula kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na mwisho imetumia shilingi bilioni 9.9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Hili ni kwa Halmashauri zote zinazozunguka Hifadhi hiyo.

MHE. MCH. ISRAEL J. NATSE: Ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ninaomba maswali mawili madogo ya nyongeza.

SPIKA: Hiyo mashine yako ina-vibrate ama kuna wengine wamewasha. Naomba uhame kidogo.

MHE. MCH. ISRAEL J. NATSE: Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Hifadhi ya Ngorongoro imeundwa kisheria na inapakana na vijiji vya Endamagh, Losteti, Mbulumbulu. Ninaomba Waziri anihakikishie juu ya ulinzi wa wananchi hasa kijiji cha Endamagh kutokana na wanyama wanaoingia huko pia ulinzi kwa wale askari wanyamapori kuwakamata wananchi na kuwapiga wakigombania mpaka wa Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji hivyo na kumwomba Waziri kuandamana pamoja nami ili kuhakikisha mipaka hiyo na hali hiyo?

Swali la pili, vijiji vinavyopakana na *TANAPA* Manyara vya Kansai, Buge, Endabash, Mara. Je, Waziri anafahamu kwamba wananchi wanakamatwa na kupigwa faini bila risiti. Njia hiyo ni kupotezea Serikali mapato?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie tena Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse kwamba Serikali imeazimia kuongeza ulinzi katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 ili kuhakikisha ulinzi wananchi wa maeneo yote wanaozunguka Hifadhi ya Ngorongoro.

Hali kadhalika kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tunaongeza kituo cha maaskari katika eneo la Engaruka na eneo la Engisero. Hivi vitakuwa ni sambamba na vituo ambavyo sasa vinafanya kazi kwanza kudhibiti wanyama.

Pili kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi yako salama.

Tatu, Serikali inaazimia kuhakikisha kwamba askari wote wanafanya kazi kwa kufuata maagizo na nidhamu ya Serikali.

Hatutarajii kwa vyo vyote vile askari yoyote kupiga wananchi wakati wowote wa zoezi hilo na tutaendelea kutoa elimu kwa upande wa wananchi na elimu kwa upande wa askari kuhakikisha kwamba wote wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Serikali inazitaka mamlaka zote ikiwa ni pamoja na askari wanaotoza faini katika Hifadhi zetu za Taifa kuhakikisha kwamba risiti inatolewa mahali popote ambako fedha imetozwa kwa niaba ya Serikali iwe ni tozo, kama faini, iwe ni kodi na tutahakikisha kwamba tunafuatilia na kuhakikisha kwamba jambo hilo halitokei tena. (*Makofi*)

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, uharibifu unaofanywa na wanyamapori unafanyika katika maeneo ya vijijini. Na mheshimiwa Naibu Waziri, hapa ametueleza kwamba upo utaratibu na Kanuni wa kuafanya fidia kwa wale ambao wanaharibiwa mali zao. Lakini hakueleza utaratibu huo ukoje ili wananchi wajue.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza akatueleza ni utaratibu gani unatumika wananchi kudai fidia za mali zao?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi, Sheria ya Wanyamapori Namba 5, ya mwaka 2009, Kifungu 71 (a) na (b), kimeweka wazi utaratibu ambao utatumika. Tayari Wizara imetoa Kanuni ambazo zimeanza kutumika mwezi Aprili, 2011 na Serikali itakuwa tayari kutoa hizo Kanuni kwa wananchi na maeneo yote ambayo yanahusika, ili waweze kujua utaratibu ambao unafuatwa.

Na. 101

**Mpaka wa Hifadhi ya Kitulo na Eneo la Wananchi
Ngulumbu**

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA alijibu:-

Mwaka 2009 wanakijiji wa Ngumbulu, Kata ya Isongole, Wilaya ya Rungwe walipeleka malalamiko Wizarani kwamba baadhi ya alama za mipaka ya Hifadhi ya Kitulo na Kijiji chao zimekosewa, hali iliyosababisha *TANAPA* kumega eneo la kijiji kuwa la hifadhi, lakini barua yao hadi sasa haijajibiwa:-

Je, ni lini *TANAPA* itarekebisha mpaka huo ili wanakijiji wapate eneo la kulima?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ngumbulu ni mojawapo kati ya vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kwa upande wa Wilaya ya Rungwe. Eneo ambalo wananchi wa kijiji cha Ngumbulu wanalalamikia liko katika vitongoji vya Ipyela 'A' na Nsanga pembezoni mwa msitu wa Livingstone ambao kwa sasa ni sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Kutokana na uharibifu uliokuwa ukiendelea katika msitu huo, Serikali ilibadili matumizi ya msitu huo na kuufanya kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kwa Tangazo la Serikali Na. 279 la mwaka 2005. Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ulirithiwa kutoka mpaka wa Msitu wa Hifadhi wa Livingstone (*Livingstone Forest Reserve, GN No. 48; 1940*).

Mheshimiwa Spika, eneo linalolalamikiwa ambalo awali lilikuwa eneo la Msitu wa Hifadhi wa Livingstone, lilivamiwa na wananchi na ninaomba nirudie, lilivamiwa na wananchi wa Kijiji cha Ngumbulu ambao wamepanda mazao ya chakula na miti aina ya mikaratusi (*Eucalyptus*). Hii inamaanisha kuwa Hifadhi haijavamia kabisa eneo la

wananchi kwani mawe ya mipaka (*boundary beacons*) yaliwekwa kwa kuzingatia ramani na Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 1940 ambalo linaonesha sehemu za kuweka alama za mpaka (*co-ordinates*) ambazo tayari zilishawekwa mwaka huo wa 1940. Zoezi hili lilifanywa na wataalam kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Dar es Salaam kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Aidha, majadiliano yanaendelea kupitia maeneo sahihi ambayo yanastahili kuwa ndani ya Hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Kamati ya ulinzi na usalama inasimamia zoezi hilo na taarifa itatolewa pindi kazi hii itakapokamilika.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, migogoro kati ya vijiji vinavyopakana na hifadhi na hifadhi zenyewe, ipo nchi nzima mahali ambapo kuna hifadhi. Ushahidi ni kwamba kuna maswali mengi sana yanaulizwa hapa Bungeni. Je, Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari kupokea ushauri wangu kwamba sasa ni wakati muafaka ambapo wangeunda Tume ya Wataalam, wazungukie hifadhi zote za Taifa na Hifadhi za Wanyamapori ili wahakiki hiyo mipaka na ikibidi wafanye marekebisho na kuwapa kipaumbele wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwamba, kama atakubaliana na ushauri huo atakubali kwamba hili liwe zoezi endelevu kwamba tuseme kila miaka mitano hili zoezi lifanyike kwa sababu idadi ya watazania inaongezeka kwa kasi na mahitaji ya ardhi yatakuwa tofauti? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba baadhi ya Hifadhi za Taifa zimeendelea kuwa na migogoro ya mipaka na wananchi. Kama nilivyosema tena katika jibu langu la msingi, mipaka ya hifadhi za Taifa, iliwekwa tangu hifadhi hizo zilipowekwa kisheria kwa sheria ambazo zilizianzisha.

Azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunalinda hifadhi hizi kwa ajili ya vizazi na vizazi vijavyo; miaka 100, miaka 500, miaka 1000 ijayo bila kujali ongezeko la watu ambao wataendelea kuongezeka katika maeneo mbalimbali.

Serikali itaendelea na utaratibu wake inaoutumia wa kuhakikisha kwamba taratibu za kuendelea na majadiliano na wananchi, kutoa elimu kwa wananchi juu ya mipaka inayozunguka hifadhi hiyo na kwamba wananchi wote sharti waheshimu mipaka ambayo ipo na hifadhi za Taifa hazitakuwa na mpango wa kujipunguza kwa maana ya kugawa eneo kwa ajili ya makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, la pili. Katika utaratibu na ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa, nakubaliana na yeye kwamba zoezi hili la kuendelea kutazama mipaka hii kwa maana ya kuilinda kwa maana ya kuhakikisha kwamba Hifadhi zetu zinahifadhiwa na zinabaki palepale, litakuwa ni endelevu, litakuwa ni shirikishi, litawashirikisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kadiri itakavyowezekana ili tuhakikishe tu kwamba, mipaka ya hifadhi za Taifa inabaki kama ilivyo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu waziri swali linalohusiana na swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002, inalazimu kabla hifadhi ya misitu haijaanzishwa na kuwa halali, inatakiwa itangazwe katika gazeti la Serikali kama tangazo la Serikali la kuanzisha hiyo hifadhi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, anijibu hifadhi ya Msitu wa Minyure, katika Jimbo la Singida Magharibi, ambayo ime-cover Kata 5 na imesababisha maelfu ya watu kuondolewa kwa nguvu, imeanzishwa kwa kutangazwa katika gazeti la Serikali la Tarehe ngapi? Mwezi gani? Mwaka gani? Ili tujue kama hifadhi hiyo ni halali?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili ni swali jipya. Na tungeshukuru kama Mheshimiwa Lissu, angelileta kwa utaratibu uliowekwa. (*Makofi*)

SPIKA: Kweli ni swali jipya sana. Naibu Waziri, unaweza kulijibu? Huwezi.

Haya, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atauliza swali hilo.

Na. 102

Kuunda Bodi Kwa Zao La Zabibu

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE aliuliza:-

Zao la zabibu ndilo zao pekee la biashara Mkoani Dodoma, lakini linaonekana linalimwa kama matundapori kutokana na kutokuwepo na chombo rasmi cha kusimamia kilimo hicho kama ilivyo kwa Bodi ya Pamba, Tumbaku, Korosho, na kadhalika.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunda Bodi ya Zao hilo ambalo ni la pekee kwa biashara hapa Dodoma?

(b) Je, ni lini Serikali itawakopesha wakulima wa zabibu, pembejeo na kuweka bei za uhakika ili kuinua kipato cha wakulima na kupunguza tatizo la wananchi wa Dodoma kuwa, omba omba kwenye mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar-es-Salaam?

(c) Je, ni kiasi gani Serikali imepata mapato kutokana na zabibu zinazolimwa Mkoani Dodoma?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania inayo fursa nzuri sana ya kuendeleza zao la zabibu kutokana na hali nzuri ya hewa inayoruhusu zabibu kuvunwa mpaka mara tatu kwa mwaka na kuzalisha hadi tani 30 kwa hekta, hasa ikimwagiliwa maji ikilinganishwa na nchi nyingine kama za Ulaya ambazo zina vikwazo mbalimbali kama vile majira yao ya “*Winter*”. Kwa sasa, wastani wa Kaya 500 huzalisha tani 1,500 za zabibu kwa mwaka na kujipatia jumla ya shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka kwa bei ya shilingi 800 kwa kilo. Mapato hayo yanaweza kuongezeka na yataongezeka kwa kuongeza tija katika uzalishaji na kuongezeka kwa viwanda vya kusindika zao hilo, hususan viwanda vya mvinyo ambavyo kwa sasa hata vilivyopo havipati zabibu zakutosha.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa Sheria Na. 19 ya mwaka 2009 na kuipa Bodi hiyo jukumu la kuendeleza mazao ya nafaka na mazao mengine yasiyo na Bodi likiwemo zao la zabibu. Kwa sababu hiyo, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuunda Bodi ya Zabibu.

Wizara yangu itashirikiana na uongozi wa Mkoa wa Dodoma na Baraza la Kanda ya Kati ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, ili zao hilo nalo liingizwe katika mipango ya Maendeleo ya Bodi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa kuwawezesha wakulima pamoja na wakulima wa zabibu kujenga uwezo wa kupata mikopo kutoka kwenye mabanki. Mfuko wa Pembejeo na Taasisi nyingine za kifedha kupitia asasi na vyama vayo vya ushirika. Kwa mfano, Benki ya *CRDB* tayari imeikopesha *SACCOS* ya Chinangali shilingi bilioni 1.5 zilizowezesha kuchimba mitaro ya zabibu, kununua mbolea na kuchimba kisima cha kumwagilia. Hivi sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo itatoa mikopo kwa wakulima pamoja na wale wa zabibu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inapata mapato yake kutoka kwa wadau wa zao la zabibu kupitia kodi mbalimbali zinazotokana na mauzo ya zao hilo. Kwa mfano, katika mwaka 2010, wakulima waliuza zabibu yenye thamani ya 1,443,026,652/= na Serikali ilikusanya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya 156,526,100/= kutoka kwa kampuni mbili za *Tanganyika Vineyards* na *CETAWICO*.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mkoa wa Dodoma ni eneo kame na linalokumbwa na matatizo ya njaa kila mwaka. Na kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba zao pekee la biashara linalokubali hapa ni zabibu. Na kwa kuwa, tumekuwa tukipata zabibu nyingi kutoka kwa wakulima wa *South Africa*. Serikali sasa ina mpango gani hata wa kupanga bei ya zabibu iwe nzuri, ili wakulima wa Mkoa huu waweze kunufaika na kilimo hicho? (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, wakulima wa Jimbo la Mtera, hususan Kata ya *Mvumi Mission*, wamesafisha shamba lenye ukubwa wa hekari 450. Lakini miaka miwili sasa wanazunguka kutafuta usajili na mrajisi wa Vyama Vya Ushirika, yuko Singida baada ya huyu wa Dodoma kustaafu. Serikali inasema nini kuondoa ukiritimba wa usajili wa vyama hivi ili wakulima wale waweze kusajiliwa na kuaminiwa na mabenki ili waweze kujiletea maendeleo? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lusinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kupongeza juhudi zilizofanywa na wakulima wa zabibu, hasa hawa wa Chinangali. Na nimshukuru aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa juhudi alizozifanya, kuhakikisha wanapata mikopo kutoka kwenye benki ya *CRDB*. Nakushukuru sana Mheshimiwa William Lukuvi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kupanga bei; nimesema bei kwa kawaida inapangwa kutokana na kwanza zao lenyewe lipatikane. Hivi sasa viwanda vilivyopo hapa, kwa mfano *Dodoma Ditillaries*, ambao ndio wanatengeneza mvinyo zile kali, *White Wine and Red Wine*, hata *wine* yao haitoshi, wanapata tani 800 tu kutoka hapa. Kwa hiyo, bado tuna jukumu kubwa kwanza la kuongeza uzalishaji, tuongeze tija katika uzalishaji ili hatimaye zikishakuwa nyingi hata viwanda vya kusindika navyo vitakuwa vingi na bei itaweza kupatikana kwa urahisi na kuwa nzuri zaidi. Lakini nakubaliana nay eye kwamba iko haja ya kuliangalia zao hili kwa sababu ndio zao pekee ambalo linaonekana linaweza likawakomboa wananchi wa hapa. Kuhusu wananchi wa *Mission*, tayari *Mvumi Mission* kule taratibu za kusajili ushirika zinaendelea. Hivi sasa, na ninayo taarifa kabisa kwamba usajili wa *APEX*, Chama Kikuu Cha Ushirika, uko katika hatua za mwisho. Msajili wa Vyama au Mrajisi wa Vyama, analishughulikia jambo hili. Naomba tu tuwasiliane na Mheshimiwa Lusinde, ninaamini ni suala tu sasa la ufuatiliaji kwa sababu, ile *APEX* ambayo inaitwa *AMKOTH*, ambayo itashughulikia vyama vya ushirika vyote vinavyohusu zabibu katika Mkoa huu, inashughulikiwa; mimi ninaamini jambo hili litakamilika katika muda sio mrefu. (*Makofi*)

MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Zabibu za mezani zinahitajika sana nchini na ndizo hizo hasa zinazoagizwa kutoka Afrika ya Kusini. Na kwa kuwa, hapa Tanzania, tunazalisha zaidi zabibu ambazo zinatengenezewa mvinyo kuliko zile za mezani. Je, Serikali kupitia

Wizara hii, ina mpango gani wa kuanzisha kuleta mbegu za bidhaa za zabibu za mezani, ambazo zitatupatia soko la ndani na la Afrika ya Mashariki na vilevile linaweza kupunguza idadi kubwa ya walevi wanaotokana na zabibu ambazo zinazalishwa sasa hivi? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Muhammed Sanya, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana na yeye kwamba *Tanzania Distillaries*, sasa hivi inaagiza mvinyo kutoka *South Africa*, kutokana na upungufu wa zabibu hapa. Na ninakubaliana na yeye kwamba kweli bado hatujafikia kiwango kinachotakiwa kuzalisha mvinyo. Lakini Serikali tayari imeshaanza juhudi hizi, kuhusu kuongeza upatikanaji; kwanza tuanzie hapa hapa Tanzania, hapa Makutupora tunacho kituo chetu cha *research* ambacho kazi yake ni hiyo. Ku-*research* uzalishaji wa zao hilo, miche inayoweza kutoa zabibu ya mezani na ile anayoisema ya makali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuhusu kuagiza miche kutoka nje, sisi hatuzuii kutoka nje, isipokuwa tunachofanya tu ni kuhakikisha kwamba Sheria yetu ya *Plant Protection* iheshimiwe. Hatuwazuwii wananchi kuleta miche, tunachotaka waangalie, wanapoleta miche wafuate taratibu zile ili wasije wakatuletea magonjwa mengine ambayo yanaweza kuathiri hata uzalishaji wa zabibu yetu hapa ambayo tayari kwa taarifa nilizonazo, ina ubora mkubwa sana duniani.

Na. 103

Shirika La NSSF Kuhudumia Wateja Wake

MHE. ABIA M. NYABAKARI aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Shirika la *NSSF* kwa nini isitengeneze utaratibu wa kuwasaidia wateja wake katika kujiimarisha kimaisha wakiwa bado wana nguvu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) tayari lina utaratibu wa kuwasaidia wananchama wake kujiimarisha kimaisha kwa kuwapa mafao ya Hifadhi ya Jamii kama vile ugonjwa, uzazi na kuumia kazini wakati bado wanafanya kazi na baada ya kustaafu hulipwa pensheni ya kila mwezi hadi wanakapofariki. Shirika hutoa matibabu kwa wanachama wake na wategemezi wao watano kwa magonjwa karibu yote bure bila mwanachama kulipia huduma za matibabu hayo. Shirika pia kwa kutambua umuhimu wa kinamama hulipa wanachama wake wa kike mishahara ya miezi mitatu

kipindi wanapopata ujauzito ili kuwasaidia katika kipindi cha kujifungua na kulea watoto wanapozaliwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika *NSSF* husaidia wanachama wake kupata makazi bora kwa kujenga nyumba za bei nafuu ambazo huuzwa kwa wanachama wa shirika na wananchi kwa ujumla. Miradi hii huwawezesha wanachama kupata nyumba za kuishi kwa urahisi wakati wakiwa bado wanafanya kazi. Miradi hii ya nyumba itakuwa endelevu na nyumba zitajengwa katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyonipatia, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kufuatana na hali ngumu ya maisha iliyopo sasa inayowakumbuka wastaafu hao na wengine hufa hata kabla ya wakati wao; je, Serikali ipo tayari kumpa mstaafu huyu posho ya kila mwezi kufuatana na cheo alichokuwa nacho kama aliyeko madarakani sasa kama angestaafu leo?

(ii) Shirika la *NSSF* limepanga mikakati gani ya kumkopesha mteja wake kwa sababu ana kianzio cha kumdhani katika shirika hilo? Je, Serikali ipo tayari kufanya hivyo kwa ajili ya maandalizi ya kustaafu kwa mfanyakazi huyu ili aweze kumudu maisha yake binafsi baadaye?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na ajira, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nyabakari kama ifuatavyo:-

Hili la kwanza kwamba, mfanyakazi au mwanachama ambaye yupo kazini, apewe posho huku akiendelea kupata mshahara wake, sidhani kama ina mantiki, kwa sababu yupo kazini anapata mshahara wake. Hii maana yake ni kwamba; ni akiba ya uzeeni, baada ya kustaafu au baada ya kufariki. Kwa hiyo, ninadhani malengo siyo kumpa mshahara au posho sasa hivi wakati bado anapata mshahara wake akiwa kazini ni baada ya kustaafu. Kwa hiyo, ninadhani hili lingendelea.

Swali lake la pili, ninadhani lina mantiki kwamba, hawa wanachama wangepewa mikopo wakiwa bado kazini ili kuwaendelea. Hili ninajibu kwamba, Shirika letu la *NSSF* nimeliona na ndiyo maana limeshaanza kuangalia uwezekano kwa kupitia *SACCOS* za Wanachama kwenye maeneo yao ya kazi, kuwakopesha kupitia *SACCOS* na hili limeanza kufanyiwa kazi. Lingine ni kwamba, Shirika linaangalia utaratibu wa kuwakopesha wanachama wake waweze kujenga nyumba kwa kupitia katika mamlaka, baada ya mamlaka ya *NSSF* kuweka utaratibu kwamba, tunaweza tukawakopesha Wanachama mikopo ya kujenga nyumba, lakini hii inahitaji utaratibu ambao unatakiwa udhaminiwe au uidhinishwe na mamlaka ya usimamizi na uhibititi wa hifadhi za jamii. Pindi hili likifanyika, *NSSF* itaangalia uwezekano wa kuwakopesha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, yaani michango yao ile iwe ni dhamana ya kuweza kukopeshwa katika mabanki mbalimbali.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, muda, Waheshimiwa bado tuna maswali mawili.

Na. 104

Kuandaa Mkakati Mahususi kwa Vijana Wanaohitimu Vyuo Vikuu

MHE. FELISTER A. BURA aliuliza:-

Kuna vijana wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu na kukosa ajira kwa muda mrefu na kubaki mtaani wakirandaranda:-

Je, Serikali imeandaa mkakati gani mahususi kwa vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuna tatizo la ajira kwa vijana ikiwemo wahitimu wa Vyuo Vikuu. Ili kukabiliana na tatizo hili la wahitimu wa Vyuo Vikuu kuingia katika soko la ajira, Serikali ina mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (i) Kama tulivyoona kwenye Bajeti ya Mwaka 2011/2012 na hata Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016), umeweka suala la kukuza ajira kama moja ya vipaumbele vitano vya Mpango huo wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, vipaumbele vingine kama vile kilimo, nishati, viwanda na miundombinu, vinatoa pia fursa kwa vijana, wakiwemo waliomaliza Vyuo Vikuu, kuajiriwa na kuajiriwa.
- (ii) Kuendelea kuboresha Sekta ya Elimu na Mafunzo ili iweze kutoa wahitimu wenye taaluma zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira na hivyo kufanya wahitimu wengi kuwa na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira. Sambamba na hili, Serikali imeendelea kuboresha mitaala kwa kuhimiza vyuo kuingiza masomo ya ujasiriamali; lakini ni vyema pia wanafunzi wanaoingia Vyuo Vikuu wakasoma soko la ajira ili kuchagua fani ambazo zinahitajika zaidi kwenye soko la ajira.
- (iii) Kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye sekta zenye uwezo wa kutoa ajira zaidi ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuwekeza kwenye sekta mbalimbali na hivyo kufanya vijana wengi wanaohitimu elimu ya juu waweze kuajiriwa.

- (iv) Kwa kupitia Wakala wa Huduma za Ajira, *Tanzania Employment Services Agency (TAESA)*, Serikali imeendelea kuwaunganisha watafuta kaza na waajiri.
- (v) Kuanzisha mfumo wa taarifa za soko la ajira ili kuwezesha watafuta kazi, pamoja na wahitimu wa Vyuu Vikuu, kufuatilia taarifa za mahitaji ya soko la ajira na kuwaunganisha na waajiri.
- (vi) Serikali inaandaa Programu za Kukuza Ajira kwa Vijana ya Miaka Mitano (2011 – 2015), ambayo inalenga katika kuwapatia vijana wakiwemo wahitimu wa Vyuu Vikuu na Elimu ya Juu, fursa za ajira, za kuajiriwa na kujajiri wenyewe. Programu inalenga katika kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali pamoja na upatikanaji wa mikopo nafuu na nyenzo za kufanyia kazi.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba, Serikali imetumia pesa nyingi sana kuwasomesha wanafunzi hadi Vyuu Vikuu na wanapomaliza Vyuu Vikuu na kubaki mitaani wakirandaranda pasipo na kazi ni hasara kubwa kwa taifa letu:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuna haja ya kuondoa dhana ya uzoefu, yaani *experience*, nafasi zinapotoka katika Idara za Serikali na Mashirika ya Umma kwamba lazima mtu awe na *experience* ya miaka kadhaa ndiyo apate kazi? (*Makofi*)

Kwa kuwa mfumo wa elimu katika nchi yetu, mfumo wa elimu ya Vyuu Vikuu katika nchi yetu hauko wazi kutayarisha wahitimu kurudi vijijini na kukabiliana na changamoto ambazo zipo katika vijiji vyetu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kurekebisha mitaala kuanzia Shule za Sekondari, Elimu ya Vyuu vya Ufundi na Vyuu Vikuu ili wanafunzi hao wanapomaliza basi waweze kukabiliana na changamoto ambazo zipo? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, tena ujibu kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

La kwanza, ninakubaliana naye kabisa kwamba, hii dhana mpaka mtu awe na uzoefu wa miaka kumi ndipo apate kazi, imepitwa na wakati kutokana na vijana wengi kuwepo wanaotoka vyuoni moja kwa moja. Serikali imeamua kwamba, itanza kuwahamisha wajaajiri na kuweka taratibu ambazo zitawezesha vijana au matangazo ya kazi yasiwe na kipengele hiki cha kutaka uzoefu wa muda mrefu ili vijana wetu wanaomaliza wapate kazi haraka.

Pili, ninakubaliana naye kwamba, mitaala yetu inabidi irekebishwe na ninadhani Serikali imeanza hili kuanzia Vyuo Vikuu. Suala la kuingia mpaka sekondari ili masomo ya ujasiriamali ya kuwafanya vijana wajue namna ya kujitegemea mara wanapomaliza masomo, ni muhimu sana na Serikali itaendelea kulizingatia. (*Makofi*)

Na. 105

Ukandamizaji na Udhalilishaji Dhidi ya Wanawake Nchini

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Wanawake ambao ni asilimia 51.3 ya Jamii ya Watanzania wanakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo umaskini, kubaguliwa katika mgawanyo wa rasilimali na kazi, ukatili dhidi yao, pamoja na matatizo ya mirathi:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kubadilisha Sheria ya Mirathi ya Kiserikali ya Mwaka 1865 pamoja na Sheria za Kimila zinazowakandamiza wanawake na kuwanyima haki za msingi?
- (b) Je, Serikali imeweka mkakati wa kutokomeza mila na desturi za makabila yanayokandamiza na kuzalisha wanawake?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Wadau wengine, tumeshaainisha na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kiserikali ya Mirathi, Sheria ya Urithi ya India ya Mwaka 1865 na Sheria za Kimila Zinazowakandamiza Wanawake, pamoja na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Mapendekezo ya marekebisho hayo, yalishawasilishwa kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria kwa hatua inayofuata.
- (b) Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ya kutomeza mila na desturi za makabila zinazokandamiza na kudhalilisha wanawake ni pamoja na kurekebisha baadhi ya sheria zinazokandamiza wanawake na au kutunga sheria zinazolinda haki za wanawake. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, yaani *The Sexual Offences (Special Provisions) Act (SOSPA)* ya 1988; Sheria za Ardhi za Mwaka 1999, Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi (*Land Disputes Settlement Act*) ya 2004 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009. Aidha, Serikali

itaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha Wananchi kuondokana na mila na desturi zenye kukandamiza na kuwadhalilisha wanawake.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na mafupi ya Mheshimiwa Waziri, ninapenda kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa Tume ya Nyalali ya Mwaka 1992 ilibainisha kuwa Sheria ya Kimila ya Mirathi inapingana na haki za binadamu; je, Serikali haioni kuwa kwa kuchelewesha kufanya marekebisho ya sheria hizi inavunja baadhi ya vifungu vya Katiba ya nchi? (*Makofi*)
- (b) Sheria ya Mirathi ya Kimila inatumika kwa asilimia 85 ya jamii ya makabila ya Tanzania na imetafsiriwa katika mahakama zote za mwanzo; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni muda mrefu sasa umepita tangu marekebisho hayo yalalamikiwe na wanawake wengi wa nchi hii; ni lini sasa Serikali italetwa Bungeni ili sisi tuweze kupitisha sheria mpya itakayolinda haki za wanawake wajane na watoto? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Sheria za Mirathi za Kimila zinazotumika katika nchi yetu, zinabagua kwa kiasi kikubwa wajane na watoto wa kike. Nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna maamuzi ya mahakama ambapo imetamka kwamba, sheria zote zile, *aspect* za sheria za kimila ambazo zinapingana na haki za wanawake hazipo *operational*, tuna maamuzi ya Jaji wa Mahakama Kuu, Jaji Mwalusanya. Kubwa, wakati tunajiandaa kurekebisha sheria hizi, ninaomba nitumie Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge, wahamasishe wanawake na wanaume waandike wosia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wosia ndiyo njia ya haraka sana itakayowalinda wanawake na watoto wetu wa kike katika mirathi na ninawaomba wanawake hasa walio vijijini, wawabane wanaume kwa sababu *experience* wenye mali ni wanaume; tuwabane waume zetu waandike mirathi ili tuweze kuwalinda watoto wetu na wake zetu pindi tutakapofariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni lini sheria hii italetwa Bungeni; niseme kwamba, Sheria za Kimila zinahitaji mjadala mkubwa sana, kwa sababu zinagusa mila na tamaduni za watu. Kwa hiyo ni lazima Serikali ikusanye maoni kutoka kwa Wadau. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya CCM ni sikivu, tumeliweka hili katika Ilani yetu ya Uchaguzi na kabla ya mwaka 2015 tutakuwa na Sheria nzuri ya Mirathi, inayolinda haki za wanawake na watoto wa kike. Ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mnataka muanze kuandika mirathi sasa hivi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita sana na maswali yenyewe yamekwisha. Leo mbele yetu tuna wageni, ninaomba tusikilizane, Mheshimiwa Naibu Waziri hebu kaeni. Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni kutoka Bunge la Vietnam. Wageni wote waliopo pale nilikuwa na maneno ya ki-Vietinis lakini nimeyasahau, tulikuwa wote nimesahau. Tuliwahi sisi wenyewe kwenda huko kama Bunge letu wakati wa Bunge la Tisa, pia aliwahi kuja Naibu Spika wa Bunge la Vietnam kipindi kile. Sasa na hawa nao wamekuja angalau tuanzishe uhusiano rasmi kati ya Bunge letu na Bunge la Vietnam. *(Makofi)*

Majina yao ni hesabu kweli kweli, lakini nitamtaja kiongozi wao anaitwa Mr. Fan Min Tunyen ni *Member of Standing Committee of the National Assembly*, wakati huo huo ni *Chairman of the Board of Deputy Affairs, Deputy Affairs ni House*, halafu ni *General Secretary of Election Council na Head of the Working Group*. Wameongozana na Balozi wao aliyeko hapa, Balozi Yuhén Deupien. Wote watakuwa na mazungumza na Kamati ya Mambo ya Nje, watakuwa na mazungumzo na mimi, pia watakwenda kutoa heshima kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, tunawakaribisheni sana; *feel at home*. Ninajua hata nikisema Kiswahili sawasawa tu, kwa sababu Kiingereza na wao ni kama sisi. Kwa hiyo, ninawakaribisha sana, muweze kujisikia nyumbani na tutakuwa pamoja baadaye kidogo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 38 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi Ignatius iliyopo Dodoma; wako wapi na walimu wao; asante sana.

Tuna wanafunzi wengine 60 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Amani, hawa ni Dar es Salaam; wako wapi na walimu wao, asante sana tumefurahi kuwaoneni, someni kwa bidii.

Wageni wengine wote, mnakaribishwa tunaokoa muda. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kutoa taarifa kwamba, kesho hatutakuwa na kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu. Sababu ziko wazi kwamba, Waziri Mkuu huyo huyo kesho hiyo hiyo inabidi awasilishe Hotuba yake. Hata siku za nyuma, kama Waziri anasoma siku ile tulikuwa pia hatumwulizi maswali. Kutokana na maswali kuwa mengi mno na bahati nzuri Mawaziri karibu wote wana *Deputy Ministers*, wanaweza kujibu. Kwa hiyo, kesho hatutakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu, tuta-move kifungu kinachohusika. Tunaendelea, Katibu kwa ajenda inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011 (The Finance Bill, 2011)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja, Naibu Waziri. Kabla hujaendelea, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, wanaombwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, wakakutane sasa hivi katika Ukumbi Na. 231, ninadhani kukutana na wageni. Kwa hiyo, mnaruhusiwa mwende sasa hivi.

Mheshimiwa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba Wajumbe wake wakutane saa saba katika Ukumbi Na. 227, saa saba. Mambo ya Nje, ninaomba mkakutane na wageni sasa hivi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011 (*The Finance Act, 2011*), pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote, ambao walichangia katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali, niliyoiwasilisha Bungeni, Siku ya Jumatano, tarehe 8Juni, 2011 na kupitishwa na Bunge lako jana.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Vilevile ninawashukuru Wadau mbalimbali katika Sekta ya Fedha, Biashara na Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla, ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kutekeleza kisheria, hatua kadhaa kuhusu mfumo wa kodi, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya ushuru, ada na tozo mbalimbali, kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kufanyia marekebisho sheria 12 zinazohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru, kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali. Kuhuisha ndani ya sheria za kodi, misamaha ya kodi inayotolewa chini ya sheria za uwekezaji na kurahisisha ukusanyaji na ulipaji wa kodi ili:-

Kwanza, kudhibiti misamaha ya kodi iliyotolewa kupitia sheria ambazo hazina uhusiano na masuala ya kodi.

Pili, kupunguza gharama kwenye vipuri vya vifaa vya kilimo ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Kilimo Kwanza, kwa kuongeza uzalishaji kwenye Sekta ya Kilimo.

Tatu, kuongeza fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Nne, kuwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kukusanya kodi kwa wakati na kuweka adhabu ya ulipaji tozo na riba kwa kodi inayochelewa kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizo ni kama zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, Sura ya 208;
- (ii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
- (iii) Sheria ya Ada za Magari Yaliyosajiliwa Nje ya Nchi, Sura ya 84;
- (iv) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178;
- (v) Sheria ya Kodi za Mapato, Sura ya 332;
- (vi) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
- (vii) Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya *Petrol*, Sura ya 220;
- (viii) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168;
- (ix) Sheria ya Ushuru wa *Stamp*, Sura ya 189;
- (x) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
- (xi) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Sura ya 82.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Muswada: Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12. Sehemu ya kwanza, inajumuisha vifungu namba 1&2, inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii, ambapo sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2011 isipokuwa kifungu cha 31(11) na kifungu cha 15(4) katika sehemu ya 12 ambavyo vitaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2012.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, tunapendekeza kuondoa sehemu ya pili ya Muswada yenye vingu namba tatu na nne, vinavyopendekeza kurekebisha leseni za biashara, Sura Namba 208, kutokana na hatua za Serikali kuanza utaratibu wa utozaji ada za leseni kuanzia tarehe 1 Januari, 2012 badala ya tarehe 1 Julai, 2011 ili kutoa nafasi kwa Halmashauri kufanya maandalizi kama nilivyobainisha jana katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, utozaji wa ada za leseni utakapoanza tarehe 1 Januari, 2012 utasimamiwa chini ya Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara ya Mwaka 2007, ambayo itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2011 kwa mujibu wa Tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, ninapendekeza kuingiza sehemu mpya ya pili ya Muswada ili kuifanyia marekebisho Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara ya Mwaka 2007, kwa kufuta kifungu cha 15 cha Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara na kukiandika upya ili:-

- (i) Kubainisha kwamba, leseni ya biashara itadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja na pia inaweza kutolewa upya baada ya kipindi hiki kumalizika. Lengo la hatua hii ni kuwezesha ada ya leseni kukusanywa kila mwaka.
- (ii) Kubainisha kwamba, viwango vya ada na leseni vitapangwa na Halmashauri kupitia kanuni zitakazotolewa na Halmashauri husika baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Hatua hii ya utozaji wa ada za leseni itaanza tarehe 1 Januari, 2012 ili kutoa muda kwa Halmashauri kufanya maandalizi ya kutosha.
- (iii) Kuweka sharti kwa Halmashauri kutoa taarifa ya leseni za biashara zilizotolewa katika maeneo yao kwa Waziri anayesimamia masuala ya biashara pindi itakapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuimarisha usimamizi wa kanuni za biashara hapa nchini na kuwianisha ukuaji wa biashara na mapato yanayokusanywa. Aidha, hatua hii itaongeza mapato kwa Serikali za Mitaa na kuongeza uwezo katika kuhimili mahitaji yao. Utekelezaji wa hatua hii, unazingatia Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa Wananchi, yaani *Decentralisation by Devolution (D by D)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu pamoja na marekebisho yake, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba 147 katika vifungu namba 56, 58 na Jedwali la Nne kama ifuatavyo:-

- (i) Kurekebisha kifungu cha 56 kwa kuongeza kifungu kipya cha 56(a) ili kwanza kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa riba kwenye kodi itakayochelewa kulipwa kwa wakati.
- (ii) Kuweka sharti kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kulipa riba pindi itakapochelewesha kurejesha kodi kwa mlipa kodi anayestahili kurejeshewa. Aidha, wakati wa kulipa malipo haya, yatazingatia viwango vya riba vya biashara vinavyotozwa na Benki Kuu ya Tanzania, yaani *The Bank of Tanzania Discount Rate at the Beginning of the Year*.

- (iii) Kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kusamehe riba au sehemu ya riba endapo ataridhika kwa sababu zitakazotolewa.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisha, ninapendekeza kufuta kifungu cha 7(a), kuondoa katika Muswada pendekezo la kutoza ushuru wa bidhaa kwa huduma zitakazotolewa hapa nchini.

Kurekebisha Jedwali la Nne ili kurekebisha kwa kiwango cha asilimia kumi, viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zinazotozwa ushuru huu. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Vinywaji baridi kutoka shilingi 63 kwa lita hadi shilingi 69 kwa lita.
- (ii) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 226 kwa lita hadi shilingi 249 kwa lita.
- (iii) Bia nyingine zote kutoka shilingi 382 kwa lita hadi shilingi 420 kwa lita.
- (iv) Mvinyo uliotengenezwa kwa Zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka shilingi 1,223 kwa lita hadi shilingi 1,345 kwa lita.
- (v) Mvinyo unaotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 utatozwa shilingi 420 kwa lita.
- (vi) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,812 kwa lita hadi shilingi 1,993 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye Sigara kama ifuatavyo:-

- (i) Sigara zisizo na kichungi na zilizotengenezwa kutokana na Tumbaku iliyozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 6,209 hadi shilingi 6,830 kwa Sigara 1,000.
- (ii) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na Tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 14,649 hadi shilingi 16,114.
- (iii) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 26,604 hadi shilingi 29,264 kwa Sigara 1,000.
- (iv) Tumbaku ambayo iko tayari kutengenezwa Sigara *cut filler* kutoka shilingi 13,436 hadi shilingi 14,780 kwa kilo.
- (v) Ushuru wa *Cigar* unabaki asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa za mafuta ya *Petrol* kama ifuatavyo:-

- (i) Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye *diesel* kutoka shilingi 314 hadi shilingi 215.
- (ii) Kuongeza ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya taa kutoka shilingi 52 hadi shilingi 400.30. Lengo la hatua hii ni kama ifuatavyo:-
 - (a) Kuondoa tofauti iliyokuwepo baina ya bei ya *diesel* na bei ya mafuta ya taa.
 - (b) Kudhibiti uchakachuuji wa *diesel* ambao hufanywa na wafanyabiashara kwa kuchanganya *diesel* na mafuta ya taa ili kujipatia faida kubwa kwa kuwa kodi au bei kwenye mafuta ya taa ni ndogo sana.
 - (c) Kurekebisha shughuli za kiuchumi hususan usafirishaji wa mafuta kutoka Tanzania kwenda nchi za jirani za Rwanda, Burundi, Kongo na Zambia na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Hivi sasa baadhi ya nchi hizi zimesitisha kununua mafuta kutokea Tanzania kutokana ubora hafifu wa mafuta hayo unaotokana na uchakachuuji unaofanyika nchini.
- (iii) Kuongeza mapato ya Taifa yanayopotea kwa kiasi kikubwa kutokana na uchakachuuji wa mafuta.
- (iv) Kupunguza gharama za uzalishaji viwandani na usafiri hapa nchini.

Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo, yaani *Heavy Finance Oil* kutoka shilingi 80 hadi shilingi 40 kwa lita ili kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa hapa nchini. Aidha, punguzo hili limezingatia ahadi ya Serikali iliyotolewa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 wakati nikiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha mwaka huo kwamba, Serikali itapunguza ushuru huu hatua kwa hatua hadi kuufuta kabisa ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 50 badala ya 120 kwenye mifuko ya plastic za *micron 30* na zaidi, yaani *Polymazor of Ethylene* na nyinginezo za *HS Code 3923.2900*.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya aina hii ni malighafi muhimu viwandani kwa ajili ya kutengeneza vifungashio vya kuhifadhia bidhaa muhimu za viwandani na hospitalini kama vile dawa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ada za Magari Yaliyosajiliwa Nje ya Nchi, Sura ya 84 kupitia Jedwali la Sheria hii ili kuruhusu ulipaji wa ada ya magari kutoka nje ya Tanzania, kwa kutumia Shilingi ya Tanzania au fedha za kigeni zinazoweza kubadilishwa katika Shilingi ya Kitanzania kwa mujibu wa taratibu za Benki Kuu ya Tanzania, yaani *any convertible currency*. Hivi sasa Sheria inaruhusu ulipaji wa ada husika kwa kutumia Dola ya Kimarekani pekee.

Mheshimiwa Spika, aidha, lengo la marekebisho haya ni kurahisisha ulipaji na ukusanyaji wa ada za magari kutoka nje ya Tanzania na kuhimiza matumizi ya shilingi ya Tanzania kwa malipo yanayofanyika ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura Namba 178 ili kuongeza vyanzo vya mapato ya Bodi ya Mikopo Tanzania, asilimia nne ya tozo ya maendeleo ya ufundi stadi. Lengo la hatua hii ni kuongeza fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kama ifuatavyo:-

- (i) Kurekebisha kifungu cha 7(3) ili kwanza kuongeza aya namba (j) ili kusamehe Kodi ya Mapato kwenye posho wanazolipwa Wafanyakazi wa Hospitali wanapotoa huduma kwa wagonjwa hospitalini. Msamaha huu unahusisha posho wanazolipwa kwa kutoa huduma za ushauri wa madaktari, wauguzi, maabara, upasuaji, uchunguzi wa wagonjwa na dawa, yaani *Intramural Private Services*.
- (ii) Kuongeza aya namba (k) ili kusamehe Kodi ya Mapato kwenye posho wanazolipwa Wafanyakazi wa Serikali na wanaofanya kazi kwenye Taasisi za Serikali zinazopata ruzuku kutoka kwenye Bajeti ya Serikali. Aidha, posho zitakazohusika na misamaha hii ni hizi zifuatazo; posho ya nyumba, posho ya usafiri, posho ya matibabu, posho ya madaraka, posho ya kazi za ziada (*extra duty allowances*), posho ya saa za ziada (*overtime*) na posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu.
- (iii) Kurekebisha kifungu cha 69(h) ili kutoza Kodi ya Mapato kwa huduma za matangazo ya ving'amuzi inayotolewa hapa nchini kwa kutumia mitambo iliyopo nje ya Tanzania. Pendekezo hili litaiwezesha Serikali kupata mapato kutoka kwenye makampuni yanayorusha matangazo haya na kuweka ushindani sawa na makampuni ya aina hii yanayoweka mitambo hapa nchini.

- (iv) Kurekebisha kifungu cha 90 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) ili kufuta kodi ya zuio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi kwa kutumia ndege za nje ya Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha mauzo ya Samaki nje ya nchi na kukuza viwanda vya samaki hapa nchini. Hivi sasa ndege zinazotua nchini kwa ajili ya kusafirisha samaki nje ya nchi, hutozwa kodi hii tofauti na nchi jirani za Kenya na Uganda, ambapo ndege za aina hii hazitozwi kodi.
- (v) Kurekebisha Jedwali la Pili linalohusu misamaha ya Kodi ya Mapato kwa kuongeza aya mpya za (o), (v) na (w) ili kuhuisha ndani ya Sheria ya Kodi ya Mapato inayotolewa chini ya Sheria za *Export Processing Zone* na *Special Economic Zone* ili kuratibu na kudhibiti misamaha hii chini ya Sheria za Kodi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama ifutavyo:-

- (i) Kurekebisha kifungu cha 8(1) kwa kuongeza aya namba 'N' ili mamlaka ya miji kuwa na mamlaka ya kutoza katika maeneo yao, ada ya leseni ya biashara zitakazotolewa chini ya Sheria ya Usajiri wa Shughuli za Biashara ya Mwaka 2007.
- (ii) Kurekebisha kifungu cha 9(1) kwa kuongeza aya namba 'J' ili kuzipa uwezo mamlaka za vijiji kutoza ada ya leseni ya biashara katika maeneo yao zitakazotolewa chini ya Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara ya Mwaka 2007.
- (iii) Kuongeza kifungu kipya cha 67(a) ili kutoa msamaha wa kodi na tozo zinazotowa na Serikali za Mitaa kwa mazao yanayozalishwa katika maeneo ya Ukanda Maalum wa Mauzo ya Nje ya Nchi. Lengo la hatua hii ni kuratibu na kudhibiti msamaha huu chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mtaa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, inapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 7(4) cha Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli, Sura 220, ili kuruhusu ulipaji wa tozo za mafuta kwa kutumia Shilingi ya Tanzania au fedha ya kigeni inayoweza kubadilishwa katika Shilingi ya Kitanzania kwa mujibu wa taratibu za Benki Kuu ya Tanzania, yaani *any convertible currency*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Sheria inaruhusu ulipaji wa kodi husika kwa kutumia Dola za Kimarekani pekee. Aidha, lengo la hatua hii ni kurahisisha ulipaji na ukusanyaji wa kodi hii na kuhimiza matumizi ya Shilingi ya Tanzania kwa malipo yanayofanyika ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 95(9) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168, ili kuongeza ukomo wa kiwango cha faini inayotowa kwa makosa ya usalama barabarani

(*Traffic Notification Fee*) kutoka shilingi 20,000 hadi 30,000. Lengo la hatua hii ni kuongeza adhabu kwa watakaovunja Sheria za Barabarani ili kupunguza ongezeko la ajali za barabarani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Jedwali la Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189, kama ifuatavyo:-

- (a) Kusamehe ushuru wa stempu wakati wa uhamisho wa mali ndani ya maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi na maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya mauzo ya nje. Lengo la hatua hii ni kuhuisha ndani ya Sheria ya Ushuru wa Stempu, misamaha ya ushuru wa stempu inayotolewa chini ya Sheria ya Kusimamia Maeneo ya Uwekezaji wa Mauzo ya Nje, Sura ya 373 (*Export Processing Zone Act*) ili kudhibiti misamaha kupitia Sheria za Kodi na hivyo kuimarisha uwekezaji katika maeneo haya.
- (b) Kusamehe ushuru wa stempu wakati umiliki wa mali (*assets*) unapohamishiwa kutoka Chombo Maalum (kampuni) cha kutengeneza, kusimamia uzalishaji wa kipato (*special purpose vehicle*), kwa madhumuni ya kutoa dhamana zinazotegemea mali husika ambayo umiliki wake umehamishwa. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha Miradi ya Uwekezaji inayohitaji fedha nyingi; kwa mfano, Miradi ya Barabara, Madaraja, Nishati na Maji. Aidha, hatua hii ni njia mbadala ya mabenki ya upatikanaji wa fedha za kugharimia miradi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na moja, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisha ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Sura ya 148, kama ifuatavyo:-

- (a) Kurekebisha Kifungu cha 16(5) ili kupunguza muda wa madai ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka kipindi cha mwaka mmoja kilichopo hivi sasa hadi miezi Sita. Hatua hii inatokana na kuanza kwa matumizi ya mfumo wa *electronic fiscal devices*, ambao umefupisha muda wa uhakiki wa madai ya walipa kodi, ambapo hapo awali ulikuwa unachukua muda mrefu. Lengo la hatua hii ni kuondoa uwezekano wa walipa kodi kudai marejesho ya kodi zaidi ya mara moja kwa kutumia stakabadhi moja.
- (b) Kurekebisha kifungu cha 17 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (6) ili kutoa adhabu kwa wakaguzi wa mahesabu ambao watabainika kula njama na walipa kodi na kughushi hati ya uhalali wa madai ya kodi. Wakaguzi wataobainika kutenda kosa hili watafungiwa kutoa huduma za ushauri kwa walipa kodi. Lengo la hatua hii ni kupunguza ukwepaji kodi unaotokana na kughushi nyaraka hizi.

- (c) Kuongeza kifungu kidogo cha 17(a) ili kuanzisha utaratibu wa marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye mauzo ya rejareja kwa bidhaa za ndani zinazouzwa kwa abiria wasio raia wa Tanzania, wanaosafiri nje ya nchi. Utaratibu huu utaanza kutekelezwa kwa kuanzia na Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere na Kilimanjaro, kwa mauzo ya thamani ya shilingi 400,000 na zaidi. Aidha, utekelezaji wa utaratibu huu mpya utaanza rasmi tarehe 1 Januari, 2012.
- (d) Kurekebisha Jedwali la Pili linalohusu bidhaa za huduma zinazosamehewa kodi (*exempt supplies and imports*) kama ifuatavyo:-
- (i) Kurekebisha aya ya 8(2) ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kuuza na kupangisha majengo ya kuishi ya nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*). Huduma ya uuzaji na upangishaji wa nyumba za kuishi inatozwa kodi pindi mpangaji au mnunuzi wa nyumba anapolipia pango au kununua nyumba zinazomilikiwa na watu binafsi. Kwa kuwa *NHC* inafanya biashara sawa na watu binafsi walio katika biashara ya majengo; ni dhahiri kuwa nayo inastahili kutozwa kodi huduma hii ili kuondoa ubaguzi baina ya wapangaji wa nyumba binafsi na wapangaji wa nyumba za *NHC*, ambao wengi wao wana uwezo wa kifedha.
 - (ii) Kurekebisha aya ya (9) kwa kuongeza aya ndogo ya (9) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwa michango ya pensheni inapowasilishwa kwa mwajiri au mwajiriwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hivi sasa Sheria haikuweka bayana endapo michango hii inastahili msamaha inapowasilishwa na wahusika katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.
 - (iii) Kurekebisha aya ya (13) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye chakula cha kuku na *scopelet feet*. Hatua hii ina lengo la kuhamasisha uwekezaji katika ufugaji wa kuku hapa nchini.
 - (iv) Kurekebisha aya ya (17)(a) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyuzi (*nylon fishing twine*), zinazotumika kutengeneza nyavu za kuvulia samaki. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji na kuendeleza Sekta ya Uvuvi hapa nchini.
- (e) Kurekebisha Jedwali la Tatu linalohusu unafuu maalum wa kodi (*Special Relief*) kama ifuatavyo:-

- (i) Kufuta aya ya (8) na kuiandika upya ili kwanza, kutoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), kwa makampuni ya madini yenye mikataba na Serikali. Msamaha huu utatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika Mikataba kati ya Serikali na Makampuni ya Madini yaliyosaini Mikataba kabla ya Julai 1, 2009.
- (ii) Ili kutoa msamaha maalum kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT - Special Relief*) kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa madini ambayo msamaha huu utahusisha huduma za bidhaa za utafiti na utafutaji pekee ambazo hufanywa na mwekezaji kabla ya kuanza uzalishaji.
- (iii) Kufuta aya ya (10) na kuiandika upya ili kuondoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT - Special Relief*) uliokuwa unatolewa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*Non Governmental Organisations*), hatua hii haitazihusu Taasisi za Kidini (*Religious Organisations*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*Non Governmental Organisations*), yataendelea kupata msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwa vifaa vya matumizi binafsi ya kawaida (*House Hold Consumables*) hususan vyakula, mavazi na vifaa kama sabuni ambavyo vinatolewa msaada kwenye vituo mahususi vya kulelea watoto yatima na mashule.

- (iv) Kuongeza aya ya 19(b) ili kuhuisha katika sheria hii msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye huduma na bidhaa kama ilivyobainishwa kwenye Sheria za *Export Processing Zones Act* na *Special Economic Processing Act*. Lengo la hatua hii ni kurahisisha utekelezaji wa sheria hizi na hivyo kuimarisha uwekezaji katika maeneo haya.
- (v) Kurekebisha aya ya (32) kwa kuongeza aya ndogo ya (2) ili kutoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT - Special Relief*) kwenye vipuri vya zana za kilimo zifuatazo; fyekeo (*threshers*), mashine za kukausha na kukoboa mpunga (*rice driers and mills*), mashine za kupandia mbegu (*planters*), matrekta ya aina zote, mashine za kunyunyiza na kutifua udongo (*sprayers and harrows*) na mashine za kupanda nafaka (*grain conveyors*).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na mbili, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82, lengo ni kufanya marekebisho katika mgawanyo wa mapato yatokanayo na tozo ya kuendeleza ufundi stadi (*Skills Development Levy*) ya asilimia sita, ambapo asilimia nne zitawasilishwa kwenye Bodi ya

Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na asilimia mbili zitawasilishwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*Vocational Education and Training Authority – VETA*) kama ilivyo hivi sasa. Lengo la hatua hii ni kuongeza fedha za mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika Hotuba ya Bajeti, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia matangazo ya Serikali kwa mujibu wa matakwa ya sheria. Hatua hizo ni pamoja na:-

(a) Kusamehe ushuru wa mafuta ya petroli unaotozwa kwenye mafuta yanayotumika kwenye kuendesha meli na vifaa vingine vinavyotumika katika utafiti wa mafuta na gesi na msamaha huu utatolewa kupitia Tangazo la Serikali. Aidha, maombi ya msamaha yatahakikiwa na kupitishwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu wa gharama kwa makampuni yanayofanya utafiti wa mafuta na gesi.

(b) Kuruhusu makampuni yaa madini kununua mafuta ambayo hayajalipiwa kodi. Chini ya utaratibu huu, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), itafungua Akaunti Maalum (*Extra Account*), ambapo makampuni ya madini yataweka kiasi cha fedha kinachowiana na kiwango cha mahitaji yao ya mafuta kwa mwezi. Aidha, kampuni itaruhusiwa kununua mafuta kwenye matanki ya makampuni ya waagizaji wa mafuta pasipo kulipia kodi kwa kiwango cha fedha kilichoweka kwenye akaunti. Endapo mahitaji ya mafuta kwa mwezi yatakuwa makubwa zaidi ya kiwango cha fedha kilichoweka kwenye akaunti, kampuni husika itawajibika kuongeza fedha za ziada zenye kukidhi mahitaji yake. Hatua hii inatarajia kutatua tatizo la ucheleweshwaji wa marejesho ya kodi iliyolipwa kwenye mafuta.

(c) Kupunguza kwa kiwango cha asilimia 50 tozo zinazotozwa na Mamlaka ya *EWURA*, *SUMATRA* na Shirika la Viwango la Taifa (*TBS*), kwenye bidhaa ya mafuta. Aidha, kwa upande wa tozo za aina hii zinazotozwa kupitia mikataba na hati nyinginezo na Kiwanda cha *TIPER*, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*), mikataba na hati husika, zitafanyiwa marekebisho ili kutekeleza hatua hii ya Serikali.

(d) Kurekebisha wiwango vya ada kwa huduma zinazotolewa na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho niliyoyapendekeza ni utekelezaji wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sasa Waheshimiwa Wabunge, muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria, Bajeti iliyokwishapitishwa hapo jana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Muswada huu, atoe maoni yake. Mwenyekiti, unakaa mbali, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda.

MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007, niweze kutoa maelezo na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011 (*The Finance Act, 2011*).

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mwaka 2011, pamoja na marekebisho yake, yaliyogusa Sheria Kumi na Tatu, umelenga kutekeleza kisheria hatua kadhaa kuhusu mfumo wa kodi, pamoja na kurekebisha baadhi ya viwango vya ushuru, ada na tozo mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, iliyowasilishwa Bungeni tarehe 8 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkullo, Naibu Mawaziri; Waheshimiwa Pereira Silima na Gregory Teu, pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano wa kuboresha marekebisho ya Sheria husika.

Kamati imefanya kazi kubwa pamoja na Wizara hasa ikizingatiwa kuwa, moja ya eneo lililolengwa hasa ni lile la kupunguza ughali wa maisha, unaosumbua maisha ya kila siku ya Wananchi wengi. Hatua zilizochukuliwa ili kufikia lengo hili ni lazima ziwe za vitendo, zinazotekelezeka na zilete matokeo yatakayoonekana.

Mheshimiwa Spika, majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, katika hotuba yake ya kupitisha Bajeti ya Serikali kuhusu eneo la kupunguza ughali wa maisha kwa Wananchi yamegusia maeneo kadhaa. Kwa hiyo, basi Kamati inatoa ushauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako linavyofahamu, Hotuba hii ya Bajeti ilipowasilishwa, lilikuwa ni tukio lililofanyika katika Nchi zote za Afrika Mashariki kwa siku moja.

Hatua hii inaweza ikachukuliwa kama ni utamaduni uliozoeleka baina ya nchi yetu na nchi jirani, lakini mantiki ya utaratibu huu, inaweza kuwa ni mkakati wa ushindani hasa ikizingatiwa kuwa, maeneo ya sheria yanayoguswa yanayohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru na ni mkakati wa Serikali wa kupanga taratibu za kuamsha Mapato ya Serikali.

Vilevile ni njia ya kujenga mazingira ya ushindani kiuchumi, kwani kodi na ushuru ni vivutio maalum vya kuongoza ni jinsi gani ufanisi na tija vinaweza kupatikana katika kutafuta fedha za kuendeshea Serikali, pamoja na fedha za kugharimia Miradi ya Maendeleo yenye uhusiano wa moja kwa moja katika uchumi na huduma za jamii za Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Kodi zenye kero zinazodumaza kukua kwa uchumi, matokeo yake ni kutokuzilipa au kuzikwepa na hivyo kuathiri ujenzi wa uchumi wa tija. Viwango vya kodi, tozo na ushuru vinapopangwa vizuri, walipa kodi watazilipa vizuri na kuiwezesha Serikali kutekeleza Mipango yake ya Uchumi pamoja na huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, eneo moja ambalo linachangia ughali wa maisha kwa wananchi ni bei kubwa ya nishati ya petroli na dizeli. Kamati imekuwa makini sana katika kuishauri Serikali kuangalia jinsi itakavyopunguza bei ya bidhaa hizi. Bei ya petroli na dizeli katika Soko la Dunia ni kubwa. Bei ya petroli kwa mwezi Juni, 2011 hadi kufikia Bandarini Dar es Salaam, ni Sh. 1,222.43 wakati bei elekezi ya rejareja ni Sh.2015.49 kwa lita, na ile ya dizeli ni Sh. 1,239.84 wakati ile ya rejareja ni Sh.2005.03 kwa lita. Hali hii inaashiria kuwa kwanza, maamuzi ya kupunguza bei tulishauri Serikali iyazingatie gharama halisi; pili, tozo zinazotowwa na Taasisi mbalimbali *TPA, TRA, SUMATRA, EWURA, TBS* na *TIPER* zipunguzwe kwa kiwango kikubwa na viwango vikotolewe kwa misingi ya kutumia fedha ya Tanzania ili zisiwe mzigo kwa watumiaji; na tatu, Kamati imeishauri Serikali kuongeza nguvu katika eneo la udhibiti na usimamizi wa biashara nzima ya mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uchakachuaji wa mafuta na lile la kukwepa kodi kupitia *dumping of transit products* ni eneo linaloongeza gharama za maisha. Maeneo haya yakidhibitiwa, mapato ya Serikali yataongezeka na jukumu hili kimsingi ni la *TRA*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa hatua hii na ufuatiliaji wake utapunguza kwa kiwango kikubwa gharama za maisha. Aidha, utaratibu huu vilevile utapunguza tatizo la uchakachuaji wa mafuta ambao umekithiri. Tatizo hili, takwimu zinaonyesha linaipotezea Serikali mabilioni ya shilingi kama mapato yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kutafakari hali halisi ya eneo hili la mafuta, licha ya kuisitiza hoja ya kupanua wigo wa mapato, tatizo linaweza kuwa siyo ufinyu wa vyanzo vya mapato, bali udhaifu katika kukusanya mapato katika fursa zilizopo. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utaratibu wa kuingiza nchini mafuta kwa wingi (*Bulk Procurement*). Kwa kufanya hivi, hatua hii itapunguza gharama za mafuta kwa asilimia 20 hadi 30 pamoja na hatua nyingine zitakazochukuliwa na Serikali, itasaidia kupunguza

kwa kiasi kikubwa gharama za mafuta katika uchumi. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa jitihada zake za kupunguza bei za mafuta pamoja na kukamilisha zoezi la kuweka Kanuni za Kisheria juu ya uendeshaji wa taratibu za *Bulk Procurement*. Aidha, ni vyema Serikali ikaanza kufikiria kuanzisha utaratibu wa kutunisha mfuko wa kugharamia miradi ya umeme vijijini kupitia mapato yatokanayo na kodi za mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za ki-kodi na ushuru ambazo zimepelekea kupunguzwa kwa bei ya mafuta ya dizeli na petroli. Aidha, hatua za kudhibiti tatizo la uchakachujaji pia linapongezwa na Kamati hasa ikizingatiwa kuwa bei zetu za mafuta ni za chini kuliko nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la kuandaa Muswada huu, Kamati imetoa ushauri mbalimbali katika maeneo husika yaliyoainishwa. Sheria ya Leseni za Biashara, sura ya 208 inatarajiwa kufutwa na Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara ya mwaka 2007 mara baada ya Sheria hiyo kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2011 kwa mujibu wa tangazo la Serikali. Kamati imekubaliana na Serikali kuongeza aya mpya itakayoweza Halmashauri kukusanya ada za shughuli za Biashara. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kutokuweka Viwango vya ada itakayotozwa kwa Majiji, Manispaa za Miji, Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Vijiji. Sababu kubwa ya ushauri huu ni kuwa Viwango vya Uchumi katika maeneo haya tofauti vinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri viwango hivi vipangwe na maeneo husika, jinsi yatakavyoona kutokana na tofauti za mazingira na shughuli za uchumi na biashara katika maeneo husika. Hata hivyo, Kamati imetoa onyo na angalizo, mamlaka husika zijiepushe kabisa na kutoza ada za kero na zisizokuwa na tija ili kuondoa usumbufu kwa wananchi na wajasiriamali waliopo kwenye maeneo hayo. Kuwatoza wananchi ada za kero; kwanza, ukusanyaji wake utakuwa ghali na usiokuwa wa tija; pili, utaleta vurugu na malalamiko yasiyo na sababu; tatu, zitafisha na kudumaza ari ya wananchi katika kuchangia nguvu zao katika shughuli za maendeleo.

Uzoefu umeonyesha kuwa mamlaka zinazotoza ada za kero hususan zikiwalenga Mama Lishe wadogo wadogo, wauza mbogamboga gulioni, wale wenye biashara ndogondogo zenye lengo la kuwapatia mahitaji muhimu hasa chakula, kwa utaratibu huu mamlaka zikifanya hivyo utakuwa ni mkakati kwa mamlaka husika kujitengenezea kero. Serikali ifuatilie hili ili kuongeza tija na mapato. Aidha, Kamati imeona kuwa kuzipangia viwango vya ada, mamlaka husika kutoka Serikali kuu inapingana na dhana nzima ya ugatuuji wa madaraka ya maeneo husika. Maeneo haya yapewe uwezo wa kupanga ada kutokana na mazingira halisi ya kiuchumi na jamii yaliyopo huko.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali katika marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, sura 147, ya kuongeza Kifungu kipya cha 56 (a), kuwa haikubaliani na kipengele cha kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kusamehe riba au sehemu ya riba endapo ataridhika na sababu zilizotolewa. Kipengele hiki hakimaanishi uwajibikaji na kinaweza kumletea matatizo mhusika katika kutoa maamuzi pale ambapo hayatakuwa sahihi au yana mashaka. Uamuzi huu ufanywe na

Kamati ili uwe wa uwajibikaji wa pamoja. Aidha, utaratibu huu utaondoa dhana au hisia za rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali juu ya marekebisho ya Jedwali la Nne ili kurekebisha kwa kiwango cha asilimia 10 viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zilizoonyeshwa. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kutokuongeza ushuru wa bidhaa, kwenye bidhaa ya maji ya kunywa yaliyofungashwa. Maji hutumika na wananchi wengi Mijini na Vijijini na ni bidhaa muhimu ya lazima. Bidhaa hii ya maji imesaidia sana katika kupunguza maambukizi ya kutumia maji yasiyo salama katika baadhi ya maeneo nchini na hivyo, kushauri yasiiongezwe viwango vya ushuru.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali wa kutenga asilimia nne ya tozo ya maendeleo ya ufundi stadi kutunisha mfuko wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hatua hii itasaidia wanafunzi wengi wa elimu ya juu kuendelea na masomo yao bila bughudha. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali, kwa vile msisitizo hivi sasa ni pamoja na kuimarisha elimu ya stadi, iangalie vile vile utaratibu wa kutunisha Mfuko wa Vyuo vya *NACTE* – Vyuo vinavyofundisha stadi katika kilimo, uvuvi na mifugo na nyinginezo. Eneo hili lina wanafunzi na wataalamu wengi wanaohitaji kupata mafunzo ya stadi hasa tukizingatia kuwa moja ya kipaumbele katika Mpango wa Miaka Mitano ni kuendeleza raslimali watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa suala la usalama barabarani linategemea sana mafunzo ya usalama na udereva yanayotolewa. Usalama unategemea pia uangalifu na uzingatiaji wa Sheria za Barabara zetu. Kamati imeshauri Serikali kuangalia tena mantiki ya kuleta marekebisho ya faini za trafiki kutoka Sh.20,000/= hadi Sh. 25,000/= ambayo kwa kweli siyo ongezeko kubwa. Faini hizi zinalenga kuongeza mapato na siyo kupunguza ajali. Tatizo kubwa ni usimamizi wa faini hizi na uendeshaji wake haujakuwa wa tija. Yapo mashaka kuwa faini hii ya barabarani, bila kusaidiwa na adhabu kali, inaweza kuchochea upotevu na pia rushwa baina ya wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani na wale wanaosimamia usalama huo.

Mheshimiwa Spika, adhabu, faini na tozo zinaonyesha kuwa kitabu cha mapato cha mwaka 2009/2010, vyanzo hivi vilikusanya mapato ya shilingi bilioni tano, mwaka 2011/2012. Imekadiriwa zitakusanywa shilingi bilioni 8.8. Kiwango hiki ni kidogo na hivyo basi, Kamati inasisitiza Serikali iweke juhudi kubwa katika kuendeleza mafunzo ya udereva, Sheria ya Usalama Barabarani, kuboresha barabara pamoja na kuepuka utoaji wa leseni kiholela. Hayo yaandamane na adhabu kali. Ama sivyo, Kamati vile vile ilishauri kama faini hizi zitasaidia kupunguza ajali, basi ziwekwe kwa viwango tofauti katika magari ya abiria kama mabasi, malori ya mizigo, pikipiki na gari ndogo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni, hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi imejibu mambo mengi ambayo yamejitokeza katika Muswada huu tunaoujadili hivi sasa. Baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina, Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda – Mwenyekiti, Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge na Mheshimiwa Luaga J. Mpina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kasililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi - Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI – NAIBU MSEMaji WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha - Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2011, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (6).

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Fedha na Uchumi wakati akihitimisha hotuba yetu ya bajeti mbadala alisema maneno yafuatayo, nanukuu: *“Kila mtu akitimiza wajibu wake, tunaweza. Tukiacha kuwa Taifa la walalamikaji, tunaweza. Tukiendeleza Umoja wa Kitaifa, mshikamano nakulinda haki za raia, tunaweza. Ninaamini, tunaweza.”* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupitia hotuba yetu mbadala na michango yetu katika Kamati za Bunge na ndani ya ukumbi huu, Kambi Rasmi ya Upinzani tuliweza kushauri na kujenga hoja za kutaka kuondolewa na kubadilishwa kwa mambo mbalimbali yaliyokuwa kwenye hotuba ya Bajeti ya Serikali na ambayo yangeweza kuwatesa wananchi. Hatimaye Serikali imelazimika kuyaondoa. Tumetimiza wajibu wetu kwa kuleta bajeti mbadala, yenye mawazo mbadala na ya Kambi mbadala. Tumethibitisha kwamba tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, tulidai ada za leseni za biashara za Sh. 10,000/=, Sh. 30,000/= na Sh. 50,000/= zilizokuwa zimewekwa na Serikali zifutwe, ili zisiwaumize wananchi wengi wanaofanya biashara ndogo ndogo na hatimaye

Serikali imelazimika kuzifuta. Tuliacha kulalamika na kuidai Serikali iwatendee haki wananchi na hatimaye Serikali imelazimika kufanya hivyo. Tumethibitisha kwamba tunaweza.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kiliongoza maandamano ya nchi nzima yaliyohudhuriwa na mamilioni ya Watanzania katika miji na vijiji mbalimbali vya nchi hii, kudai tozo na kodi mbalimbali katika bei ya mafuta na bidhaa nyingine muhimu zipunguzwe, ili kupunguza ukali wa maisha. Tulijenga mshikamano na wananchi na ndani ya Kambi Rasmi ya Upinzani na hatimaye Serikali imelazimika kupunguza kodi na tozo hizo. Ni matumaini yetu kuwa sasa angalau bei za mafuta zitapungua. Tumethibitisha kwamba tunaweza.

Mheshimiwa Spika, mbali na kupunguzwa kwa kodi na tozo kwenye mafuta kama tulivyotaka, Kambi ya Upinzani inaona bado ipo haja ya kuhakikisha bei ya mafuta inashuka zaidi na zaidi. Tangu mwaka 2008 Serikali ilikuwa inasita kutekeleza kufanya uagizwaji wa jumla wa mafuta (*Bulk Procurement*), lakini kwa kuwa suala hili pia limesukumwa na Kambi ya Upinzani kabla hata ya kuanza kwa Mkutano huu, hatimaye Serikali imelazimika kutekeleza. Tumethibitisha kwamba tunaweza.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa sasa kupitia uagizwaji wa jumla wa mafuta kupitia Shirika la Petroli Tanzania (*TPDC*), wafanyabiashara wa ndani wa mafuta watakuwa wakinunua mafuta katika shirika hilo, hivyo bei atakayonunulia mlaji inaweza kuwa nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, tulipinga ongezeko la faini ya makosa ya barabarani (*Traffick Notification Fee*) kutoka Sh. 20,000/= hadi Sh. 300,000/= iliyopendekezwa na Serikali na hatimaye Serikali imelazimika kupunguza faini hiyo mara kumi hadi kufikia Sh. 30,000/=, tumethibitisha kuwa sisi ni Kambi Rasmi, tunajali haki za watu wetu na kwa hiyo, tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa faini za makosa ya barabarani zimepunguzwa hadi kufikia Sh. 30,000/=, bado Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ipunguze faini hiyo hadi kufikia Sh. 20,000/=, kwani bado kuna ongezeko la Sh. 10,000/= ambalo linaweza kuchochea rushwa.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Serikali ilipata mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 10, kutokana na faini hii ya makosa ya barabarani, lakini katika mwaka ujao wa fedha pamoja na kusudio la Serikali la kuongeza faini hiyo bado itapata mapato pungufu ya shilingi bilioni nane kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali ijikite zaidi katika kuimarisha Sheria na Maadili yanayohusu usalama wa vyombo vya usafiri barabarani, badala ya kutumia faini ambazo zitachochea rushwa na kuongeza makosa ya uendeshaji wa magari barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo tuliyoelezea, Kambi Rasmi ya Upinzani tunapendekeza kifungu cha 23 cha Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2011, kifanyiwe marekebisho kwa kufuta kiasi kipya cha faini ya Sh. 30,000/= na kurejesha kiasi cha faini kilichokuwepo cha Sh. 20,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kupitia taarifa rasmi ya vipaumbele vya bajeti mbadala tuliyoitoa siku chache kabla ya Mkutano huu wa Bunge kuanza, pamoja na mambo mengine, tuliitaka sehemu ya tozo ya kuendeleza ujuzi (*Skills Development Levy*) ielekezwe kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na hatimaye kodi hiyo imeelekezwa tulikotaka, tumethibitisha kwamba tunaweza.

Mheshimiwa Spika, hakika tunaweza. Hiyo ndiyo raha ya Watanzania kuchagua Wabunge wengi wa Upinzani. Kwa kura zao, idadi ya Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeongezeka, na hivyo tumezidi kutimiza wajibu wetu wa kuibana Serikali iliyoko madarakani katika kuhakikisha matakwa na maslahi ya wananchi yanaheshimiwa. Daima hatutarudi nyuma, tutaendelea kupigania wananchi wote wa Taifa hili bila kujali jinsia zao, dini zao, makabila yao na tofauti zao zozote zile.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa heshima na taadhima kubwa, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote kwa kutuchagua kwa wingi kuingia Bungeni katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana. Tunaamini watatupa dola na kutufanya tuwe wengi zaidi mwaka 2015 ili tuzidi kusimamia matakwa yao kikamilifu, kwani bado yapo mambo mengi ambayo Serikali imekataa kuyafanyia marekebisho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (4) cha Muswada huu, kinafanya marekebisho ya Sheria ya Kodi kwa kuongeza kifungu cha 56(a) cha sheria ya kodi, kwa kuweka faini ya kulipa kwa riba iliyopo sokoni ya kodi ambayo haikulipwa kwa wakati pamoja na ziada ya 5%.

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kambi ya Upinzani, tunapendekeza kuondolewa nyongeza ya asilimia tano ya riba hiyo, kwani itatoa mwanya kwa watendaji wa mamlaka za ukusanyaji kodi kutumia vibaya mamlaka yao kunyanyasa wananchi na kujinufaisha wao binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu hicho hicho cha 4 (5), Kamishna wa Mamlaka ya Mapato (*TRA*), amepewa mamlaka ya kutoza faini au kumpunguzia mlipaji riba inayotakiwa kulipwa zaidi kama mhusika atakuwa na sababu ya msingi ya kuchelewa kulipa kodi hiyo (*good cause*).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunataka kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuyawekea mipaka mamlaka hayo aliyopewa Kamishina wa *TRA*, kwani yanampa mwanya wa kufanya upendeleo kwa baadhi ya watu, kunyanyasa au kujinufaisha binafsi kwa sababu tu amepewa uhuru wa kuamua sababu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha (6) cha muswada huu kinafanyia marekebisho Jedwali la Nne la Sheria ya Kodi kwa kuongeza kodi katika bidhaa mbalimbali kama maji na vinywaji baridi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kushusha mfumuko wa bei za vyakula ambao pia unajumuisha maji na vinywaji hivyo. Waziri alishakiri kuwa mfumuko wa bei kwa kiasi kikubwa unasababishwa na ongezeko la bei za vyakula. Kwa hiyo, ongezeko hilo la kodi katika maji na vinywaji baridi, kwa vyovyote vile litasababisha kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika vyakula na maisha kuzidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ongezeko hilo la kodi katika maji na vinywaji baridi na kurejesha kodi iliyokuwepo zamani.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na mtaalam Kankesu Jayanthakumaran wa Australia, kuhusu tathmini ya maeneo maalumu ya uwekezaji kiuchumi, yaani *Export Processing Zone (EPZ)* na *Special Economic Zone (SPZ)* uliochapishwa mwaka 2003, unaonyesha dhahiri kuwa nchi zinazoendelea bado hazifaidiki na uwekezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu ambazo Mtafiti huyo alizitaja kama sababu ya nchi kutokufaidika na uwekezaji katika maeneo hayo ni misamaha ya kodi na nafuu nyinginezo za kifedha. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa misamaha ya kodi ya miaka kumi inayopendekezwa katika vifungu 15, 19, 25 na 31 vya Muswada huu kwamba wapewe wawekezaji katika maeneo hayo, tunataka ifutwe.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 30 cha muswada huu kinafanyia marekebisho jedwali la pili aya ya nane la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwa kuondoa Shirika la Nyumba la Taifa katika msamaha wa kodi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa uamuzi huu wa Serikali utawaathiri sana wapangaji wa nyumba za shirika hilo, kwani kwa sababu ya kutakiwa kulipa kodi hiyo ya *VAT*, shirika litalazimika kupandisha kodi kwa wapangaji wake na hivyo wapangaji wataathirika. Kwa mantiki hiyo, Kambi ya Upinzani tunataka kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuurejesha msamaha wa kodi ya *VAT* kwa shirika hilo ili kodi za nyumba hizo zisipande na kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia ilitarajia Muswada huu uzingatie mapendekezo mengine tuliyoyatoa kwa maslahi ya wananchi, lakini hayazingatiwi. Kwa hiyo, tukiweka mbele maslahi ya Taifa, tunachukua fursa hii kusisitiza tena kuwa mapendekezo hayo yafanyiwe utekelezaji kama ifuatavyo:-

- Tunataka Sheria ya Kodi ya Mapato ifanyiwe marekebisho na kushusha kiwango cha chini kabisa cha kodi ya mshahara (*PAYE*) mpaka 9% na kiwango cha juu

- mpaka 27% ili kuwezesha wafanyakazi wabakiwe na fedha na hivyo kutumia katika uchumi na kukuza uzalishaji;
- Tunataka Kodi katika misitu irekebishwe ili kuiongezea Serikali mapato ya shilingi bilioni 100 kwa mwaka;
 - Tunataka misamaha ya kodi kwa wawekezaji wakubwa ipunguzwe hadi kufikia asilimia moja ili kuipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 658;
 - Tunataka Kodi katika Sekta ya Madini irekebishwe ili kuipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 240;
 - Tunataka Msamaha wa ushuru wa mafuta kwa kampuni za madini uondolewe ili kuipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 59;
 - Tunataka pensheni ya Sh. 20,000/= kwa mwezi tuliyotaka ianze kutolewa kwa kila mzee mwenye umri wa zaidi ya miaka 60, iingizwe katika Muswada huu wa fedha, ili kuwapunguzia ukali wa maisha wazee wetu; na
 - Tunataka posho za vikao (*sitting allowances*) zifutwe katika mfumo wa malipo ya ndani ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka kuona Watanzania wakinufaika na kodi zao na raslimali zao zote walizojaliwa na Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo kazi waliyotutuma, na sasa tumeanza kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa kuwasilisha.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwaeleza kwamba wale watakaochangia Muswada huu, hatuhesabu kama wamechangia mara moja au mara ngapi. Kwa hiyo, tunaanza kuhesabu kuanzia bajeti ile na kesho tunaendelea na Waziri Mkuu. Kwa hiyo, hawa wanaochangia Muswada huu hatuwahesabu kama wamechangia.

Naanza na Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu na wengine nitaendelea kuwataja baadaye.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hii *Finance Act*, lakini kabla sijaanza kuchangia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotoa na niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Fedha na Uchumi, tumefanya nao kazi vizuri sana na haya waliyoyafanya ndiyo ambayo tunakubaliana. Lakini nimpongeze sana Mwenyekiti wangu wa Kamati kwa hotuba yake nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hoja moja ya msingi ambayo naomba sana wenzangu Wabunge walielewe hili. Tunatambua nia nzuri ya Serikali ya kuona namna ya kutatua tatizo la mikopo katika Vyuo vya Elimu ya Juu na tunaunga mkono juhudi hizi. Lakini tunataka tutoe ukweli kwamba unapojenga nyumba, huwezi ukajenga ukuta mmoja, nyumba yenye kuta nne ikasimama. Ni lazima ujenge kuta zote nne ndiyo utaweka paa na utaweka hizo bati. Hoja yangu ya msingi ni kwamba, ni kweli Serikali imeangalia vizuri kwamba ipo haja ya kuondoa tatizo lililopo kwenye Vyuo Vikuu. Lakini Vyuo Vikuu pekee hawatajenga nchi hii peke yao bila kuangalia kada nyingine za katikati na za chini.

Mheshimiwa Spika, labda niseme historia ya *skills development levy*. Hii *levy* huko nyuma miaka ya 1980 na 1990 ilikuwa inaitwa *housing levy* na ilikuwa ni asilimia sita. Lakini ilipoanzishwa *VETA* ikaonekana kwamba ni vizuri asilimia mbili ziende kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana walioko *VETA*. Kwa hiyo, asilimia nne zikabaki kama *housing levy*. Lakini baadaye ikabadilishwa, ikaonekana yote kwa pamoja asilimia sita iitwe *Skills Development Levy* ambayo madhumuni yake makubwa ilikuwa kwanza ni kusaidia vyuo vya *VETA* au *VETA* kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

Pili, ilikuwa ni kusaidia wale wanafunzi ambao wamepitia kwenye mfumo wa elimu, *basic education* kama Darasa la Saba, la Kumi na Mbili, *Form Six* na wengine kutoka kwenye vyuo ili waweze kupata mafunzo ya kwenda kujiajiri kwenye kazi au kuajiriwa. Haya ndiyo yalikuwa malengo ya *Skills Development Levy*. Kwa hiyo, leo hii hali ilivyo ni kwamba *VETA* ina Vyuo 25 katika nchi hii. Kwa msingi huo ni kwamba, hizi fedha za asilimia mbili, wao wenyewe *VETA* bado hazitoshi na wamepeleka maombi mengi sana Serikalini kwamba iongezwe mpaka asilimia nne waweze kuendeleza ujenzi wa Vyuo ambavyo Wabunge wote tumeongelea hapa.

Pili, tunao mpango wa kujenga Vyuo vya Ufundi kila Wilaya na katika hili huu mpango, tegemeo kubwa ni kwenye *levy* hii. Kama ingekuwa imeongezwa kwa wenzetu wa *VETA*, haijaongezwa na taarifa zilizopo Serikali na ndivyo ilivyo haijatenga fedha kwenye bajeti ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi vinavyoendelea katika Wilaya 136. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba kundi kubwa linaachwa, tumeangalia kundi moja. Lakini niwaambie wenzangu kwamba ibada ya Watanzania leo ni wale wanaomaliza kidato cha nne ambao maskini wa Mungu wanamaliza hawana skills zozote zile na maskini wa Mungu siyo wote wanaokwenda Kidato cha Tano, wengi wanabaki. Kwa hiyo, eneo pekee ambalo linasaidia hawa vijana ni kwenda kwenye Vyuo vya Ufundi ili waweze kupata zile *skills* za maisha waweze kuajiriwa kirahisi. Sasa hatujawaongezea fedha, lakini tumepeleka zote kwenye *higher learning institutions*. Hiyo hoja yangu ni muhimu sana na nilidhani Serikali iangalie hilo.

Tatu, ni kwamba ili Mhandisi afanye kazi, ni lazima awe na *technician* ili afanye kazi, ni lazima awe na hawa mafundi stadi na *ratio* ya kimataifa ya Mhandisi mmoja, *technicians* watano na *craftsmen* 25 ndiyo tunatakiwa tuizingatie katika mipango ya kuendeleza elimu. Huwezi ukaendeleza wataalam wa ngazi ya juu Chuo Kikuu peke yao bila kuendeleza wataalam wa kati. Kwa hiyo, sisi tunaona kabisa kwamba tumelenga kutatua tatizo moja, lakini hapa katikati tunapasahau. Sasa daktari akienda kufanya kazi yake, atafanyaje bila kuwa na *nurse*? Bila kuwa na *RMA*, haiwezekani. Kwa hiyo, kama

tunapanga mkakati wa kutoa mafunzo, hii *levy* igawanywe kwa makundi yote matatu na makundi matatu yanayosimamia elimu katika Tanzania, kundi la kwanza ni *Tanzania Commission for Universities (TCU)* huko ndiyo kuna hiyo *Loans Board*, wako pale tumeliangalia vizuri, nalipongeza.

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ni *Vocation Education Training Authority (VETA)*. Hao ndiyo wana asilimia mbili. Lakini kundi la tatu Baraza la Ufundi, *National Council for Technical Education* hawana kitu na ndiyo tunategemea vijana wa *Form Four* waende kule kwenye Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya Uganga, Vyuo vya Ualimu hakuna *levy* yoyote na mimi naomba kuitahadharisha Serikali kwamba kundi hili ni kubwa sana. Linaanza kundi la *VETA*, wale Darasa la Saba na *Form Four* ambao hawana sifa za kwenda Vyuo vya Ufundi ni kundi kubwa, linafuatia kundi la wale ambao wanamaliza *Form Four* wenye sifa nzuri kidogo kwenda kwenye Vyuo vya Kilimo, Vyuo vya Ufundi ambalo ni kubwa sana na kundi la tatu ndiyo hili la Chuo Kikuu ambao. Kwa takwimu nilizonazo, hawawezi kuzidi laki moja, ukichukua *enrolment* ya vyuo vyote. Kwa hiyo, napendekeza kwamba tunaelewa nia nzuri ya Serikali, lakini naiomba hii *levy* ya *skills development* igawanywe katika hizo Bodi tatu kama ifuatavyo:-

Kwamba, wangeacha asilimia tatu ziende *higher learning institutions* kwa maana ya Bodi ya Mikopo, asilimia mbili iende *VETA* lakini asilimia moja iende *NACTE* ambao hawana kitu mpaka sasa hizi na wanavyuo vingi vya ufundi. Lakini tuelewe vilevile kwamba uchumi unakua na uchumi unavyokua, maana yake ni kwamba hata hii *skills development lev*y nayo inakua. Kwa asilimia moja au mbili baadaye inaweza ikasaidia sana kueneza *skills* za vijana wetu wanaosoma katika Vyuo vya Ufundi. Naomba nisisitize, tumelisema kwenye Kamati na Mwenyekiti amelisema, lakini Serikali inaliacha, hili ni bomu baadaye la vijana hawa wa Kidato cha Nne kama hatutaangalia kwa kuwapeleka leo hii, tutakuwa na hali ngumu sana, baadaye tutarudi kukaa humu ndani tutafute sheria namna ya kuwasaidia hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, la pili, naunga mkono maoni ya Kamati kwamba Kamishna asipewe madaraka ya yeye kuamua. Ni vizuri kuwe na Kamati ambayo itafanya hayo maamuzi ili ionekane ni maamuzi shirikishi na kukwepa pengine mianya ya rushwa kama tunavyosema mengine.

Mheshimiwa Spika, sina mengi, ila nasisitiza hilo kwamba tusilimbikize kiporo hiki, leo tumepewa nafasi tuigawe vizuri hii *levy* na tuone umuhimu kwamba inatatumika vipi kwa kizazi kijacho hapo baadaye. Naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu na pia nianze kwa kumpongeza Waziri kwa uwasilishi mzuri na pia Msemaji wa Kamati hii husika jinsi alivyoyaweka mambo vizuri.

Mheshimiwa Spika, jana tulipiga kura hapa ndani kupitisha Bajeti ya Serikali zilitoka "*Hapana*" nyingi kwa nguvu na makofi kupigwa, lakini leo tunasikia tena

kwamba tumeweza katika hoja ambayo jana ilipingwa. Kisebusebu na kiroho papo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata tukiwa wanasiasa wa rangi mbalimbali, lakini mambo ya ukweli ni lazima yabakie kuwa ya kweli. Ingawa pia haishangazi kwa sababu hata vitabu vilishaandika kwamba watakuwa na macho, hawaoni; watakuwa na masikio, hawasikii; lakini wana midomo, wanasema. Kwa hiyo, mimi naomba sana kwamba tuwe waungwana hata kwa nafsi zetu wenyewe, mambo mazuri yanapokuwa yamefanywa na mwenzio, unamwambia hapa hongera. Shetani mpe haki yake hata kama anaitwa shetani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kuchangia mada hii katika eneo la msamaha wa kodi kwenye *Economic Processing Zones* na *Export Processing Zones*. Pendekezo la Waziri anataka msamaha wa kodi wa miaka kumi. Maoni yangu ni kwamba miaka kumi ni mingi sana ikitokea *abuse* na sheria tumeshaweka itakuwa ni vigumu sana katikati kurekebisha hilo jambo na kwa sababu ni pendekezo linaletwa jipya, mimi nadhani tuanze na miaka mitano badala ya kumi. Kuondoa kabisa hatuwezi, *for a simple reasons* kwamba tuko katika ushindani na maeneo haya yana-*attract foreign direct investment*, kwa hiyo, hatuwezi tukafuta kabisa msamaha kwenye eneo hili. Lakini tuanze na miaka mitano na sio kumi moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni hili la *skills development levy* ambayo Mhandisi Mahenge amekuwa analizingumza. Naomba nianze kwanza kwa ku-*declare interest*. Mimi nimepitia mfumo wa elimu yote ya ufundi ya nchi hii. Kuanzia Shule ya Sekondari ya Ufundi, Chuo cha Ufundi Dar es Salaam ambacho sasa kinaitwa *DIT*, Chuo Kikuu fani ya Uhandisi, Shahada ya Kwanza, Shahada ya pili mpaka Shahada ya Uzamivu. Kwa hiyo, ninachokisema nitakuwa nakisema kutokana na uzoefu wangu binafsi na siyo nadharia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Mtumishi katika fani ya Uhandisi kwa miaka 26, ninachotaka kusema hapa ni kwamba namna mabadiliko haya yanavyotaka kuletwa, kwanza yataathiri sana kada ya chini ya kada ya kati ya mafundi na mafundi michundo.

Mheshimiwa Spika, mwenzangu Mheshimiwa Mahenge amesema mabadiliko haya hayazingatii uwiano wa watalaam, nami nakubaliana kabisa. Lakini ninayo hoja nyingine pana zaidi. Ukitazama shida kubwa iliyopo miongoni mwa vijana, ni ukosefu wa ajira, na *formal employment* haitapatikana Serikalini ika-*absorb* vijana wote hawa wanaoingia katika soko la ajira za aina mbalimbali, *formal* na *informal*.

Mheshimiwa Spika, ninazo takwimu za wastani kwamba katika wanafunzi wanaoandikishwa Darasa la Kwanza mpaka kuhitimu, *average* ni asilimia 52 ndiyo wanaoingia Kidato cha Kwanza kwa miaka hii mitatu iliyopita. Kati ya hao wanaofaulu mitihani ya Kidato cha Nne kwenda Kidato cha Tano kwa wastani wa miaka hii mitatu ni asilimia 23, maana yake ukichukua asilimia 23 ya asilimia 52 ya *output* ya Darasa la Saba hiyo inazidi kuwafanya hawa wawe wachache zaidi. Katika hiyo asilimia 23 wanaomaliza *Form Four* ni asilimia 11 ndiyo wanakwenda Kidato cha Tano na cha Sita.

Kwa hiyo, ukiichukua hii ukai-*factor*, huku unazidi kuona kwamba kuanzia wale waliohitimu Darasa la Saba wanazidi kupungua zaidi. Katika asilimia hiyo 11 waliofaulu kutoka *Form Four* kwenda *Form Six* wanaokwenda Chuo Kikuu baada ya hapo na Vyuo vingine vya Elimu ya Juu ni wachache zaidi. Hawa wako katika mfumo rasmi wa mafunzo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, *Skill Development Levy* ilianzishwa kwa ajili ya hawa wanaokuwa nje ya mfumo rasmi. Ukitazama katika hotuba ya Waziri, utaona kwamba pamoja na sheria ilitaka asilimia sita ya hiyo tozo ipelekwe kwenye huo mfuko, Mamlaka ya Elimu ya Ufundi wamekuwa wanapata asilimia mbili tu kwa miaka yote, asilimia nne imekuwa ikibaki Hazina na haikuelezwa wazi kwamba huko Hazina ilikuwa inabaki kufanya nini, haina maelezo mazuri kwamba fedha iliidhinishwa na Bunge itumike kwa ajili ya kuendeleza ujuzi wa vijana, inakusanywa halafu asilimia inabaki Hazina bila ku-*address* tatizo ambalo lilikuwa limelengwa ilitatue. Ndiyo maana mpaka leo bado vijana wengi wapo tu mitaani, wamemaliza Darasa la Saba, wamemaliza Darasa la Kumi na Mbili hawana ujuzi wowote. *VETA* inasuasua katika kukidhi mpango wa Serikali wa kuwa angalau na Chuo cha Ufundi Stadi kwenye kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu, hili ni kosa limekuwa linafanyika. Lakini tunataka kurekebisha lile kosa kwa kutenda kosa linguine. Ninaamini kwamba *two wrongs never make right*. Iko haja kweli ya kuwa na uhakika wa mfuko wa mkopo wa Elimu ya Juu, lakini hiyo haiondoi umuhimu wa mafunzo ya ufundi na ufundi stadi. Jeshi hili linalohitaji hayo mafunzo ni kubwa sana kulinganisha na hawa vijana waliopo katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, tutengeneze tu utaratibu mzuri wa kuwapa mikopo vijana kwenye elimu ya juu, lakini pia ni lazima huu mfuko ubaki kuhudumia walengwa tangu unapoanzishwa, tusiwanyang'anye haki zao hawa vijana wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya wanazo programu mbili sambamba zinazo-*address* tatizo hili la vijana. Vijana wasipokuwa na uhakika na *future* yao kama alivyosema Mheshimiwa Mahenge, ni bomu tunalolikalia juu. Shida kubwa ya hawa vijana ni kwamba wanahitaji wawe na uhakika wa *future*, na uhakika wa *future* yao utapatikana kama watakuwa na stadi za maisha. Sasa tunataka tuwalenge tu hawa wachache waliopata *opportunity* ya kwenda kwenye Vyuo Vikuu na hawa wengine je?

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Waheshimiwa Wabunge kama mnaambiwa m-*set priority*, utawaacha mamilioni bila huduma, bila *certainty* yeyote ya maisha yao ukaangalia hawa laki moja au laki moja na ishirini? Mimi nadhani hii siyo sahihi. Kenya wanachofanya, kuna *KKV* (Kazi Kwa Vijana) na *Kenya Youth Empowering Program*. Kwa bajeti yao ya mwaka huu wametenga mabilioni ya pesa. Mimi ningetegemea sana sambamba na kutoa *portion* ya tozo kuipeleka kwenye mkopo, basi hata *VETA* nayo ingeongezewa. Lakini *VETA* imeachwa na hiyo hiyo asilimia mbili na asilimia nne yote inapelekwa kwenye mikopo ya Vyuo vya Juu.

Mheshimiwa Spika, naomba tubadilisha kidogo, *VETA* waongezewe angalau wapate nusu ya hiyo tozo na tuwa-*task* waendele kupanua Vyuo kwenye maeneo

ambayo leo hayana Vyuo na asilimia mbili iende kwenye Vyuo vya Juu. Asilimia moja ikaimarishe mafunzo ya Ufundi Mchundo.

Mheshimiwa Spika, tumewahi kuona katika nchi hii mafunzo ya kada hizi yanaondolewa ovyo ovyo tu, tukajuta baada ya kuwa tumesha-*adopt* mpango huo, zikaondolewa taaluma za kilimo kwenye Sekondari, Vyuo vya Ufundi vikafungwa, michezo ikaondolewa, tukawa tunajiuliza, hii lengo lake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nina-*declare* kwamba nimepitia mkondo wote huu na nimefanya kazi, kwa hiyo, najua madhara ya kuondoa watendaji wa ngazi hizo katika shughuli za maendeleo.

Naomba sana Waziri atakapokuwa anahitimisha, wafanye haya mabadiliko, hizi fedha zote asilimia nne ile isiende kwenye mikopo ya Elimu ya Juu, isipokuwa zigawanywe kwa *ratio* ambayo naipendekeza, kwamba asilimia tatu *VETA*, asilimia mbili Vyuo vya Juu kwa sababu siyo chanzo pekee kilichopo, walikuwa na chanzo kingine kinachotoa mikopo kwenye Elimu ya Juu na asilimia moja ipelekwe *NACTE* kwenda kusaidia kada ya Mafundi Mchundo.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana tu kutoa mchango mzuri kwa sababu tunategemea uchumi wa nchi yetu unakua kwa hiyo, wale wachangiaji nao wanazidi kuwa wengi. Kwa hiyo, fedha zitakuwa nyingi za kutosha kuhudumia sehemu zote hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimetumia miaka 12 iliyopita nikijaribu kuelewa Sekta ya Madini na matatizo yake. Nimetumia muda wote huo nikijaribu kuelewa kile ambacho nimekiita uporaji wa raslimali za madini ya Taifa letu. Katika miaka 12 hiyo nimeona mengi sana na nimejifunza mengi sana kuhusiana na matatizo makubwa yanayohusu Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho nimekiona na ambacho nataka nikipendekeze leo kuwa ndiyo sababu kubwa ya Taifa hili kutokufaidika na raslimali kubwa ya madini tuliyonayo, ni misamaha mikubwa ya kodi ambayo ilitungiwa Sheria na Bunge hili mwaka 1997 kwa kupitia *Financial Laws Miscellaneous Amendments Act*, kwa kutumia Tanzania *Investment Act*, na mwaka 1998 kwa Sheria ya Madini ya mwaka huo. Hizo sheria tatu zimetengeneza kile kitu ambacho nimekiita katika tafiti zangu utatu usiokuwa mtakatifu, yaani *unholy trinity*

Mheshimiwa Spika, hizo ndizo sheria ambazo zimesababisha jana Waziri wa Fedha amesema kwamba kwa mwaka huu Taifa linategemea kupata mapato ya shilingi bilioni 32 kutokana na raslimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, tumeletewa taarifa ya hali ya Uchumi wa Taifa na imetuambia kwamba kwa mwaka jana peke yake, Sekta ya Madini iliingiza Dola za Marekani bilioni 1,560. Kwa bei ya shilingi elfu moja na mia sita na zaidi kwa dola moja sasa hivi, hicho kiwango cha mapato yanayotokana na madini yetu kitakuwa zaidi ya shilingi trilioni nne, (*give or take*) mahesabu yangu yanaweza yasiwe sahihi sana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ni kwamba nchi hii inaangamizwa na misamaha ya kodi. Taifa letu linaangamizwa na wema huu mkubwa ambao tumewapatia makampuni tajiri yanayotoka nchi tajiri za Magharibi na kutajirika na utajiri wa raslimali kubwa za nchi hii ya madini. Ni sheria, siyo kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ambayo ninayasema, nimeyazungumza sana kama nilivyosema na nimeandikia ripoti mwaka 2008 inayosema: “*The golden opportunity, how Tanzania is failing to benefit from gold mining.*” Sasa leo nataka nisizungumze habari ya tafiti zangu, nataka nizungumze yale ambayo timu mbalimbali za kitalaamu za Serikali yetu zimeyasema kuhusiana na misamaha ya kodi inayoangamiza Taifa hili. Kwa hiyo, nataka nitumie maneno ya watalaam wa Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 wakati Waziri Mkuu wakati huo akiwa Fredrick Sumaye, iliundwa Tume kuchunguza matatizo ya Sekta ya Madini na mchango wake kwa pato la Taifa iliyoongozwa na Dkt. Kipokola, Tume hiyo katika *finding* nyingi ilisema kwamba, Taifa hili linaangamizwa na misamaha mikubwa ya kodi tuliyoyapa makampuni ya madini kwa kuyatungia sheria mwaka 1997.

Mwaka 2005 mara baada ya Mheshimiwa Rais Kikwete kuingia madarakani na kuliambia Bunge kwamba hali ya madini haikubaliki tena, mwezi Januari wa mwaka uliofuata Rais aliunda Tume inayojulikana kama Tume ya Masha, kwa sababu Mwenyekiti wake alikuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Mheshimiwa Lawrance Masha. Mwezi Septemba, 2006, Tume ya Masha iliyohusisha watalaamu wa Wizara 11 za Serikali hii ilitoa *conclusion* ambayo nafikiri ni vizuri nikatumia maneno ya Tume hiyo, walisema: “*there is no win win situation in the mining sector in Tanzania,* kwa sababu ya wema wetu wa kutoa misamaha ya kodi.”

Mheshimiwa Spika, mwaka jana *Society for International Development* yenye Makao yake Makuu London, wametoa taarifa inayosema kwamba katika kipindi cha miaka 10 kufikia mwaka 2008 dhahabu pekee ya Tanzania imeingiza zaidi ya dola bilioni tano, mapato ya Serikali ya Tanzania ni pungufu ya dola milioni mia tatu, kwa sababu ya misamaha ya kodi ambayo Serikali hii na Bunge hili limekuwa linawapa matajiri wa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, nilisema juzi wakati nikichangia Bajeti kwamba sisi ni Taifa ambalo hatujifunzi kutokana na historia yetu, na kwa sababu hatujifunzi kutokana na historia yetu, tutatumbukia katika mashimo ambayo tumekuwa tunatumbukia kwa miaka ya nyuma. *We have not leant from our history, we are condemned to repeat the mistakes of the past.*

Mheshimiwa Spika, leo tunaletewa Muswada wa Sheria unaopendekeza siyo tu kutoa misamaha kwa maeneo maalumu ya uwekezaji *Economic Processing Zones (EPZ) or Special Economic Zones (SEZ)*, lakini vile vile tunapendekeza kuongeza misamaha ya kodi katika Sekta ya Madini, Sekta ambayo kwa kutumia maneno ya Kamati ya Masha imetuweka katika hali ambayo *there is no win win situation*.

Mheshimiwa Spika, tunawaongezea badala ya kuondoa misamaha ya kodi kama ilivyopendekezwa na ripoti ya Kamati ya Jaji Mark Bomani iliyoteuliwa na Rais wetu mwaka 2007 na ikatoa ripoti kwamba misamaha ya kodi kwa makampuni ya madini ifutwe, na Mheshimiwa wangu hapa alikuwepo kama alivyokuwa Mheshimiwa Mwakyembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya kukosa ujasiri, watapiga makofi, watagonga meza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) imesema kwamba makampuni ya madini yaliagiza lita milioni 133 za mafuta ya *diesel*, zimetulipa dola laki mbili kwa sababu ya sheria tulizozitunga kwenye Bunge hili katika miaka ya 1990. Hatujifunzi kutokana na historia yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya aina hii, tutaona lipi? Tumeambiwa tuna macho, hatuoni; katika mazingira ya aina hii, tutasikia lipi? Katika mazingira ya watu ambao hawaelewi walikokuwa jana au juzi, tutafanyaje zaidi ya kupinga? Tutafanyaje zaidi ya kuwaambia Watanzania kwamba katika hali hii *resistance to oppression is obedience to God* kama alivyosema Suzan B. Anthony, aliyefungwa kwa kuwa mwanamke aliyepiga kura wakati Sheria za Marekani zilikuwa zinakataza wanawake kupiga kura. Alisema katika mazingira ya aina hii *resistance to oppression is obedience to God*.

Mheshimiwa Spika, tumefika hatua Watanzania inabidi tupinge mambo ya aina hii ili tumtii Mungu. Tunapendekeza misamaha kwa *Special Economic Zones*. Nilikuwa nasoma, kuna makala hapa ya Profesa *Howard Stein* wa Chuo Kikuu cha *Michigan Ann Arbor (Africa Industrial Policy and Economic Processing Zones)*, anasema, rekodi ya nchi za kiafrika katika maeneo ya uwekezaji maalum, *generally* imekuwa *failure*, hawatengenezi ajira, hayatengenezi fedha za mapato ya Serikali, yanatajirisha yale ambayo tayari ni matajiri. Sisi kama Taifa lisilojifunza kutokana na historia, kama Serikali isiyojifunza kutokana na makosa ya nyuma, tunapendekeza tuwape hawa misamaha zaidi ya kodi kwa miaka kumi ili watajirike zaidi, na sisi tuwe dampo la takataka za viwandani zinakotoka kwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya aina hii *resistance to oppression is obedience to God*. Nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waandishi wa Habari, kama mnataka nakala za Hotuba, naomba mwende kwenye Idara inayohusika ya habari kwa sababu mimi Mezani iko ya kwangu tu

inayonihusu, haiwezi kutoka nje. Kwa hiyo, mwende Idara ya Habari mtapata *documents* zote mnazozitaka.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuhitimisha hatua muhimu ya Bajeti ya Serikali katika kuangalia hatua mbalimbali ambazo zitaongeza mapato na zile ambazo ni za kusimamia uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Niwashukuru sana wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Baridi Magharibi, kwa kuendelea kuwa na imani na mimi. Tuko pamoja katika kutafuta maendeleo ya Jimbo, maendeleo ya Wilaya yetu, Maendeleo ya Mkoa wetu mpya unaokuja. Lakini kubwa zaidi maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiwasikiliza baadhi ya wachangiaji humu, utadhani kwamba hali ngumu ya maisha ya Watanzania ni kana kwamba Serikali kikwazo chake ni kutokuwa na dhamira au kutokuwa na sera. Lakini ndugu zangu ni vizuri tu kama viongozi wa nchi hii tukatambua kama ukuaji wa uchumi wa nchi yetu bado ni mdogo haya yote tunayoyasema hayawezi kufanikiwa. Ni vizuri sana tunaposimama na kutoa ushauri, uwe ushauri wa kweli na wa dhati ambao kweli utaikwamua nchi hii kwenda mbele. Hotuba hizi za kufurahishana sidhani kama zitatusaidia katika kujenga uchumi huu. Naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Waziri wa Fedha kwa bajeti hii ya mwaka huu na hasa katika eneo muhimu ambalo Kamati ya Fedha na Uchumi ilishauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni-*declare interest* yangu, mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Tumefanya kazi nzuri sana na Wizara ya Fedha na watalaam wao, tumeuliza maswali ya msingi na ndiyo maana sura ya bajeti ambayo sasa tunaanza kuhitimisha katika kupitia Muswada huu, imekuja katika sura hii. Napongeza sana Serikali kwa upande wa mafuta ya taa na *diesel*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na uoga kidogo kwa eneo la mafuta ya taa kwa kipindi kirefu, lakini tunajua na tunafahamu kwamba mwananchi wa kawaida pamoja na kwamba Serikali ililenga imsaidie, lakini imekuwa hatunufaiki na punguzo hilo la kodi. Wamenufaika wafanyabiashara wachache wasio waadilifu kwa kufanya biashara ya kuchakachua. Sasa biashara hii inafika mwisho na ninaamini mapato ya Serikali ambayo yalikuwa yanavuja kupitia utaratibu huu, yatasaidia sana katika kuongeza mapato ya Serikali na hivyo basi, kuiwezesha Serikali kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeongea sana suala zima la kutumia jiografia ya nchi yetu kama kichocheo cha maendeleo ya nchi yetu. Sasa eneo hili ndiyo lilikuwa kikwazo kikubwa. Juzi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, niliwasikia Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani wakiunga mkono wazo hili. Mimi naamini tuko pamoja. Lakini kilichonishangaza jana, ni pale walipoanza kuikataa Bajeti ya Serikali kwa kusema *no*. Naheshimu uamuzi wao, lakini ndiyo nasema, ni sura mbili hizi ambazo kwa binadamu

hasa unapokuwa kiongozi watu wanakushangaa. Tunataka turejeshe imani ya nchi zinazotuzunguka na zinazotegemea Bandari ya Dar es Salaam katika kuagiza na kutoa shehena zao kwenda nchini mwao.

Kwa hiyo, hatua hii tuisimamie vizuri. Lakini pia twende mbali zaidi tuangalie pia sheria ya *EWURA* tuweze kuona uwezekano kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati, tuangalie uwezekano wa kuongeza adhabu katika hao ambao wanakiuka utaratibu huo. Ikibidi anayepatikana na kosa hilo tusiishie kumpa faini tu, ikibidi hata tufilisi maghala yao, vifaa vyao ili liwe fundisho. Huu ndio uchumi tunaongelea Bila mafuta, hatuwezi kusema kwamba uchumi tutausukuma kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kufuta kodi ya zuio kwa usafirishaji wa samaki za nje kwa kutumia ndege za nje. Tumelisema sana suala hili, nilikuwa nashindwa kuelewa ugumu ulikuwa wapi mpaka usafirishaji wa samaki kutoka Mwanza tunafahamu ulikuwa umekwisha, watu wanasafirisha samaki kwa magari kwenda Nairobi. Pengine tuwe wepesi katika kuyaona, maana wafanyabiashara wamekuwa wakiishauri Serikali. Lakini nashukuru kwamba limekuja pamoja na kwamba limechelewa. Naamini itatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimbie kidogo. Mimi naungana sana na aliyosema Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, sipendi kurudia. Serikali isikie kilio hiki, tunaweza tuka- *re-align* ile asilimia ambayo tunataka iende, lakini lazima kada hizo na ndiyo maana ilianza kwa msingi huo. Haiwezekani leo, kwa sababu tuna tatizo la kupata fedha kwa ajili ya mikopo ya vijana wanaosoma Chuo Kikuu, sasa ndio tubadilishe tufanye *u-turn* kusahau hiyo, tutakuwa tunafanya makosa makubwa sana. Serikali iendele kutafuta njia nyingine ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaokwenda Vyuo Vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumelisemea hili kwenye Kamati na kusema historia ya suala hili la maji kutotoza, maana naanza kuona Serikali inaanza, ni kama kwenye soda, vinywaji baridi, bia, sasa inaanza kwenda kwenye maji ionekane kama ndiyo *source* kubwa ya mapato ya Serikali. Mimi nasema, *is a wrong trend* na ni vizuri tukasema hapana.

Mheshimiwa Spika, wewe unajua kule kwako vijijini ndani kabisa miaka kumi iliyopita ilikuwa huwezi kukuta mwananchi wa kawaida anakunywa maji ya chupa. Vile vile kwa wananchi, Wabunge wote mliopo hapa mimi nasemea ya kwangu ya Bariadi najua sana. Leo unakwenda kila kijiji, kila kitongoji mwananchi yule yule anakupatia maji safi, salama ya chupa. Ndiyo maana kiafya magonjwa sijui mnaita *airborne diseases*, nini kwa Kiswahili? *waterborne diseases*, maana yanatokana na usafi, maji yaliyo safi na salama. Naishukuru sana Serikali, kwa hiyo, uamuzi wa *bulk import* ya mafuta ni uamuzi mzuri sana upande wa Serikali. Lakini natoa angalizo kwamba hatutaweza kuona faida yake mara moja kwa sababu pale Kurasini *Oil Jet* ambapo meli hizi zinaleta mafuta hayo, kiwango cha mzigo wa meli ni ndogo, huwezi ukaleta pale meli ya zaidi ya tani 40,000 huwezi. Sasa unaleta mzigo wa mafuta lakini pale kuna meli zinaleta mafuta ya kula. Msongamano wa meli.

Lakini tuna uamuzi mwingine mzito wa kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kuingiza *MW 160*. Limo kwenye *speech* ya Waziri wa Fedha. Sasa haya yatatumia mafuta ya mitambo *HFO*, tutaongeza msongamano wa pale kwenye *KLJ* katika kupakua mizigo. Kwa hiyo, tusitegemee kwamba hili tutalipata haraka. Lakini jibu ambalo lipo ni lile boya la mafuta au *tank rage* ambapo tukilikarabati, tukajenga jipya tutaweza kuleta meli kubwa kuanzia tani 80,000 mpaka 200,000 hapo ndiyo mtapata *economies of scale* mara moja. Tuelekee huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa utaratibu wa kusamehe ushuru wa mafuta ya *petrol* unaotokana na mafuta yanayotumiwa na vyombo vya kutafuta *gas* na mafuta. Ndugu zangu tunapongelea haya masuala tuwe tunayajua. Nimewasikiliza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wakichangia kwamba Mheshimiwa Hayati Mwalimu hakutaka madini na *petrol* yaendelezwe hadi hapo Watanzania tutakapokuwa tumeelimika na tuna uwezo wa kuyatafuta na kuyatumia. Hapana jamani, baadhi yetu tumekuwepo tumeshiriki. Mwalimu alikuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana, hawajahi kusema kitu kama hicho.

Mheshimiwa Spika, sera ya kwanza ya kuhuisha Sekta ya Madini na utafutaji wa *petrol* ilifanywa chini ya Uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ndiyo maana tukaja na sheria ya kwanza ile ya mwaka 1979 kwa upande wa madini na sheria ya mwaka 1980 tukaja na sheria ya kutafuta *petrol* ambayo ndiyo inatumika mpaka leo.

Sasa tunapoanza kusema lugha hizo ni za kudanganya watu. Lakini sisi lazima tujue katika ukanda huu ndiyo tunashindanisha makampuni haya, tunayatafuta na *Mozambique* na wenzetu hapa wa Kenya. Ningelipenda mtu aje aniambie kwamba katika Mkataba wa *Mozambique* wa kutafuta mafuta na *gas* kwamba *exemption* hizi ambazo Tanzania inatoa eti hawatoi. Mimi nashauri Serikali ya *Mozambique* tukiwa na *common secretariat* nayajua sana yanayoendelea huko, hatuwezi hapa kama viongozi tujifanye kama sisi hatujui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnapionona naongelea sana mambo ya mafuta na madini, watu hawajui *background* yangu. Mimi ni miongoni mwa Watanzania ambao tumenufaika na kusomeshwa na Taifa hili katika maeneo haya.

Bahati mbaya tumefikia muda wa kustaafu, mwalimu alikuwa amejiandaa sana na masuala haya na naiomba Serikali kwa eneo hili tuanze kuwekeza vizuri kama tulivyokuwa tunafanya miaka ya 1970 na miaka 1980. Najua *effort* hii inayoendelea sasa hivi tumepata *gas*, najua tukiweka nguvu zaidi kwa kuyavutia makampuni haya, iko siku moja inshallah tutayagundua mafuta. Lakini tuwe tumejiandaa vizuri, tuwe na watalaam wazuri watakaoweza kuiongoza na kuisimamia sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia *Finance Bill* ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, tunajadili *Finance Bill* kama hatua ya mwisho ya kuhitimisha Bajeti ya Serikali ambayo Mheshimiwa Waziri Mkullo, alihitimisha jana. Ninaomba niipongeze Serikali kupitia Waziri wa Fedha, Serikali imejitahidi sana kujibu hoja za Wabunge, lakini kujibu hoja nyingi ambazo zilitolewa na Kambi ya Upinzani, lakini pia na Wabunge kutoka Kambi hiyo ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ni ya Chama cha Mapinduzi na mimi napongeza kwamba yapo mambo ya msingi ambayo yalitolewa na Kambi ya Upinzani, Serikali imeyakubali. Kwa sababu hii, Serikali ni ya watu, kwa hiyo, haiwezi kupuuza kila kitu ambacho kinakuja. Lakini pia Serikali haiwezi kutekeleza kila kitu au kukubali kila kitu ambacho kinaletwa na Kambi ya Upinzani. Vinginevyo itakuwa siyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, itakuwa ni Serikali nyingine kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kuiomba Serikali baada ya kupitisha Muswada huu leo jioni ijiandae kuhakikisha kwamba bajeti hii inaanza kutumika sawa sawa kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 na kusije kukawa na kisingizio cha kuchelewa kuanza shughuli kwa sababu ambazo hazitaweza kuelezeka kwa sababu tayari tunayo *Finance Bill* ambayo tunaipitisha leo. Tulishaambiwa ilikuwa tofauti zamani *Finance Bill* ilikuja mwishoni kabisa na kwa maana hiyo, ilikuwa inaathiri utendaji wa shughuli za Serikali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo: Nimesoma mabadiliko ambayo yameletwa na Serikali kwenye suala la mafuta. Ni kweli kama alivyotoka kusema Mheshimiwa Chenge kwenye suala la mafuta ya taa kwa kuipongeza Serikali kwa kuongeza kodi, lakini mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kijijini kabisa kule Mbozi Mashariki wananchi ninaowawakilisha asilimia 98 ni wakulima na wakulima hawa labda ni asilimia 0.01 ambao wanatumia nishati ya umeme. Wananchi wengi wanatumia mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, ziko shule mbili hapa, ile inayosema kwamba mafuta ya taa yanawanufaisha zaidi watu wa mijini au wafanyabiashara wakubwa. Lakini pia iko shughuli nyingine kwamba kwa sababu hakuna nishati nyingine ya kutosha kubwa kule kijijini zaidi ya mafuta ya taa, basi mafuta ya taa yanafaa zaidi wananchi wa vijijini na Watanzania wengi zaidi ya asilimia 75 wanaoishi vijijini kuliko hata wale wa mjini.

Kwa hiyo, nataka kwa kweli kuiomba Serikali ongezeko la kodi kwenye mafuta ya taa imekuwa kubwa sana kutoka Sh. 52 mpaka Sh. 400.30 ni ongezeko la Sh. 348.30 kwa lita. Ni kweli ninachozungumza inawezekana nisiwapendeze watu wengine. Lakini nazungumzia suala ambalo wananchi wangu wamenituma. Ni dhahiri kwamba mafuta ya taa yanatumika na wananchi wengi vijijini. Sisi wengine tumesoma kwa kutumia koroboi, mafuta yasingekuwepo na bei ingekuwa kubwa tusingekuwa hapa. (*Makofi*)

Leo wako vijana na wengine wako Shule za Sekondar za Kata wanasomea vibatari ambavyo vinatumia mafuta vya taa. Mafuta haya wanapewa hela na wazazi wao wakanunue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa msimamo wangu siungi mkono suala la kupandisha mafuta ya taa kwa kiwango kikubwa hicho kwa Sh. 348 kwa lita. Naiomba Serikali kwa dhati kabisa iangalie hili tusitumie hoja kwamba watu wanachakachua mafuta, wanatumia mafuta ya taa, maana yake tukisema hivyo, ina maana Serikali imeshindwa kuwadhibiti watu hawa. Tutakuwa tunaleta sababu ambayo siyo ya msingi kabisa. Serikali ifanye kazi yake iwakamate hawa wanaochakachua na wapewe adhabu kubwa na hawatarudia tena kuchakachukua mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeletwa hapa na wananchi, kwa hiyo, lazima tuseme yale ambayo wananchi wangependa tuyaseme, yale ambayo wananchi wanatutuma tuyaseme. Tuiombe Serikali ili mafuta yapunguzwe kidogo kidogo iendeleze kwa dhati kabisa na kwa uharaka kabisa suala la kusambaza nishati ya umeme vijijini, lakini pia na bei ya umeme yenyewe iweze kuwa ni ile ambayo wananchi wengi wanaiweza. Vinginevyo tutakuwa hatuwatendei haki hawa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie ni suala la kusamehe kodi na nilikuwa nimeleta mabadiliko ambayo nitayasema labda jioni kwenye masuala ya *EPZ* na *SEZ*. Mwalimu Nyerere, naomba nim-*quote* aliwahi kusema maneno haya: “Mataifa madogo duniani ni kama vile mwanamke mzuri aliyevaa nguo fupi kwamba huyavutia Mataifa makubwa yenye nia mbaya.” Haya yalikuwa ni maneno ya Mwalimu Nyerere ambayo aliyasema huko nyuma. Mataifa makubwa yanapokuja kwetu na kufanya biashara na sisi sio kwamba yanatupenda sana, hapana, yanatupenda kwa kile tulichanocho, lakini nia ni mbaya, nia sio nzuri hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo kila kitu tunachokifanya, tunataka tutoe msamaha na hapa tunazungumzia *withholding tax* kwenye *foreign loan*, *dividends*, *land payables* kwenye *EPZ* na *SEZ*. Mimi nadhani huruma hii wakati mwingine inatuponza sana. Jana nilikuwa naangalia *television*, kuna binti fulani alienda *DRC* kwa ajili ya kuangalia mechi kule, sisemi kwamba *DRC* ni nchi ya Kizungu au namna gani, lakini *harassment* ambazo wananchi wetu wa Tanzania wanafanyiwa nje wakati mwingine ni kubwa mno, lakini Watanzania tumeendelea na kuwa na roho ya huruma sana. Mimi nadhani tufike mahali, tuna *SEZ*, tuna *EPZ* hebu tuziache, kama kuna watu ambao wanataka kuja, waje lakini tusitoe miaka kumi kwa kuondoa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ni lazima sana na kama ni utamaduni basi tungeanza na miaka mitano, lakini sio miaka kumi. Tulipata tabu katika maeneo mengi ambayo tumesign mikataba na bahati mbaya sana mikataba mingi ambayo inakuja katika Bunge hili haipitiwi na Wabunge. Serikali inaleta mikataba hii wakati tayari kumeshakuwa na makosa, hata tukija kujadili hapa haitusaidii, makosa yanakuwa yameshafanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba katika maeneo ambayo tutaingia mikataba kwenye *SEZ* na *EPZ* tusirudie makosa yaleyale kama ambavyo tumefanya makosa kwenye sekta ya madini, tuseme Serikali ijirekebishe. Mwaka jana tumepoteza zaidi ya shilingi bilioni 27 kama *exemption* kwa ajili ya mafuta kwa ajili ya watu wa migodi na hii

ni *component* moja, ni eneo moja tu la *exemption* ya mafuta, lakini makampuni haya yanachofanya nini, yanatuletea madawati, kudhamini michezo ni kama kutuletea pipi tu wakati wao wenyewe wakichukua vitu vikubwa sana. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyo sikivu basi maeneo haya tuyafanyie kazi, tuyarekebishe ili Watanzania waweze kufaidika na maliasili iliyopo katika nchi hii, vinginevyo hatutaweza kwenda hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nizungumzie suala lingine la kuondoa pia kodi kwenye Halmashauri za Wilaya ambako kutakuwa na maeneo ya uwekezaji kwa maana ya *SEZ*, lakini pia na *EPZ*. Tunasema tunataka tuondoe kodi ili shughuli hizo ziweze kufanyika sawasawa. Ni eneo lingine ambalo naona tutakuwa tunaitwisha Serikali mzigo tena kwa sababu kama tukiondoa zile kodi ambazo zilikuwa zinatozwa na Halmashauri ili kuwapa nafuu wawekezaji katika maeneo haya, maana yake tunataka kusema nini, Serikali ibebe mzigo wa kupeleka ruzuku kufidia vile vyanzo ambavyo vitakuwa vimeondolewa kwa sababu ya kuwepo kwa *SEZ* na *EPZ*. Tunajua mpaka sasa Serikali uwezo wake wa kupeleka pesa kwenye Halmashauri nyingi bado sio mkubwa sana, tunataka tufute vyanzo vya kodi kwenye Halmashauri kwa sababu ya *EPZ* na *SEZ*, kama tunafanya hivyo, Serikali iwe tayari kuhakikisha kwamba vile vyanzo ambavyo tutaviondoa Serikali inavifidia bila kigugumizi kingine tena.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la kodi kwenye sekta ya kilimo. Naiomba Serikali na hili eneo pia nitaishauri Serikali jioni tutakapokuwa tunapitisha Muswada huu Kifungu kwa Kifungu, tuangalie maeneo muhimu ya baadhi ya vifaa ambavyo vinapendekezwa viondolewe kodi. Ukiangalia kwenye sheria, baadhi ya *spare parts* za matrekta kwa mfano majembe hayakuwekwa pale. Bado tunalipia trekta ya tela hata kwa mkulima, unaambiwa uendeleo kulipa kodi ya trekta. Mimi sielewi kama tumedhamiria kusamehe ushuru kwenye dhana za kilimo kwa maana ya kwamba tuweze kwenda sambamba na dhana ya Kilimo Kwanza, inabidi tusamehe kabisa ushuru wa matrekta na vifaa vingine ili tuweze kumsaidia huyu mkulima Mtanzania. Mimi nafikiri sio suala la matrekta tu, lakini yawe majembe ya kukokotwa na ng'ombe na hata majembe ya mkono ambayo Watanzania wengi wanatumia kule vijijini na yenyewe pia yapunguzwe kodi kwa sehemu kubwa sana.

Vifaa vya umwagiliaji kwa maana ya *irrigations*, bado kodi inatozwa kwenye *spare parts* za kwenye mitambo ya umwagiliaji. Kwa hiyo, naiomba Serikali tufikirie pia kuondoa kodi kwenye vifaa vyote vya *irrigation equipment*. Najua kodi yenyewe kwenye *irrigation equipment* ilishatoka lakini bado *spare parts* zake kodi zinaendelea kutozwa na Serikali. Kwa hiyo, naomba katika eneo hilo pia tulifikirie sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo machache, naomba niunge mkono Muswada huu lakini yale maeneo ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi basi yafanyiwe kazi kwa umakini mkubwa ili nchi hii iweze kwenda mbele na sio kupiga hatua nyuma, nashukuru sana ahsante. (*Makofi*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kushukuru sana kwa kupata nafasi hii adimu ya kuchangia Muswada huu wa Fedha.

Kwanza, nianze kwa kuipongeza sana Serikali, Serikali yetu sikivu, Serikali ambayo tumeipa ridhaa tena kwa kura nyingi kuiongoza nchi yetu na nasema hivi kwa sababu hii ni Serikali ambayo imeleta bajeti na bajeti hii imetokana na mpango, maeneo mengi sana ambayo wananchi walikuwa wanazungumzia na sisi Wabunge tulichangia kwa kweli yamezingatiwa. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa sababu uwezo wa kuongoza nchi wanayo na nia katika Serikali inaonekana dhahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, nianze kwa kuchangia Muswada huu kwa kusema kwamba Muswada wa Fedha mara nyingi unagusa sheria mbalimbali ambapo ndani ya zile sheria kuna eneo la tafsiri, ipo haja ya Muswada wa Fedha ukawa na eneo la tafsiri kwa maana kuna maneno mengine ambayo yanatumika ni mapya. Kwa hiyo, *interpretation clause* kwenye Muswada wa Fedha ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, niendeleo kusema kwamba tumekubaliana ni vyema bajeti yetu ikawa ni bajeti inayojitegemea na sio bajeti tegemezi. Tunaposema tusiwe na bajeti tegemezi basi inaenda sambamba na kwamba hata Mikoa, Wilaya na Kata hazipaswi kuwa tegemezi na hivyo ni muhimu sana tukaangalia jinsi ya kupanua wigo wa kuwapa vyanzo vya mapato mbadala ili nchi yetu isiwe tegemezi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na eneo la kwanza *Part Two*, inazungumzia *Business Licensing Act*, imeongeza ada mbalimbali katika ngazi za Halmashauri. Ada hizi ni sahihi, lakini niombe kutoa ushauri kwamba Watendaji wetu wasipotoshe azma hii nzuri ya Serikali. Kwa sababu tunasema Halmashauri ziwe tegemezi, zaidi ya asilimia 50 ya Halmashauri zetu wanategemea ruzuku, vyanzo vya mapato tulivifuta wenyewe kwa kumlenga huyu Mtanzania asiwe anachajiwa kiasi kikubwa lakini kadri tunavyozidi kwenda, tumeona kwamba hizi Halmashauri zinakuwa ni tegemezi mno kwa Serikali Kuu, sasa ni muhimu Halmashauri zikawa na vyanzo vya mapato. Kwa hiyo, vyanzo hivi niombe kusema kwamba viamuliwe na *By Law* za maeneo husika, yaani vile viwango visitajwe na Serikali Kuu. Vipo vyanzo ambavyo vitakusanywa katika vijiji, Wilaya na Miji. Kwa hiyo, Sheria za maeneo husika ndizo ziseme kama ni Kodi ya Majengo *Property Tax*, iwe ni kiasi gani kulingana na uchumi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, pia Watendaji wetu wasituangushe. Watendaji wa Vijiji na wa Kata, wasitumie nia hii njema ya Serikali tofauti na lengo na hivyo Halmashauri ziweke *database* kwamba katika eneo letu tuna *asset* kiasi gani, *property* kiasi gani na tunatarajia kukusanya mapato kiasi gani. Kwa hiyo, hilo litasaidia maana kuna Halmashauri zingine hawana *database*, wanawaachia wale Watendaji wakusanye, sasa ni ngumu kujua amekusanya asilimia 100, 80 ya malengo na kadhalika. Kwa hiyo, tuweke *database*, waangalie wale watu ambao wana uwezo wa kulipa kodi hizo basi jambo hili lifanyike maana ni utaratibu mzuri wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nikienda Sehemu ya Tatu inayozungumzia *Amendment of the Excise (Management and Tariff) Act*, Kifungu cha 6, Kifungu cha 56A(2), kinasema kutakuwepo na *interest* pale mtu atakapochelewa kulipa kodi atapaswa kulipa inasema *interest shall be commercial bank lending rate of the Bank of Tanzania and a further five*

percent per annum lakini baada ya ile *interest* maana yake kutakuwa kuna asilimia tano. Ukienda Kifungu cha 56A(4), inasema tena hiyo *interest* inaweza ikawa *compounded*, maana yake ni kwamba hizi ni hatua zitakazokwenda kuchukuliwa pale mtu atakuwa ameshindwa kulipa kodi anazopaswa kulipa, kunakuwa na *interest*. Sasa wataalamu wanasema kodi na tozo na ada mbalimbali ambazo tunazi-*introduce* zinatakiwa zikusanywe na sio kuweka riba kubwa ili labda mwananchi awe na hofu alipe. Kwa maana hiyo, ni muhimu tukawa na utaratibu mzuri wa kukusanya kodi, ndiyo ushauri wangu. Ukienda nchi za Europe, America huoni utaratibu wa kukwepakwepa kodi hizi za kawaida tena mtu anafurahi anapochangia. Kwa hiyo, tuangalie *best practice* ya ukusanyaji wa kodi hizi, tunaweza tukatamka kodi na baadaye tukatamka riba na riba zikawa kubwa na wakwepa kodi wakawa wengi zaidi. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo ningeomba ushauri uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, Kifungu cha 10, nipongeze azma ya Serikali ya kuamua kutumia aina zote za fedha, unaweza ukatumia *Tanzanian Shilings* lakini pia tunaweza tukatumia *foreign currency* pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inazungumzia Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ambapo inafuta kodi Maeneo Maalum ya *Export Processing Zone* na hapohapo tumezishauri Serikali za Mitaa ziweze kujitegemea, hapohapo tunasema kodi hizi zisilipwe, sasa haya ni mambo ambayo lazima tuyaangalie kiseru, maana tumeshauri *Local Government Authority* zisiwe tegemezi. Kwa hiyo, tujaribu tu kutafakari ni namna gani tunaweza tukaimarisha Serikali za Mitaa zikawa zina vyanzo bora vya kuweza kujijendesha na Serikali zetu za Mitaa zisiwe tegemezi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naomba kuchangia ni pamoja na suala zima la Elimu ya Ufundi, Sehemu ya Kumi na Mbili, imeelezea *Amendment of The Vocational Education and Training Act*. Kwa kweli kundi hili la vijana wetu wanaohitaji elimu ya ufundi kama walivyokwisha sema wengine ni kubwa na kazi hii tumeianza vyema, niipongeze Serikali, lakini hatujafika tunakokwenda. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa na *levy* maalum kwa ajili ya kuendeleza *Vocational Training*, nikichukua takwimu mwaka huu Chuo cha VETA Dodoma, walikuwa wana nafasi kwa mfano 150, maombi yalikuwa 600 maana yake wanachukua watoto 150, hawa 450 tunawapeleka wapi. Kwa hiyo, ni muhimu tukaangalia namna bora ya kuweza ku-*accommodate* kundi hili kubwa la elimu na naomba kushauri kama tulivyotumia ule utaratibu wa *DDH* kwenye hospitali ni pale ambapo Serikali inaingia ubia na sekta binafsi, *Private Partnership*. Ikiwezekana hata kwenye hizi shule za ufundi tuingie nao, tu-*support* yale mashirika ya dini, vyuo kama vya *Don Bosco*, vyuo vya Makanisa, kwa sababu baadhi ya maeneo hatuna majengo ya kuwapeleka watoto mara moja wanapomaliza Darasa la Saba na *Form Four* na lazima wapate elimu, tukiwa-*support* wale watoto wanakwenda kusoma kule kwa hiyo, wanakuwa ni Taifa lililoelimika, vijana wenye nguvu na uwezo kama tulivyofanya katika sekta ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nipongeze sana Muswada huu mzuri na maeneo yote kwa kweli ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipopongeza maeneo muhimu ambayo yamefutuliwa kodi ikiwa ni maeneo ya nyavu za kuvulia samaki, malipo kwa wafanyakazi na waajiri katika mifuko ya hifadhi, kodi upande huo imetolewa, lakini pia nafuu maalum ya kodi kwa vifaa vya kilimo. Vifaa vya kilimo kumekuwa na nafuu ya kodi kwa bajeti hii maana yake ni bajeti inayomuangalia Mtanzania hasa ukizingatia asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutashukuru sana vifaa hivi vikipungua bei, sisi Wanyalukolo kule tunatumia sana majembe, tunaomba bei zipungue, matrekta bei zipungue, JKT SUMA muangalie sana. Vifaa hivi vya kilimo na pembejeo vikipungua bei kwa kweli tutaondokana na umaskini. Kwa haya, kwa kweli niipongeze sana Wizara pamoja na Serikali kwa azma hiyo. Haya tuliyokubaliana ya kupunguza na marejesho yafanyike mara moja kama tulivyokubaliana, Sheria hii inaanza kazi tarehe 1 Julai, 2011. Kwa hiyo, naomba sana vifaa vya kilimo, majembe ya mkono, bei zishuke mara moja, tunapoenda kwa wananchi tukitoka hapa kuandaa mashamba, matrekta na pembejeo zote ziwe ni bei ambazo sisi wananchi tunaweza tukazimudu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa hivi nitamwita Mheshimiwa Amina Mwidau, nadhani tumetamka vizuri jina lako maana ulikuwa unalalamika.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana jina langu umelitamka vizuri sasa hivi, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika *Finance Bill* hii. Mimi nianze kuchangia Sehemu ya Nne ya Muswada huu inayopendekeza marekebisho katika Sheria ya Ada ya Magari ya Nje, Sura ya 84. Kifungu cha 10 cha Muswada kinatoa utaratibu wa kufanya malipo hayo kwa kutumia fedha za kigeni au fedha za Tanzania. Pendekezo langu ni vyema Kifungu cha 10 kikaongeze maelezo ya ziada ili ada ya magari isilipwe tu kama ilivyo sasa hivi kwa kuangalia viwango vya ada kwa kigezo wa uzito wa gari husika na umbali wa gari linapotembea likiwa Tanzania. Ni vyema tozo mpya ya kodi kwa magari hayo iwe itakayoweka ada mpya ya kila siku gari husika litakapokuwa Tanzania, liwe limetembea au halijatembea, lilipiwe ada ambayo inaweza ikaitwa *daily charge for foreign presence in Tanzania*. Hilo ni pendekezo langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Tisa ya Muswada, *page number 15*, naona imechangiwa hata na maelezo ya Kambi ya Upinzani na mimi naunga mkono katika hili. Katika Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 164, pamoja na madhumuni na sababu za Muswada kueleza kuwa ni kutoa adhabu kali kwa watenda makosa ya usalama barabarani. Nimshukuru kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, alipopunguza mpaka shilingi elfu thelathini lakini bado mimi naona ni kubwa ni bora irudi ileile shilingi elfu ishirini kwa sababu hiyo shilingi 20,000 yenyewe kutoa ni tatizo, kuongeza mpaka shilingi 30,000 tunatengenezea ulaji kwa *Traffic* wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukatafuta njia nyingine mbadala za kuweza kuwa na utaratibu mzuri wa usalama barabarani kwa kujifunza hata katika nchi nyingine, sio za nje tu na hata za Afrika kama Botswana. Botswana wana utaratibu nzuri tu ambao unaisaidia pia Serikali kuliko kuongeza adhabu ambayo haitusaidii sanasana ni kutengeneza mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inayopendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura ya 148 ambayo ni *page number 18*. Katika Kifungu cha 31 cha Muswada kinapendekeza kuongezwa kwa Kifungu cha 17(A) katika *VAT Act*. Mapendekezo yangu, Kifungu cha 17(A)(2)(a) kinachoeleza sehemu ya kuondokea Tanzania kwa wasafiri wa nje kuwa ni katika Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage na *Kilimanjaro International Airport (KIA)*, kirekebishwe na isomeke kuwa katika viwanja mbalimbali vya ndege vilivyopo na vitakavyojengwa na eneo lolote lenye mipaka halali ya nchi. Eneo lolote lenye mipaka halali na njia mbalimbali siyo anga tu, bali njia mbalimbali kama anga, reli na barabara.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itoe sababu za kwa nini Kifungu cha 17(A)(4), kinaeleza kuwa Kifungu chote cha 17(A) kitaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2012 badala ya kuanza pamoja na Sheria zingine ambazo zinaanza tarehe 1 Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuchangia Sehemu ya Sita ya Muswada inayopendekeza Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, *page number 12*. Kifungu cha 14 kinachorekebisha Kifungu cha 7(3) ambapo (b) inasema ondoa kituo (*full stop*) mwishoni mwa *paragraph (i)*, pendekezo langu ni vema Sheria Mama, *Income Tax Act* ikarekebishwa kwa kufuta kiwakilishi (*it*) katika Kifungu cha 7(3)(i). Hivyo isomeke, *payment that is unreasonable or administratively impractical* na siyo *payment that it is unreasonable or administratively impracticable*.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ni huo, naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Nashukuru umeniokolea muda. Sasa namwita Mheshimiwa Moses Machali. Nadhani huyu ni mchangiaji wa mwisho.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa fursa hii ili kusudi niweze kuchangia Muswada ulio mbele yetu. Mimi kimsingi mchango wangu ni wasiwasi mkubwa unajitokeza kwenye misamaha ambayo inaendelea kutolewa kwenye makampuni ya madini kupitia bidhaa mbalimbali ambazo wanakuwa wanazitumia katika kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu tumekuwa tukisikia malalamiko ya hapa na pale juu ya misamaha ambayo inatolewa kwenye makampuni ya madini ambayo yanafanya kazi katika migodi mbalimbali hapa nchini. Pia nimepatwa na wasiwasi kwa

kuona kwamba makampuni haya bado yanaendelea kupewa misamaha ya kodi mbalimbali halafu tunakwenda kusema kwamba tunataka tutoze kodi mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo yamekuwa yakisaidia jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ukiangalia lugha hapa iliyotumika kidogo inaleta utata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nitaomba ninukuu. “Kufuta aya ya 10 na kuiandika upya ili kuondoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko ya Thamani uliokuwa unatolewa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali yaani *Non-Governmental Organizations*. Hatua hii haitazihusu Taasisi za Kidi (*Religious Organisations*). Aidha, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, *Non-Governmental Organizations* yataendelea kupata msaada maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vifaa vya matumizi ya kawaida, *household consumables* hususani vyakula, mavazi na vifaa kama sabuni ambavyo vinatolewa msaada kwenye vituo mahsusvi vya kulelea watoto yatima na shule.”

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha wakati akihitimisha hoja yake ajaribu kufafanua huu msamaha maalumu, kuondoa Msamaha Maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwa *Non-Governmental Organizations* ni msamaha gani? Kwa hiyo, nitaomba tuweze kupata ufafanuzi wakati anahitimisha hoja yake kwa sababu tunashuhudia mara nyingi sana mashirika haya yanatoa huduma kwenye jamii. Mashirika haya ni *non-profit organizations* siyo kwamba yanafanya biashara. Sasa inanipa wasiwasi kuona kwamba makampuni ya madini ambayo yanafanya biashara ya madini, yanapata misamaha ya kodi lakini mashirika ambayo hayafanyi biashara ambayo ni *non-profit making organizations*, Serikali inataka kuyatoza kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa unamtoza kodi huyu mtu ambaye ni *service oriented*, ambayo ni *free* kwa wananchi wa Tanzania halafu mtu ambaye anafanya biashara unampatia *tax exemption* sijui hapa tunafanya kitu gani. Naona tunafanya mchezo wa kuigiza hapa. Kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba makampuni haya ya madini hayaendelei kupewa misamaha kwa sababu tukiangalia hata mchango wa sekta ya madini katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu bado haujaweza kuridhisha. Kuna taarifa ambazo siyo rasmi kutoka kwa wananchi mbalimbali hapa nchini, wamekuwa wakiyalaumu makampuni haya kwamba yanatengeneza pesa nyingi sana ikilinganishwa na kiasi ambacho tunabaki nacho sisi hapa nchini sasa bado wanaendelea kupewa misamaha, halafu tunasema tutoze mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, leo labda kwa mfano unasema utamtoza kodi labda *Kigoma Development Initiative* halafu Mashirika ya Kidini pia ukayaacha, sijui tunafanya nini. Kwa sababu sioni tofauti ya asasi ambazo zinaongozwa na madhehebu mbalimbali ya kidini, jinsi gani yamekuwa yaki-*deliver service* kwenye jamii zetu pamoja na *NGOs* za kawaida ambazo zinapatikana huko mtaani. Sasa unasema kwamba huyu umtoze halafu huyu usimtoze, bado hapa inaingia dhana ya ubaguzi, kwa sababu wote naweza nikasema ni asasi ambazo haziwezi kutengeneza faida yoyote. Nitaomba tupate ufafanuzi wa kina katika hili ni kwa nini Serikali bado inataka kuendelea kuyapa msamaha makampuni ambayo yanatengeneza faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Zimebaki dakika 10 naona nitoe matangazo. Nafikiri Kamati ya Mashirika ya Umma, Kamati ya Fedha na Uchumi nadhani na Serikali yenyewe, inabidi wakutane maana kuna Shirika ambalo linaitwa *Consolidated Holding Corporation*, linatakiwa kumaliza kipindi chake tarehe 30 Juni hii, keshokutwa. Shirika hilo halijamaliza kazi zake na kama hatutafanya kazi hii leo, tarehe 30 litakuwa halipo na mtu wa kufanya kazi hakuna. Kwa hiyo, tunakusudia jioni kuleta *a Supplementation Order Paper* ambayo itaonesha nini tutakachokifanya jioni. Kwa hiyo, tukirudi, tutaanza kuwataka wanaohusika waanze kujibu hoja hizi, tuingie kupitisha Azimio hilo. Naomba Kamati inayohusika na Azimio nayo iandike maoni yake na Kambi ya Upinzani ifanye hivyo. Nasikitika muda umekuwa mfupi lakini naamini mnaweza kwa sababu haya masuala ukweli yametokea kwenu zaidi kuliko hata Serikali.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.50 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumesambaza Orodha ya Nyongeza ya Shughuli, msije mkashangaa hii inatokea wapi, Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Randama za Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011,
(*The Finance Bill, 2011*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Nilipositisha shughuli za Bunge asubuhi, nilisema kwamba tutaanza kuwaita watoa Hoja kusudi waweze kutoa ufafanuzi wa maeneo mbalimbali na kama

mtakavyoona kwenye *Order Paper* hii mpya, tuna hilo Azimio muhimu sana ambalo ni lazima tulifanyie kazi leo.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nachukua nafasi hii kumpongeza kwa jinsi alivyoiwasilisha kwa ubora kabisa. Nichukue nafasi hii kuzungumzia kidogo juu ya fursa za uwekezaji zilizopo hapa nchini na ni kwa nini Serikali imeendelea kutoa baadhi ya misamaha ya kodi kama sehemu ya kuwavutia wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Agosti, 1947 nchi ya India ilikuwa imebakiza saa chache kupata uhuru. Kiongozi wake akiitwa Nehurul Jhwalal, akawaambia saa 6.00 usiku India itapata uhuru. Wakati wa hotuba yake, akasema maneno haya ambayo napenda ninukuu.

“Je, sisi Wahindi ni werevu kiasi gani? Ni werevu kiasi cha kutosha kwamba tuzishike na kuzichukua fursa za kupambana na changamoto zilizo mbele yetu kama Taifa?”

Mheshimiwa Spika, kufikia mwakani, nchi ya India inategemewa kuwa na uchumi mkubwa, namba tatu duniani. Nchi yetu ya Tanzania kama tunavyofahamu, tunazungukwa na majirani wengi na majirani wanaitazama Tanzania. Nchi ya Tanzania hadi kufikia hapa tulipo, sio tu kwamba tunahitaji uwekezaji, tunahitaji uwekezaji mkubwa katika viwanda, katika maeneo mbalimbali ambayo tumejiridhisha kwamba ni lazima yawepo ili kuisogeza nchi yetu mbele. Nchi yetu ina *square kilometer* za mraba 945,000 na *population* au ukuaji wa idadi ya watu ni 3% na hadi kufikia mwaka huu tunakadiriwa kufikia watu milioni 41.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwaka jana 80% ya bidhaa zote za *textile*, zilikuwa zinapelekwa nje ya nchi zikiwa hazijaongezewa thamani. Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji mkubwa wa bidhaa za ngozi katika Afrika lakini thamani ya ndani ambayo inawekwa hadi kufikia mwaka jana, ilikuwa ni 10% tu na 90% ya hizo bidhaa zinapelekwa nje pasipo kuongezwa thamani. Hii ni moja ya sababu kwamba nchi yetu ni lazima ifanye kila inaloweza kuongeza thamani na kuweza kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Maeneo Maalumu ya Uwekezaji ya *EPZ* na *SEZ*, *Special Economic Zone*, ambayo yalisemwa na baadhi ya wachangiaji asubuhi, ni maeneo muhimu sana katika uchumi wetu. Kuna mtu alizungumzia habari za tafiti, lakini naomba pia nimwambie tafiti hasa zinasema yafuatay. Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), linasema nchi 120 Duniani hadi kufikia leo zina *EPZ* na zina *Special Economic Zone*. Kutokana na Ripoti ya Benki ya Dunia, inasema nchi ya China imeweza kukua na kuwa na uchumi wa pili Duniani, wa pili kwa ukubwa kutokana na uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Uchumi ya *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, Ripoti hiyo inasema 22% ya *GDP* ya pato la Taifa la China, linatokana na uwekezaji katika maeneo ya *SEZ*. 46% ya *Foreign Direct Investment*, fedha ambazo zinatoka nje moja kwa moja na kuwekezwa katika Jamhuri ya watu wa China, zimewekezwa katika maeneo ya *SEZ*. 60% ya wao kuweza kupeleka bidhaa nje, imetokana na maeneo ya *SEZ*. Watu milioni 30, zaidi ya nusu ya Watanzania katika nchi ya China, wanafanya kazi katika maeneo haya ya Uwekezaji Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jirani zetu hapa Kenya, wana utaratibu uleule wa kuwa na msamaha wa miaka 10 kama ambavyo Tanzania tunao. Itifaki ya Afrika Mashariki, ambayo inaziingiza nchi zote katika umoja wetu huu wa forodha, tumesema kwamba miaka 10 imeruhusiwa kwa mwekezaji maalum kuweza kupewa msamaha wa kodi. 7% ya mapato yote ya Kenya yanayotokana na kupeleka bidhaa nje, yanatokana na *EPZ* sio zaidi ya hapo, 2.2% ya pato la Taifa, linatokana na *EPZ*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 Serikali ya Rais Kikwete, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ilianzisha *EPZ Act*, mwaka 2006 mfumo wa *EPZA* ulianzishwa. Miaka minne baadaye, kuna makampuni 44 ambayo yameanza chini ya huu utaratibu, kuna pesa ambazo zimewekezwa na makampuni haya zaidi ya shilingi trilioni moja ambazo tayari zipo katika utaratibu wetu na Serikali ilitoa mtaji wa shilingi bilioni 20 kuikabidhi *EPZ* na *EPZ* ikatumia bilioni 20 kuvutia uwekezaji wa zaidi ya trilioni moja. Hadi kufikia mwaka jana, zaidi ya dola milioni 355 ilikuwa ni *export value* ambayo ni mauzo ya nchi yetu nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 thamani ya uzalishaji katika maeneo ya *EPZA* ilikuwa imefika takribani dola za kimarekeni milioni 500 au nusu bilioni; 22% ya bidhaa ambazo tunapeleka nje, bidhaa za viwandani zimetokana na *EPZA*. Mwaka 2009 vilevile jumla ya *export* ya Tanzania, bidhaa ambazo nchi yetu ilipeleka nje zilikuwa ni thamani ya dola za Kimarekani bilioni tatu na 3.6 ilitokana na *EPZA*.

Mheshimiwa Spika, watu 13,000 wamepata ajira tunayoita ajira ya moja kwa moja. Watu 50,000 wamepata ajira inayojulikana kama *indirect employment*, ajira inayotokana na hizo ajira za mwanzo. Nchi ya Rwanda mwaka huu, wametuma watu wao kuja *EPZA* kujifunza; wakamwomba Meru, Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA*, aende Rwanda akawafundishe mtindo huu.

Mheshimiwa Spika, misamaha hii ya kodi inatolewa kwa wawekezaji wapya tu. Naomba nirudie na tungeomba Watanzania wafahamu, ni wawekezaji wapya ambao tunawavutia, tukishindana na nchi nyingine zote Duniani, ndio tunawapa fursa hii ya miaka 10 ya uwekezaji. Niseme, huwezi kupata pato lolote au kodi au ajira ambazo hazipo, bila kuwa na huyu mwekezaji ambaye tunamhitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mzee Kenyatta alisema, “*Man eat nothing, society is nothing*”. Wakati mwingine kama huna kitu ambacho unaweza ukala utakuwa na hasara zaidi na msamaha huu wa miaka 10, wataalamu wamesema, unapoanzisha kiwanda, kuanzia mchakato wa kutafuta fedha, kwenda kwenye mabenki na kukopa, kuanza

kujenga hicho kiwanda, kuleta mitambo na kui-*install* au kuiweka, kuanza uzalishaji na hadi kuanza kujiendeleza, kufikia *a breakeven point*, inachukua miaka nane. Miaka miwili tu ndio ambayo inajulikana kama *incentives* ambazo tunawapa wawekezaji. Viwanda vya *Kamal* ambao wameanza kuwekeza karibu na Bagamoyo, milioni 220, wameanza kusema hata hiyo miaka 10 ni michache!

Mheshimiwa Spika, naomba niseme katika nchi ya Kenya, wana utaratibu wa miaka 10, viwanda vyao vimesonga mbele na sisi tunawafukuzia. Afrika Mashariki kama nilivyosema, utaratibu ni miaka 10. Nchi ya Nigeria ni miaka 10, nchi ya Ghana ni miaka 10, nchi nyingine zilizoendelea kama *the Philipines, Malaysia; Malaysia* wana miaka mitano ya *tax holiday* kwa sababu ni lazima wavutie uwekezaji. Nchi ya *Philipines* wana miaka nane. Mwaka 2004 – 2009 chini ya mpango huu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, *TIC – Tanzania Investment Centre*, imeweza kuvutia mitaji, tunaita *Foreign Direct Investment* ya thamani ya bilioni 3.4 za Kimarekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania inazidi kupanda, Tanzania ni lazima tujitahidi kuwavutia wawekezaji. Tanzania ni lazima tufahamu kwamba uwekezaji huu unaleta thamani, unaleta ajira, unaleta ujuzi, unaleta teknolojia na ni lazima tuukubali. Sasa hivi katika bandari yetu ya Dar-es-Salaam tuna uwezo wa ku-*handle* makontena yale yanayotoka katika bandari 400,000 kwa mwaka. Mombasa, wanatuzidi kwa makontena 600,000 kwa mwaka na sisi tunatarajia tupate uwekezaji wa zaidi ya milioni 540 katika Bandari ya Dar-es-Salaam ili tuweze kufikia kuwa na kontena milioni 1.4 ambayo itakuwa ni zaidi ya mara mbili ya bandari ya Mombasa na hapo ndipo tutafikia lengo la kuwa kiongozi katika Afrika ya Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji uwekezaji zaidi ya bilioni 3.5 kuweza kujenga reli ya kati iende Rwanda, iende Burundi. Sasa hivi napozungumza rafiki yangu Zitto, kutokea kule kwake Kigoma, kutokea Mwanza, mizigo yote ambayo inapita katika reli ya kati ni *metric tones* 250,000 tu. Miaka miwili ijayo kampuni ya *Kabanga Nickel* peke yake, ambayo inaanza uzalishaji katika miaka miwili, wameomba *metric tones* 250,000 wenyewe; kwa maneno mengine kampuni moja itachukua mabehewa yote yaliyopo sasa hivi ya reli ya kati. Ni lazima na ni muhimu, nchi hii iendeleo kuwavutia wawekezaji, tuweze kuwashinda majirani zetu, tuweze kuwa mbele nao ili Taifa letu liweze kusonga mbele. Hatuwezi kufanyia siasa au mzaha mambo ya kweli ambayo yanawagusa wananchi, haiwezekani, bila uwekezaji wa kweli, uliosimamiwa vizuri, nchi yetu haitaweza kubadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Ilikuwa ni tarehe 12 Juni, 1981, Mzee mmoja anayejulikana kama Ronald Regan alisimama katika ukuta wa Berlin, kuna mtu mmoja alikuwa anafanya uchawi wa kuzuia zile nchi mbili kuungana, kwa kuzuia maendeleo ya Ujerumani, alikuwa anaitwa bwana Gorbachov. Akautazama ukuta, akasema bwana Gorbachov, vunja ukuta huu! Ukuta huu ni ukuta wa ukweli, mambo ambayo ni lazima wananchi wayafahamu, yanayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba ukuta huu uvunjwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ukweli juu ya kazi ambazo zinafanyika na Serikali hii, ziweze kuwafikia wananchi kwa sababu, mwisho wa yote ni muhimu tukafahamu mapinduzi yanayoendelea katika Mkoa wa Mtwara. Mapinduzi yanayoendelea katika lile eneo la *corridor* ya Mtwara, ni mapinduzi ambayo yataibadilisha Tanzania lakini ni mapinduzi ambayo yanahitaji uwekezaji wa kweli. Miezi mitatu iliyopita Serikali ya CCM imefanikiwa kupata mwekezaji wa takribani bilioni tatu, dola za kimarekani, kwa ajili ya kuwekeza katika Liganga na Mchuchuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme Mchuchuma ina uwezo wa kutoa makaa ya mawe, wanakadiria zaidi ya miaka 400 tutaendelea kuchimba. Nchi ya China peke yake, 80% ya umeme wanaotumia unatokana na makaa ya mawe. Dunia nzima inatumia zaidi ya 50% kutoka makaa ya mawe lakini haiwezekani kabisa bila uwekezaji mkubwa unaosimamiwa na Serikali makini kwamba tukafikia pale tunapotarajia kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, nikushukuru sana wewe, niwashukuru ndugu zetu wa Kambi ya Upinzani wale ambao wanafahamu na wanakubali kuuvunja ule ukuta, ukuta wa ukweli, ili tuweze kuwa pamoja katika mambo yote yenye mustakabali na kuleta maendeleo na maslahi kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja 100% kwa 100%. (*Makofi*)

T A A R I F A

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, Taarifa!

SPIKA: Taarifa!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, Taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8). Napenda kumpa Taarifa rafiki yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwamba wakati Mzee Kenyatta, anasema *man eat nothing, society is nothing* alikuwa anamjibu Mwalimu Nyerere, kwa kuiambia Kenya ni *man eat man society*.

Mheshimiwa Spika, napata wasiwasi aina ya viongozi wa kisiasa tunaowajenga ambapo tunaweza tukatumia maneno ya kejeli ya viongozi wa nchi jirani kumsema Baba wa Taifa. Naomba Mheshimiwa Mbunge, apate hii Taarifa na aifute taarifa yake aliyokuwa ameitoa kuhusu Kenyatta. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ukitoa Taarifa ni Taarifa, Taarifa haiwi ugomvi! Taarifa ikiwa ugomvi ni kitu gani? Taarifa ni Taarifa sio ugomvi. Tunaendelea, Mtoa Hoja!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kutoa shukrani za dhata kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kimaandishi. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Mheshimiwa Christina Lissu Mughway, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Fedha na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Masuala ya Fedha. Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughway Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Mohammed H. Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mbunge wa Gairo, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo na Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Namelok E. Sokoine, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi S. Chana, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyagwine, Mbunge wa Tarime na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhata kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada. Aidha pia napenda kutoa shukrani zangu za dhata kwa Kambi ya Upinzani kwa maoni na ushauri wao. Naahidi kwamba Serikali itafanyia kazi mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Kambi ya Upinzani.

Naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa kuhusu msamaha wa miaka kumi unaotolewa kwenye maeneo ya uwekezaji *EPZ* na *SEZ* kwamba upunguzwe hadi miaka mitano. Namshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara nafikiri amelitolea ufafanuzi wa kutosha. Hata hivyo, nataka nitoe taarifa kwamba marekebisho yanayotarajiwa kufanywa katika Sheria ya *EPZ* siyo mapya wala hayakusudii kutoa mapendekezo ya utungwaji wa sheria mpya. Lengo la marekebisho hayo ni kuhuisha Sheria ya sasa iliyopo ya *EPZ* ili iendane na Sheria nyingine zilizokwishatungwa na Bunge lako Tukufu. Ni ushauri wangu kwamba kama kuna haja ya kufanya marekebisho, basi marekebisho hayo yaelekezwe kwenye Sheria ya *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, suala la ushuru wa bidhaa kwenye maji yaliyofungashwa, maji yaliyokusudiwa kutozwa ushuru wa bidhaa ni maji ya chupa ambayo hutumiwa na watu wenye uwezo. Hata hivyo, maji ya kawaida ya bomba, visima, yanayotumiwa na watu wengi hayatazwa kodi abadani. Hata hivyo, maji ya chupa yanatozwa ushuru wa bidhaa hata katika nchi zote za Afrika Mashariki, ni makubaliano ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni mgawanyo wa *Skills Development Levy*, *TCU*, *VETA* na *NACTE*, taasisi hizi zina majukumu yanayotofautiana. Majukumu ya *NACTE* ni kuratibu elimu ya mafunzo ya ufundi kwa kuhakikisha kwamba elimu ya mafunzo ya ufundi inaendana na mahitaji ya soko la ajira, kuhakikisha kwamba viwango vya ubora wa mafunzo vinatolewa kwenye elimu ya ufundi na mafunzo. Kusajili na kutambua uwezo wa Vyuo vya Ufundi vya binafsi na vya Serikali katika kutoa mafunzo. *NACTE* kama Baraza halina vyuo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, *VETA* inawajibika na utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi wakati Baraza la Elimu ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu linatoa mikopo kwa ajili ya kuwapatia mikopo Wanafunzi wa Elimu ya Juu kulipia ada za shule majukumu ambayo ni tofauti na majukumu ya *NACTE*. Kama *NACTE* inahitaji fedha za ziada, maombi hayo yaletwe Hazina.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu bei ya tozo na ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za mafuta. Baada ya kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa na tozo kwenye mafuta, bei elekezi ya mafuta katika vituo vya kuuzia mafuta itakuwa kama ifuatavyo: bei ya dieseli itapungua kutoka shilingi 2005.03 hadi shilingi 1681.03. Bei ya mafuta ya petroli itashuka kutoka shilingi 2015.49 hadi shilingi 1790.49. Bei ya mafuta ya taa itaongezeka kidogo toka shilingi 1557.67 hadi shilingi 1680.97 kwa lita sawa na ongezeko la shilingi 123.30 kwa lita. Ongezeko la ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya taa ni shilingi 348.3 na shilingi 224.51 ni punguzo la tozo zinazotozwa kwenye Halmashauri kwa mamlaka ya udhibiti.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya tozo ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya dieseli na mafuta ya taa yanasababisha bei zitofautiane sana

ikilinganishwa na bei ya bidhaa hizo katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mfano, bei ya Diesel nchini Kenya ni shilingi 1857.06, Uganda ni shilingi 2131.20, bei ya petroli Kenya ni shilingi 2007.83 na Uganda ni shilingi 2355.20, bei ya mafuta ya taa Kenya ni shilingi 1497.35 na Uganda ni shilingi 1760. Kwa takwimu hizo, bei zinazopendekezwa hapa nchini hazitakuwa tofauti na majirani zetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchukua hatua ya kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa na tozo kwenye mafuta, hatua nyingine za kudhibiti uchakachuuji zitachukuliwa. Nimechukua maoni ya Bunge lako Tukufu za kuhuisha Sheria ya *EWURA* ili iweze kutoa adhabu kali zitakazoongeza nguvu katika kusimamia biashara ya mafuta hapa nchini. Hivyo, tutawasiliana na *EWURA* kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja ya pato la Taifa. Serikali inatoa misamaha ya kodi kupitia Sheria za Kodi na zisizo za kodi kwa nia ya kutoa vivutio vya uwekezaji au unafuu wa kodi kwa wawekezaji na makundi ya watu kwa nia ya kutekeleza sera mbalimbali za Taifa. Ni kweli kuwa misamaha ya kodi inapunguza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa misamaha hiyo ilitolewa kwa nia njema ya kusaidia Serikali kufikia malengo yake ya kuhudumia wananchi, imebainika kuwa misamaha hiyo wakati mwingine inatumika vibaya na hivyo kutoleta mafanikio yaliyotarajiwa. Kwa sababu hiyo, Serikali inaendelea kupitia baadhi ya misamaha ili kuangalia kama bado inahitajika au lah! Hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ili kupunguza misamaha zimeanza kuzaa matunda na kupunguza misamaha kutoka asilimia 4.2 ya pato la Taifa katika mwaka 2006/2007 hadi kufikia asilimia 2.3 ya pato la Taifa katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupitia misamaha hiyo mwaka hadi mwaka ili kuhakikisha kuwa misamaha isiyo na tija inaondolewa, kwa mfano msamaha unaondolewa chini ya Kifungu cha 10, Jedwali la Tatu kinachotoa msamaha kwa *NGOs* na Asasi za hisani, *charitable organization* kimependekezwa kuondolewa mwaka huu. Aidha, Serikali kupitia *TRA* imejipanga kunufaika na Mfuko wa Dhamana wa Ushauri wa Sera na Usimamizi wa Kodi (*Transit Fund for Revenue Policy and Administration for Developing Countries*) ulioanzishwa na Shirika la Fedha Duniani ili kuweza kufanya uchambuzi wa kina na kuangalia upya misamaha ya kodi na kuiondoa misamaha yote ambayo haina tija hasa kupitia upya Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani (*VAT*).

Mheshimiwa Spika, hoja ya kushusha kiwango cha chini kabisa cha kodi mpaka asilimia tisa kutoka asilimia 14 na kushusha kiwango cha juu cha kodi ya mapato asilimia 27 kutoka asilimia 30. Serikali inatambua tatizo la ukali wa maisha linalowakabili wafanyakazi na imekuwa ikijitahidi kutokana na uwezo wake wa kibajeti kuchukua hatua za kupunguza makali hayo. Kwa mfano, imepunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka asilimia 18.5 katika mwaka wa fedha 2006/2007 hadi kufikia asilimai 14 katika mwaka

2010/2011. Aidha, kiwango cha chini cha kutozwa kodi kimeongezeka kutoka mapato ya mwezi ya shilingi 80,000 hadi kufikia shilingi 135,000 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, hoja la pendekezo la kupunguza kiwango cha chini kabisa mpaka asilimia tisa kutoka asilimia 14 na kushusha kiwango cha juu mpaka 27 kutoka 30 ni nzuri. Hata hivyo, inakadiriwa kuwa utekelezaji wa pendekezo hili unaweza kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi ya shilingi bilioni 293,572 milioni katika mwaka 2011/2012. Kiasi hiki ni kikubwa sana na kinaweza kuleta pengo kubwa sana kwenye mahitaji ya kibajeti katika mwaka huu wa fedha. Serikali itaendelea kulifanyia kazi pendekezo hili na kuchukua hatua stahiki kulingana na uwezo wake wa kibajeti mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye uuzaji na upangishaji wa nyumbani za *National Housing Cooperation* urejeshwe. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), huduma ya upangishaji na uuzaji wa nyumba za kuishi unatozwa kodi inapotolewa na mfanyakabiashara aliyesajiliwa na *VAT*. Hivyo ili kuondoa ubaguzi kwa wapangaji wengine ambao nao wangependa pia kupanga kwenye nyumba za Shirika la *NHC*, Serikali imeamua kuondoa msamaha huu. Uamuzi huu umezingatia hali halisi kwamba wapangaji wa *NHC* wana uwezo sawa na wapangaji wa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, marejesho ya *VAT* kwa wasafiri isiwe kwa viwanja vilivyotajwa pekee. Marejesho ya *VAT* kwa kuanzia yataanza kutekelezwa kwenye viwanja vilivyotajwa kwa vile kuna miundombinu ya kurahisisha marejesho hayo. Utaratibu unaendelea ili marejesho hayo yatolewe kwenye viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu Sehemu ya Nne ya Muswada inayofanya Marekebisho ya Sheria ya Kodi kwa kuongeza Kifungu cha 56A cha Sheria ya Kodi kwa kuweka faini ya kulipa kwa riba iliyopo sokoni ya kodi ambayo haikulipwa kwa wakati pamoja na ziada ya asilimia tano. Kwa mujibu wa Sheria ya Mapato, Sura 332, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 na Sheria ya Ushuru wa Stamp, Sura ya 189, Kamishna amepewa mamlaka ya kutoza riba kwenye kodi ambayo imelipwa nje ya muda. Mapendekezo ya kutoa mamlaka kama haya kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 yanaleta uwiano kati ya sheria hii na sheria nyingine za kodi zinazosimamiwa na mamlaka ya mapato. Aidha, ziada ya asilimia tano inayopendekezwa ni kwa ajili ya kodi ambayo haijalipwa na siyo asilimia tano ya kodi yote.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 ya kuongeza Kifungu cha 56A, Kamishna Mkuu wa Mapato kusamehe riba au sehemu ya riba endapo ataridhika. Utaratibu wa kumpunguzia riba mlipaji kodi ni wa kawaida ulimwenguni kote na unatambuliwa na Sheria zote za Kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania isipokuwa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa. Ili kutekeleza utaratibu huu kwa misingi ya haki na usawa, Mamlaka unao Waraka Maalum unabainisha mipaka na masharti ambayo mwombaji anapaswa kuyatimiza. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia Sheria inayosimamia uendeshaji wa masuala ya kodi itaweka bayana masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuongeza nguvu katika eneo la kudhibiti usimamizi wa biashara nzima ya mafuta nchini, tatizo la uchakachujaji wa mafuta na lile la kukwepa kodi kupitia *dumping of transit goods*. Ili kusimamia kikamilifu biashara nzima ya *transit trade*, Serikali inatekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Mali zote zipitazo nchini kwenda nchi jirani uwekewa alama ya forodha na kodi ya mzigo wenyewe, alama hii hurejeshwa pale inapothibitika kuwa mizigo hiyo imevuka mpaka;

(ii) Mamlaka ya Udhibiti wa Mafuta (*EWURA*), itashirikiana na *TRA* kuweka vinasaba, *fuel marking* ili kutofautisha mafuta yanayotumika nchini na yale yanayokwenda nchi jirani;

(iii) Mpango wa ubadilishanaji habari ki-electronic miongoni mwa nchi za ukanda huu. Utaratibu huu utawezesha kujua mizigo ambayo imevuka mpaka na kuingia nchi jirani; na

(iv) Mamlaka ya Mapato iko mbioni pia kuanzisha utaratibu wa kufuatilia ki-electronic mwenendo wa magari yanayobeba mizigo ya *transit* ambao inaitwa *electronic cargo trucking system*.

Mheshimiwa Spika, mikakati hii yote inasaidia kuzuia uvujaji wa mapato kwenye biashara ya *transit* unaofanywa na wafanyabiashara wachache wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya vipuli vya umwagiliaji visitozwe kodi ya *VAT*. Vifaa vya umwagiliaji kama *generator*, mashine za kusukumia maji vilipewa msamaha wa *VAT* vinaponunuliwa na mkulima kupitia Sheria Na.5 ya mwaka 2005 kama ilivyo kwa kilimo ambapo vipuli vya mashine za umwagiliaji pia vinaweza kupewa msamaha wa kodi endapo vitaainishwa na kufahamishwa wazi ili pasiwepo na upotevu wa mapato. Kwa vile havijabainishwa waziwazi, Serikali itawasiliana na wadau wa kilimo cha umwagiliaji maji ili vifaa hivyo viweze kupewa msamaha katika bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya marekebisho ya ushuru wa bidhaa kwenye dieseli na mafuta ya taa na kupunguza viwango vya tozo, bei za mafuta kwenye vituo vya kuuzia mafuta kwa mujibu wa bei elekezi, *indicating pump prices* za tarehe 8 Juni, 2011 itabadilika.

Kwa mantiki hiyo, bei ya dizeli inatarajiwa kupungua kutoka shilingi 2,005.3 kwa lita hadi shilingi 1,681 kwa lita sawa na punguzo la 16.2% ambapo shilingi 99 ni punguzo la ushuru wa bidhaa na shilingi 224.51 ni punguzo la viwango vya tozo. Bei ya mafuta ya taa itaongezeka kidogo kutoka shilingi 1,557.67 hadi shilingi 1,680.97 kwa lita sawa na ongezeko la shilingi 123.3 kwa lita ambayo ni 7.9% ambapo shilingi 348.3 ni ongezeko la ushuru wa bidhaa na shilingi 224.51 ni punguzo la kiwango cha tozo. Aidha, bei ya mafuta ya Petroli inatarajiwa kupungua kutoka shilingi 2,015 hadi shilingi

1,790.49 kwa lita, sawa na punguzo la shilingi 224.5 Ambayo ni 11.2% ambalo linatokana na punguzo la viwango vya tozo.

Ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa, mabadiliko ya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa, hivi sasa ushuru wa bidhaa ni shilingi 52, ushuru unaongezeka hadi shilingi 400.30. Baada ya marekebisho hayo tofauti kati ya ushuru wa awali na sasa ni shilingi 348.3, unaondoa tozo zilizokuwa zinatozwa na mamlaka za udhibiti shilingi 225, ushuru wa bidhaa unaobaki kwenye mafuta ya taa ni shilingi 123.3. Hii ina maana gani? Bei ya sasa ni shilingi 1,557. Bei ya sasa elekezi itakuwa ni shilingi 1,680.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada ya Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011
(The Finance Bill, 2011)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, *schedules of amendment* ya kwanza ni ya Mheshimiwa Eng. Ramo Makala Makani na nyingine ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, nyingine ya Mheshimiwa John J. Mnyika, nyingine ya Mheshimiwa Tundu M. Lissu, nyingine ni ya Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe. Hizo ndiyo tulizozipata na ambazo zimefuata utaratibu unaohusika. Kuna nyingine imeletwa sasa hivi lakini hiyo haitakubalika lakini ile iliiyoletwa mwanzo ilifuata utaratibu.

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

MHE. TUNDU M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mapendekezo yaliyopo na mabadiliko ya Kifungu cha 4 yanasomeka kama ifuatavyo:-

In clause (4) as amended (a) by inserting immediately after the word Act in the proposed section 15(4)(a); and then the following new sentence; Provided that the Village Council may with the approval of the District Council within whose Jurisdiction the Village Council is situate make by-laws for imposition of charges or fees for various types of business licences in respect of businesses operating within the area of the Jurisdiction of the Village Council.

(b) Inserting immediately after the word Jurisdiction in the proposed Section 15(5)(a); and then the following a new sentences; provided that the Village Council shall wherever required furnish the District Council within whose Jurisdiction the Village Council is situate with information relating to licences issued within its area of Jurisdiction.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yana lengo moja lakini kabla sijazungumzia lengo lake naomba niseme kwamba sheria zetu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria ya Halmashauri za Wilaya ya mwaka 1982 vile vile Sheria ya Mamlaka za Wilaya katika Halmashauri za Miji ya mwaka 1982 pamoja na *Local Government Finances Act* yaani Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa zinatambua pamoja na mambo mengine *Local Government Authorities* ni pamoja na Halmashauri za Vijiji na hizi *Local Government Authorities* kama zilivyo Halmashauri za Wilaya au Halmashauri za Miji zimepewa mamlaka ya kutoza kodi katika hizo sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mapendekezo haya ni kutambua hiyo kanuni ya kisheria kwamba mamlaka za vijiji nazo zina uwezo kisheria kwa sheria zilizopo za Tanzania za kutoza kodi na ushuru wa biashara mbalimbali zinazofanyika katika maeneo ya mamlaka ya Halmashauri za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada kama ulivyo na hicho kifungu cha nne kama kilivyo, kimeacha hilo pengo la kutokutambua kwamba mamlaka za Vijiji zina uwezo kisheria wa kutoza kodi na mapendekezo haya yanapendekeza kufuta hilo pengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba, kwa utaratibu wetu wa kutunga Sheria za Halmashauri chini ya hizo Sheria tatu nilizozitaja, Mamlaka ya Halmashauri za Wilaya au za Miji ni kutunga Sheria na hizo Sheria ili ziwe halali na zianze kutumika zinatakiwa ziridhiwe na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa. Kwa upande mwingine, Mamlaka za Vijiji nazo zina mamlaka ya kutunga sheria ndogo ndogo na hizo sheria ili ziwe halali na ziweze kutumika inabidi ziridhiwe na Halmashauri za Wilaya. Sasa kifungu (b) cha mapendekezo yangu ni kuziwezesha, moja, kama nilivyosema kutambua hiyo kanuni ya Mamlaka za Vijiji kutunga sheria

MWENYEKITI: Hii haina kengele ya *warning* ni ile ile moja basi.

MHE. TUNDU M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri au mtoa hoja au AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Waheshimiwa Wabunge watampigia makofi Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu anachofanya ni kwamba anarudisha mamlaka kwenye Halmashauri za Vijiji, kufanya yale ambayo tumesema *Local Government Authority* inaweza kuyafanya isipokuwa wanatakiwa na wenyewe wawape ile *District Council*. Kwa hiyo, marekebisho hayo ni sawasawa. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hicho kwa mujibu wa Sheria za *Local Government* hakuna *by-law* yoyote ...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza Mheshimiwa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo ya hiki kifungu.

MWENYEKITI: Kifungu kipi?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Kifungu hicho hicho kabla hakijapita.

MWENYEKITI: Tumeshaki-*amend*!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Nimesimama kabla hujahoji.

MWENYEKITI: Ngoja kidogo, kiutaratibu tu. Katika kifungu hiki asingeweza kusimama mtu yeyote mwingine zaidi ya aliyetoa hoja ku-*amend* na ndiyo tulimwita Mheshimiwa Tundu M. Lissu.

Sasa hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu imepita kwa hiyo, hatufumui kitu kingine hata kama kimeandikwa na Serikali, *amendment* zilizofanywa na Serikali zimeshapita na hoja aliyoleta Mheshimiwa Tundu Lissu imepita. Sasa wewe unauliza nini?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, sisimami kuleta *amendment* kwa sababu sijaleta *amendment* katika hiki kifungu, lakini nasimama kwa mujibu wa taratibu kwani Mbunge anaweza kusimama kutaka maelezo kwa Waziri Mtoa hoja kuhusiana na hicho kifungu na maelezo ambayo nayaomba ni kwamba, katika mabadiliko haya Mawaziri wanaotajwa kwa ajili ya *consultation* na *approval* ni Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Fedha. Yaani kwa mujibu wa taratibu zetu za Sheria za Serikali za Mitaa, Waziri wa Serikali za Mitaa ndiye anaye-*approve by-laws*. Kwa hiyo, ingepaswa kuwa *in consultation with the Minister responsible for Trade and Minister responsible for Finance and approved by Minister for Local Government*. Kwa sababu *Minister for Local Government* ndiye ambaye ana *approve bylaws* ambazo zinatungwa kule chini. Kwa hiyo, nilikuwa nataka tu nipate hayo maelezo ya upande wa Serikali.

MWENYEKITI: Waziri wa Nchi, TAMISEMI!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo hayo ni sahihi kwamba Serikali za Mitaa kwa maana ya Serikali za Vijiji wakitunga sheria zinakwenda kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ikitunga Sheria zozote zile iwe za makusanyo, usafi wa mazingira na nyingine zozote *by-law* ambayo inatungwa na Halmashauri haiwezi kufanya kazi mpaka imeidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 5

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 6

MHE. TUNDU M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Kifungu cha 6, inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(a) *Deleting the worlds and further 5% per annum appearing after the world year in the proposed section 56A subsection (ii) as amended.*

(b) *Deleting the new section 56A subsection 5 as amended and renumbering sub clause 6 and sub clause 5.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya marekebisho katika Kifungu cha 6 kwa kupendekeza kwamba kifungu cha 56A (2) cha hii Sheria ya Ushuru wa Forodha kisomeke kama ifuatavyo:-

The rate of interest chargeable under sub section (i) shall be the Commercial Bank landing rate of the Bank of Tanzania discount rate at the start of the year and further 5% per annum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba, hayo maneno *and further 5% per annum* yafutwe kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Kifungu kidogo cha (5) inayopendekezwa ambayo inairuhusu Mamlaka ya Kodi kumpa *referral taxable person* kwa *rate* ya kibenki ya Benki ya Tanzania, hakuna fidia ya 5% ambayo TRA kwa mfano inatakiwa kumlipa yule ambaye anatakiwa kuwa *refunded* na hiyo *tax*, wakati akikosea yeye siyo tu analipa riba lakini vile vile anapewa *penalty* ya 5% ya ziada. Sasa lengo la mapendekezo yangu ni kuondoa huo upendeleo. TRA wakikosea walipe *rate* ya riba kama ilivyo kwenye sheria lakini vile vile mlipa kodi akikosea alipe kiasi kile kile cha *interest* ya kibenki asilipe ziada ambayo TRA wakikosea hawatalipishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kifungu kidogo cha (5) inampa Kamishna wa Kodi mamlaka ya kusamehe kodi na napendekeza hiyo mamlaka ifutwe. Kumekuwa na matumizi mabovu sana ya misamaha ya kodi katika Tanzania. Kuna viongozi waliokuwa viongozi wakubwa wa Serikali hii ambao wako Mahakamani leo kwa sababu ya ku-*abuse* utaratibu wa kusamehe kodi. Umefika wakati wa kuwanyang'anya hao watendaji mamlaka ya kusamehe kodi. Sheria iwe wazi kwamba misamaha ya kodi haitatolewa na mtu mmoja. Kwa hiyo, pendekezo langu ni kumnyang'anya Kamishna mamlaka ya kusamehe kodi na sheria iseme ukikosea unaadhibiwa, unalipa kodi na unalipa riba hakuna msamaha wala nini kwa sababu umekosea. Kwa hiyo, lengo langu ni hilo katika hivi vifungu viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kufuta maneno *and further 5% per annum* hayana maelezo ya kutosha na ilivyo sasa lugha iliyotumika hapa ni *term of art* wanasema kwamba ile *Bank of Tanzania Discount Rate at the start of the year and further 5% per annum*. Kwa hiyo, ni maneno ambayo kwa kweli yapo sawasawa na ndivyo ilivyo kwa desturi na hayo ya kifungu kidogo cha (5) nimemsikiliza sana Mheshimiwa Tundu M. Lissu lakini siridhiki kwamba maelezo yake ni sahihi na nashauri kwamba kifungu kidogo cha (5) kibaki kama kilivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa maelezo katika hotuba yake ameeleza sababu ni kwa nini kifungu kile kiwe vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu akikubali kifungu hiki na tuendeleo na hoja nyingine.

MHE. TUNDU M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nashangaa kidogo kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema hakuna maelezo ya kutosha. Kama nilivyosema hii Kifungu cha (6) inapendekeza kwamba anayekosea ambaye hatalipa kodi siyo tu anailipa mamlaka ya mapato kodi *plus* riba vile vile anatakiwa alipe adhabu nyingine ya 5%. Lakini kwa kifungu kidogo cha (5) kilichofanyiwa marekebisho *TRA* wakikosea kweli wanampa *refund*, wanampa riba yake lakini wao hawana adhabu, wamekosea lakini hawaadhibiwi. Pendekezo langu liko wazi kabisa kwamba kama tunakubali *principle* ya kuadhibiwa kwa makosa ya kutolipa kodi kwa kulipishwa ziada ya 5% basi na *TRA* wanapokosea na wao waadhibiwe, kusiwe na upendeleo katika mfumo wetu wa Sheria za Kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kifungu cha pili...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza tufanyie maamuzi hiki cha kwanza halafu tunakwenda hicho cha pili.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, amevijibu vyote kwa pamoja.

MWENYEKITI: Si atajibu tena? Tunataka atueleze zaidi ya hapo hii ya *further five percent per annum*, tunaomba mtupe *clarification* kwa sababu sisi tunasikiliza.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waziri anaweza kuieleza vizuri kwa sababu hii ni *issue* ya biashara. Hii ni adhabu ambayo mtu akichelewa kulipa kodi anachajiwa na ninavyoelewa, kwa ufahamu wangu wa kisheria ni kwamba, adhabu ile na *interest rate* inakuwa ni *commercial bank rendering rate* ya Bank of Tanzania, *discount rate* kwa *base* za *treasury bills*, sasa uki-*discount* unafanya tena *further five percent per annum* kwa mwaka, nafikiri inaeleweka labda nashindwa kuieleza tu kwa sababu nashangaa Mheshimiwa Tundu Lissu ni Mwanasheria, angekuwa mtu mwingine ndiyo ningesema sasa hapa labda nizungumze Kiswahili rahisi zaidi. Lakini, kwenye hili naona hii ndiyo *practice*, ndiyo desturi ambayo inafanyika katika mambo haya.

MWENYEKITI: Haya ahsante, Waziri wa Fedha!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee majibu aliyotoa Mwanasheria Mkuu. Hii ni *practice* katika nchi zote za za *Common Wealth*, ndivyo inavyofanyika kwamba mlipa kodi akikosea anatozwa faini. Si kweli kwamba TRA hawaadhibiwi, tuna *appeal tribunals* na kesi nyingi ambazo zimesomwa *tribunals*, TRA imeshindwa, kwa hiyo tuna *provisions* ambazo ziko kwenye sheria za kuiadhibu TRA. Ningeomba kwa kweli hii tungekwenenda nayo jinsi *practice* ilivyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunakwenda kwenye ile ya pili. Mheshimiwa ile ya pili.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye neno la mwisho ni mimi, ndiye mtoa hoja?

MWENYEKITI: Yaani huwa tunaongea mara mbili, tukiendelea kubishana kweli tutafika mwisho? Sisi hapa baada ya hili tutaanza kupiga kura, ndiyo maana nikasema kwamba ungeeleza hii ya pili kusudi tuendelee na safari.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa vile mimi ndiye mtoa hoja inabidi nijibu hizi hoja, wao hawajatoa, hii hoja ni ya kwangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, ni kweli ni hoja yako ndiyo maana uliposema tukasema na wenyewe waseme, tukifika hapo tunapiga kura ndiyo kanuni inavyosema. Sasa ndiyo maana nikakwambia hebu elezea hii ya pili nayo.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili na yenyewe ni rahisi sana. Kama nilivyosema inapendekezwa kumpa Kamishina wa Kodi mamlaka ya

kusamehe hizi adhabu wanazopewa hawa wanaokwepa kodi na kama nilivyosema hayo mamlaka ya kusamehe kodi, mamlaka ya kufuta adhabu, yametumiwa vibaya na watendaji wa Serikali na pengine nikumbushe tu kwa waliosahau, mwaka 1996 wakati Tume ya Rais ya kuchunguza rushwa, Tume ya Jaji Warioba ilipotoa ripoti, moja ya maeneo iliyoyazungumzia sana ni mamlaka makubwa ya kutoa misamaha ya kodi kwa Maafisa wa Mamlaka kama *TRA* pamoja na Mawaziri. Sasa pendekezo langu ni kuhakikisha kwamba hii mianya ya rushwa, hii mianya ya upendeleo inafutwa kabisa kwa kuwanyang'anya hawa maafisa uwezo wa kusamehe adhabu za wale wanaokosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni *simple* kama una kosa uadhibiwe, hujalipa kodi ya Serikali ulipishwe kodi, upigwe penati, mambo yaishe, hii habari ya kupeana misamaha ya kodi ndiyo inayozaa rushwa na ufisadi katika nchi hii na imefika wakati tuseme katika sheria kwamba hatutaki tena mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hiyo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma taarifa ya Tume ya kero ya rushwa na mimi pia nilikuwa kwenye *secretariat* ya Tume hiyo, hakuna mahali popote ambapo Tume imesema kwamba kuna mamlaka makubwa ya kusamehe kodi. Tume ilichosema ni kwamba kuna utashi '*discretion*' wa mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachosema ni kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu katika hoja yake anasema *delete the new section 56A(5) as amended* basi hakuna mbadala. Sasa haya maelezo anayotoa hayapo, nasikitika kusema maneno haya lakini nitayasema kwa sababu kweli itanifanya niwe huru, nafikiri tuiseme tu kwa sababu tunaonekana kwenye televisheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiseme tu kwa sababu wewe mwenyewe umesema kwamba futa kifungu kipyua na 56A(5) halafu uviandike vingine vile kama 5 na 6. Sasa haya maelezo mengine unayoyotoa hayapo, siyo msingi wa mapendekezo haya. Sisi tunasema hivi Kamishina anaweza ku-*remit* kiasi chote au sehemu ya *interest*, ndicho tunachosema, kama mtu ameshindwa kwa muda unaotakiwa kama ataonesha sababu kwa nini hakufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tusiwe kama watu tusiofikiri sana na nasema hivi situkani mtu, nasema hivyo kwa sababu katika biashara unaweza kuchelewa kulipa kodi na ukawa na sababu. Sasa ukisema kwamba umechelewa, hakuna maelezo, kwa kweli tutakuwa tunafanya sheria ki-Hitler na pengine ni vizuri kwa sababu tunazungumza na Watanzania, maneno haya ya kusema kwamba kodi bila mpango yanavutia sana watu, lakini mpango uliopo ni huu kwamba mtu atasema sababu na Kamishina ni *institution* siyo Kitilya, ile *process* nzima ya kufanya maamuzi iko ndani, *internal mechanism of decision making*, hata ukisikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali anafanya maamuzi, hafanyi peke yake, ni *institution* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba ni vizuri kwanza tufikiri vizuri, tufikiri kwa mapana na tuwe wakweli tu kwamba, yapo mazingira ambayo yanaweza kufanya mtu akachelewa kulipa kodi na akisema kama ana sababu za msingi, sababu hizi zinakubalika kisheria, ndiyo tunavyo–*propose* wewe unasema hayo yafutwe. Nadhani kwamba siyo sahihi na naomba mapendekezo yaliyoletwa na Waziri yabaki kama yalivyo. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Naomba tufanye uamuzi halafu tutakupa nafasi kuhusu utaratibu. Haya baada ya mapendekezo, sasa tunapiga kura ya ndiyo au siyo. Wanaofikiria mapendekezo A na B yaliyoletwa na Mheshimiwa Tundu Lissu yakubaliwe waseme ndiyo,

WABUNGE FULANI: Ndiyoo!

MWENYEKITI: Wanaosema yasikubaliwe waseme siyo.

WABUNGE FULANI: Siyoo!

MWENYEKITI: Nafikiri waliosema siyo wameshinda. Kwa hiyo Kifungu cha (6) pamoja na mabadiliko kinaafikiwa? (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu ilikataliwa na Bunge*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema tuamue ndiyo kisha nije kuzungumza kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Ndiyo tumeamua, sasa nakuita.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sisi tuliomo humu ndani ni viongozi, Kanuni ya 64(1)(g), sisi tuliomo humu ndani ni viongozi, wengi wetu kwa njia moja ama nyingine tumepigiwa kura na hapa tunafanya kazi ya kuandika sheria, hii ni *legislative process*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maneno ambayo Mheshimiwa Mwanasheria ambaye namheshimu sana, ameyatumia ambayo nadhani nina uhakika kabisa kwamba yanakwenda kinyume na kanuni zetu kuhusiana na lugha ya kuudhi. Kusema kwamba Mheshimiwa Mbunge anaposimama kuhoji na kupendekeza ni kutaka kuonekana kwenye

TV, siyo lugha ambayo nilitegemea itatoka kwa Jaji Werema, labda siku tatu zilizopita alikuwa anaumwa, hajawa sawasawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba tufikiri sawasawa, maana yake ni kwamba anasema Wabunge hawafikiri sawasawa. Hii siyo lugha ambayo naitarajia kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kikatiba, aliyesomeshwa kwa fedha za maskini wa Kalinzi, Mwandiga na kwao Musoma, naomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aheshimu Wabunge na afute kauli zake za kuudhi alizotoa mbele ya Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kadri siku zinavyokwenda mnajua kwamba saa nyingine mnatumia lugha zisizokuwa na maana na ni wote wala siyo kusema ni huyu wa sasa hivi, tumekuwa na tabia ya namna hiyo na mbaya zaidi tunatumia hata vyombo vya habari kujaribu kushambulia nafasi za kazi zetu. Sisi tutumie kanuni zetu, lugha ya heshima ni lazima tuifuata na namna ya ku-*argue* hoja yako maana yake huu ugonjwa wa kutumia lugha zisizokuwa na msingi unaendelea humu ndani na naamini kabisa tutaweza kubadilika na tukafuata utaratibu unaofaa. Kwa hiyo nasema kwamba ni kweli maneno ya kusema tunaongea ili tuonekane kwenye TV, ningependa yaondoke. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Afute kauli.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tu kukanusha kwamba mimi sijaumwa, ni mzima kabisa, sijaumwa kiakili wala kimwili. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali hajaumwa na nimefuta ile kauli ya kuumwa. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante na ile ya kusema kuna watu wanataka waonekane katika TV na yenyewe itoke, basi yamekwisha.

MBUNGE FULANI: Afute!

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti,

MWENYEKITI: *Microphone, microphone, microphone* unayotumia husikiki.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli kwamba tunazungumza kwa ajili ya kuonekana kwenye TV, naitoa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Hapo sawa!

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati
ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

MWENYEKITI: Sasa tutaanza na Mheshimiwa Zambi, ndiye aliyeanza, naomba Mheshimiwa John Mnyika uwe mwangalifu kama litafanana vile vile hatutakufikia.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba labda utanisaidia kuniongoza. Lile la kwangu Serikali imekwishalifanyia kazi lakini nilikuwa na hoja nyingine kwenye moja ya hoja za Serikali katika kifungu hicho hicho.

MWENYEKITI: Unataka maelezo au ile *amendment*?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Naam!

MWENYEKITI: Kuna *amendment* au maelezo tu?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maelezo zaidi ya Serikali tu, lile la kwangu nililolipendekeza limefanyiwa kazi.

MWENYEKITI: Basi naomba twende kwa Mheshimiwa John Mnyika kwa utaratibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuwasilisha mabadiliko ambayo yanahusu kifungu cha (8) cha Muswada wa Sheria ya Fedha ukurasa wa 5 na yanahusiana vile vile na ukurasa wa 2 wa *schedule* iliyowasilishwa na Serikali kipengele cha (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yanakusudia na nitasoma: *“In clause eight which relates to the fourth schedule by inserting under heading 27.10 and just before its code 27.10, the following particulars, particulars nyingine ziko kama ambavyo zimeelezwa na Serikali isipokuwa kwenye sehemu ya new excise rate ambapo napendekeza kwamba iwe ni shilingi 300.30 kwa upande wa mafuta ya taa na shilingi 115/= kwa upande wa gas oil.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapendekezo haya, hoja ambayo Serikali imeikubali ambayo ni ya wananchi na imetolewa na Kambi ya Upinzani ni kushusha gharama za maisha. Hoja hii imekuwa na sura mbili kwa upande wa suala hili tunalozungumza la mafuta, kuna suala la tozo za mafuta na kuna suala la kodi za mafuta, lakini ukiyatazama sasa mapendekezo ya Serikali yaliyoko kwenye ukurasa wa pili wa *schedule* ya kupandisha kodi ya mafuta ya taa kutoka shilingi 52/= mpaka shilingi 400.30 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya takriban 600%, wakati huo huo kupunguza kodi ya

mafuta haya mengine ikiwemo dizeli kwa kiwango kidogo sana cha kutoka shilingi 314/= mpaka shilingi 215/= peke yake ambayo ni sawasawa na punguzo la sh 99/=, peke yake kwenye kodi iliyoko kwenye mafuta

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba halikujikita kwenye lile lengo la msingi la kupunguza gharama za maisha, bali imelenga lengo la msingi lingine ambalo na lenyewe naliunga mkono la kupunguza uchakachaji ambao umekuwa ukiligharimu Taifa hasara ya sh. bilioni takriban 50, gharama ya uharibifu wa magari na kuharibu biashara ya usafirishaji wa mafuta. Ni hoja ambayo naiunga mkono lakini namna ambavyo imechukuliwa na Serikali imelenga kuondoa uchakachaji bila kuelekea kwenye suala la kupunguza bei za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naunga mkono kabisa msimamo na maoni ya wote kwamba tusiguse kodi ya ushuru wa magari kwa maana ya *fuel levy* shilingi 200/= kwa sababu inatusaidia kwenye kujenga barabara zetu. Lakini pamoja na kuacha kugusa *fuel levy* Serikali imeshindwa kufanya uamuzi mgumu wa kukubali kugusa kwa kiwango kikubwa zaidi kidogo *excise duty* ili kuweza kwenda kweli kupunguza bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa marekebisho haya ya kuwianisha bei ya mafuta na bei ya petroli yazingatiwe ili usimwongezee mzigo sana mtu anayetumia mafuta ya taa na wakati huo huo usimwongezee mzigo mtumiaji wa daladala, pikipiki na vyombo vingine vya usafiri.

MWENYEKITI: Haya kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa Waziri maelezo sijui kama...

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika maelezo ya Naibu Waziri alisema kwamba ushuru ni sh 400/= ukitoa sh. 52/= unabaki na sh 348.30/= lakini tumekwishatoa tozo la sh. 225/=, ukienda kwenye ile *paper* tumetoa pale, ukishatoa hizo tozo kinachobakia ambacho kitaongezeka kwenye bei ni shilingi 123.30/= ambazo ni sawasawa na 7.9% ya nyongeza. Kwa hiyo, nyongeza itakayoongezwa kwenye mafuta ya taa ni 7.9%.

La pili, *schedule* ambayo Mheshimiwa amependekeza kwamba mafuta ya taa yaongezwe kwa shilingi 300.30 na hizi nyingine, matokeo yake kwa hesabu walizozifanya wataalam wangu za haraka haraka ni kwamba bajeti itakuwa na hasara ya shilingi bilioni 128,436,000,000. Kwa hiyo, pendekezo halihimiliki.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na maelezo yaliyotolewa na Serikali. Kwa sababu kwa mujibu wa kitabu cha mapato ukurasa wa 10, voti namba 21, kuhusiana na mapato ya mafuta inaonyesha kwamba Serikali ilikusudia mwaka huu wa fedha kukusanya kidogo ukilinganisha na mwaka uliopita wa fedha kabla ya marekebisho ya hivi viwango ambavyo vina-*involve* kuongeza tozo ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongeze tu jambo moja la msingi katika maelezo haya kuhusiana na jambo hili ambalo liko mbele yetu. Hapa tunafanya maamuzi

ambayo tunakokotoa mahesabu ya kodi, lakini maelezo ya tozo tunaelezwa kwa mdomo sio sehemu ya marekebisho haya ya sheria. Hofu yangu tukipitisha mapendekezo haya ya Serikali kama yalivyo, Watanzania watajenga imani kwamba bei ya mafuta itashuka kwa kiwango kilichozungumzwa na Serikali wakati ukweli ukiwa ni tofauti. Kwa sababu kwa mujibu wa bei elekezi iliyotolewa na *EWURA* tarehe 8 Juni, 2011, tozo za Serikali za Taasisi zinachukua asilimia 2.23 tu ya bei ya mafuta wakati huo huo kodi ni kati ya asilimia 25 na asilimia 26 ya bei ya mafuta. Tafsiri yake ni nini?

Ukinunua lita moja ya mafuta shilingi 2,000/=, shilingi 600 umelipa kodi. Sasa kama hii kodi haishuki kwa kiwango cha kutosha ukweli ni kwamba tunawapa wananchi matumaini hewa, tutapitisha haya mapendekezo lakini bado bei haitashuka, tutaendelea kulalamikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri maelezo ya mwisho.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni hii karatasi ambayo imekokotolewa na wataalam...

MWENYEKITI: Iko wapi?

WAZIRI WA FEDHA: Wala sikuifanya mimi.

MWENYEKITI: Iko wapi hiyo karatasi?

WAZIRI WA FEDHA: Hii hapa nitakuletea.

Tunasema amependekeza mafuta ya taa yaongezwe kwa shilingi 300/= ile *excise duty*. Sasa ukichukua hiyo maana yake ni kwamba *at the end of the day* tutakuwa na *loss* ya 128 *billions shillings*, kwa hiyo bei anayosema yeye... Hii nitamkabidhi Mheshimiwa Mwenyekiti baadaye.

Lakini tunachosema ni kwamba, kinachoongezeka sasa hivi katika bei ya mafuta ni shilingi 1,557.67 kwa tarehe 16 Juni, 2011. Tukiongeza hizi bei tunafikisha shilingi 1,680/= na kwenye maelezo tumeeleza. Kwa hiyo, hiyo nyongeza kutoka shilingi 1,680/=, kutoka iliyokuwa shilingi 1,557/= nyongeza ya 123 ukifanya hesabu nyongeza yake ni asilimia 7.9. Kwa hiyo, hatujaongopa chochote hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tumeshapita na hii hoja ilikuwa ya mtu mwingine. Nini tena?

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MHE. KABWE Z. ZITTO: No! Ni maelezo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu sio lazima kuwe na *amendment*, kuna maelezo ambayo mtu unaweza ukahoji kupata ufafanuzi wa Serikali, ndio utaratibu ambao unatumika siku zote na miaka yote ambayo nimekuwa Mbunge.

MWENYEKITI: Kabla ya kuhojiwa, *in fact* kama ningetaka kupata maelezo ningepata ya Mheshimiwa Zambi kwa sababu ndiye aliyetangulia wakati ule nikamwambia.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mimi halikuwa suala la *amendment* Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Kuhusu nini Mheshimiwa?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu maelezo ya ziada ya Waziri kabla hatujaamua. Naomba nisikilizwe.

MBUNGE FULANI: Tulishaamua.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegonga meza kabla hatujaamua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, mimi ndiyo nimekaa hapa Mezani, mwenye hoja alijibu tukapiga kura wewe haikuwa hoja yako na usingeweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa ni hivi anapoleta *amendment* Mheshimiwa yeyote mwenye *amendment* yake. Kama mna maneno ya ziada anaungwa mkono. Vile alivyoleta Mheshimiwa Mnyika pale kama mtu alikuwa anataka kuongeza kwa Mheshimiwa Mnyika pale angeongeza kanuni inaruhusu. Lakini ukishafika Mheshimiwa Mnyika anajibu na Waziri anajibu huwezi tena mtu mwingine kuingia. Unaingia tu pale anapokuja na *amendment* yake, ameeleza maelezo yake, anaweza kuungwa mkono. Soma kanuni. Anaungwa mkono na mtu yoyote ama wanaompinga ama wanaomuunga mkono. Ikishaachiwa upande wa pili wamejibu anabaki sasa yule mwenye hoja na wale wanaojibu hoja yake, sio zaidi ya hapo.

Suala ambalo tulikuwa tunasema angetakiwa aeleze ilikuwa Bwana Zambi, lakini bahati mbaya nikapita, kwa hiyo, tunaendelea na uamuzi tumefanya. Naomba msome vizuri kanuni hiyo ya kufanya *amendment* katika kipindi hiki na tulitoa ile semina kwa maelezo hayo hayo. Kwa hiyo, anapotoa mtu maelezo au *amendment* zake kama mtu anataka kumuunga mkono asimame na tutampa nafasi. Dakika zake tatu, mwenye hoja ni dakika tano, mwingine anayemuunga mkono au anapinga ni dakika tatu, huo ndio utaratibu. Kwa hiyo, tunaendelea kitu kinachofuata.

Kifungu cha 9

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati
ya Bunge pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11

10. **MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kifungu ya

MWENYEKITI: Ya 10 tumeshapita.

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Uliwahi ku....

MWENYEKITI: Tumehoji tayari, hatuwezi kuwa tunarudi nyuma na mbele.

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo ya Serikali kwenye Kifungu hicho. Kwa hiyo, naiondoa.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Meshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14, napendekeza marekebisho yafuatayo. Marekebisho ninayopendekeza ni kufuta kabisa aya ya (k) kutoka *paragraph* (c) ya hiyo Kifungu cha 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba iwapo mapendekezo yangu yatakubalika labda niseme hiyo (k) ambayo napendekeza ifutwe inataka nini. Inapendekezwa katika hiyo aya ya (k) kwamba kuwe na misamaha ya posho zinazolipwa watumishi wa Serikali kwenye nyumba, usafiri, posho ya majukumu, posho ya muda wa kazi za ziada, *overtime*, *honoraria*, sijui inaitwaje wanayolipwa watumishi wa Serikali au Taasisi ambazo bajeti yake yote au kwa kiasi kikubwa inalipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba watumishi wa Serikali wanalipwa mishahara midogo sana na kwamba kuna haja ya kuongeza mapato yao, lakini dawa ya kuongezea mapato watumishi wa Serikali sio kuwapa posho ambazo hazitahesabiwa kwenye mishahara yao siku wanapostaafu badala yake zinawekwa kwenye posho, dawa ya kuongeza vipato vya wafanyakazi ni kuhakikisha kwamba mishahara yao inapandishwa ili kuondokana na huu utaratibu wa posho ambao Mpango wa Taifa wa

Maendeleo wa Miaka Mitano umeeleza wazi kwamba posho zimesababisha *paving incentives structure* katika utumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hii misamaha ya kodi ikiondolewa kama ninavyopendekeza mapato ya Serikali yataongezeka. Kama lengo ni kuongezea mapato watumishi basi badala ya kuwalipa hizi posho ambazo hazitahesabika kwenye mishahara yao basi ziwekwe katika mishahara ile *at the end of day* wanapomaliza kazi wawe wana mishahara mikubwa ambayo itahesabika katika *gratuity* zao, itahesabika katika viinua mgongo vyao. Hii kuwapa posho ambazo hata kama hazilipiwi kodi zinaonekana nzuri sasa hivi, lakini wanapomaliza ajira zao pensheni ni ndogo, kiinua mgongo kidogo, haitawasaidia wafanyakazi wetu na vile vile inaipunguzia Serikali yetu mapato.

MWENYEKITI: Nawasubiri wanaotaka kuunga mkono, sijawaona. Mheshimiwa Manyanya, kuunga au kutokubaliana vyovyote sawa.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kufuatia maelezo ya mtoa hoja nami kwa upande mmoja naunga, lakini upande mwingine nakataa. Ninachozungumzia ni kwamba ni ukweli kama ambavyo Serikali imezungumzia kwenye mpango wake iko haja ya kuangalia vizuri namna nzuri ya kuwezesha hizi posho na mishahara ya wafanyakazi kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu posho hizi pia zinalipwa kwa shughuli maalum na wakati mwingine kwa wafanyakazi wanaofanya kazi maalum na sio wote. Posho hizi pia ukifuatilia upande mwingine zimekuwa zikitumika kuepusha matumizi ambayo yalikuwa katika Serikali au Mashirika ya Umma kwa kulipia gharama ambazo zilikuwa hazipati uhakiki unaowezekana kwa mfano, hospitali, kwa hiyo ikafikia bora kutoa posho kama hizi. Kwa hiyo, nashauri kwamba kinachotakiwa kwa sasa kabla Serikali haijapata utaratibu huo mzuri hali ya posho hizi ibaki kama ilivyo na kama ilivyopendekezwa na Serikali.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu ni kuondoa kodi kwenye posho. Hoja iliyopo mbele yetu sio kuwepo au kutokuwepo kwa posho. Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu ni kwamba, wakati ambapo tunazungumzia misamaha ya kodi inazidi kuongezeka na wakati ambapo kuna malalamiko makubwa ya wananchi kuhusiana na posho mbalimbali ambazo watumishi wa Serikali na viongozi wanalipwa haileti picha nzuri kwa umma kuja na hoja ya kuweka misamaha ya kodi kwenye posho hizo zinazolalamikiwa.

Kwa hiyo Mheshimiwa Tundu Lissu anapendekeza kwamba badala ya kuweka sheria hii ya kuweka misamaha kwenye posho hizi zinazolipwa kifungu hicho kiondoke kabisa, kabisa kisiwepo ili tubakie tuna mjadala mmoja tu wa suala la posho zinazolipwa na sio suala la misamaha ya kodi kwenye posho. Kwa hiyo, naomba hili liwe *clear* ili Waheshimiwa Wabunge wanapofanya maamuzi waweze kuelewa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu kusiwepo na msamaha kwenye kodi ya mapato ambayo maana yake mapato hayo ni ya posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko dhana hapa inataka kujengwa kwamba kuna watu wanalalamika kuhusu mambo haya. Mimi huwa najiuliza sana, Mwalimu aliyeko kule Ilagala, Mwanajeshi ambaye analala analinda kwenye lango pale Benki, wale Mapolisi wetu ambao wako kule mbali vijijini, Madiwani wetu wa kule vijijini, tunakaa Bunge hili tunasema zile posho wanazopewa ni tatizo, nadhani hapa liko tatizo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, tatizo hili la nchi tuliangalie kwa upana wake, tusiliangalie kwa kuangalia jambo moja moja. Naunga mkono Serikali kwamba hizo posho wanazopewa hao wafanyakazi wadogo, Walimu, Wanajeshi sijui watu gani bado Manesi, Waganga wetu wanaoookoa maisha yetu bado waendeleo kulipwa lakini tuendeleo sasa kuangalia kama walivyosema kwenye Mpango wetu wa Miaka Mitano kwamba, umefika wakati kama nchi wakae waliangalie jambo la posho kwa mapana yake ili baadaye tuje na mkakati bora ambao wananchi na Watanzania watauelewa na watafaidi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nitoe taarifa?

MWENYEKITI: Unamtaarifu nani?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Namtaarifu Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuzungumza hivi sasa. Kwamba kwa mujibu wa sheria zetu posho zinazozidi shilingi laki moja ndizo zinazotowza kodi, sheria ya sasa. Walimu wa Ilagala, Kalinzi na kwingine kokote, Polisi wanaolinda hawalipwi posho inayozidi shilingi laki moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunatoa msamaha wa kodi, tunatoa *tax exemption* kwa watu wenye pesa tayari. Tunatoa *tax exemption* kwa watu ambao wanapata posho zaidi ya shilingi laki moja, Wakurugenzi, Makamishna, Wabunge, Mawaziri na kadhalika. Kwa hiyo, naomba tusiwapotoshe wananchi kwamba tunatetea watu maskini, watu maskini hawalipwi posho hizo, Polisi wanalipwa shilingi 1,000/= mpaka shilingi 3,000/= haitozwi kodi tayari. Tunakataa pendekezo hili la kuondoa msamaha wa kodi kwenye posho.

MWENYEKITI: Taarifa hiyo tunaipokea.

Naendelea, nilikuona umesimama Mheshimiwa nani? Mheshimiwa Mkono sijakuita nilikutaja kwa kukuona mkono, basi simama, nimechanganya mkono na Mkono mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Haya Mheshimiwa Mkono simama.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Hili suala la posho nadhani halieleweki vizuri. Posho kubwa inayotolewa nchini ni Madiwani, maana Madiwani wote hawalipwi mshahara, wanalipwa posho. Ukisema hiyo posho pia itozwe kodi siamini kama tutakuwa tunawatendea haki hawa Madiwani. Sisi Wabunge tunapata sh. 70,000/=. Sasa nadhani ndugu zangu Wapinzani tunajaribu kuona hivi tunakotoka kwenye Wilaya huko na wenzetu pia ni Waheshimiwa Madiwani leo hapa mnawakandamiza hata kidogo wanachopata, unasema toa. Sisi ni Madiwani ama ni Wabunge tu. (*Makofi*)

Nadhani kwa hili tukubaliane na hoja ya Serikali.

MWENYEKITI: Bado hii hoja tunaendelea nayo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Bunge letu ili wakati mwingine tufikie mahali tukubaliane mambo kimsingi. Nataka kuzungumza kwamba, nadhani ingekuwa ni busara kwetu kulitazama suala hili la posho na kuangalia umuhimu wa kuondoa kodi kwa kuzingatia kuwaombea wale wanaopata posho kidogo, posho ile iongezeke na kodi iweze kuwa *reflected* kwenye sheria ili wasiweze kuja kuumia katika kipindi hicho ambacho posho zao zitakuwa zimeongezeka. Nasema hivi kwa nini?

Serikali imeshatangaza itapandisha mishahara ya watumishi, hoja hiyo ni ya msingi sana. Nadhani kazi yetu kubwa sasa ni kuishauri Serikali, wale watumishi ambao posho zao bado ni ndogo ziweze kupanda, lakini wakati huo huo tayari tumeshapitisha sheria, hata posho zile zikishapandishwa wataumizwa kwa maana ya kwamba posho hizo zitakatwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu niendeleo kusema tukubaliane vitu vya kimsingi kwa wakati ambao ni wa kimsingi. Tayari wako Madiwani ambao ni wahudumu wa Taifa hili, wana posho hizo kisheria za kukatwa mapato na wengine waweze kuingia kwenye kundi hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Simbachawene, halafu nitatoa fursa kwa Serikali halafu mtoa hoja ataendelea.

MHE. SELEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kimsingi kama walivyochangia wenzangu ifike mahali wewe mwenyewe ulisema Bunge hili ni moja lenye uwakilishi wa kweli. Lakini uwakilishi wa kweli pia uzingatie na ujikite sana katika maslahi mbalimbali, kwa mfano, tunapowaondolea posho wenzetu au wanapokatwa kodi inawaondolea morali wenzetu ambao tumewakabidhi kijiti cha utekelezaji wa shughuli za jamii na si kwamba wanapata zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale kuwaondolea kodi ni kuwapa unafuu lakini pia tunawatia moyo Waheshimiwa Madiwani, watumishi wetu wanahitaji kwa kweli kuona ama sisi kufahamu na kutambua kile ambacho wanakifanya ni sahihi na tuliwaona na si kunyang'anya sehemu ya ile morali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali tu kwamba wenzetu wa CHADEMA wameteleza kidogo na naomba tuwaunge mkono wafanyakazi hawa kwa hoja iliyo mbele yetu na naunga mkono pendekezo la Serikali ili kuweza kuona kwamba kazi hii isonge mbele vizuri. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hoja yetu hapa ambayo imeletwa na Mtoa Hoja Mheshimiwa Tundu Lissu kwa nia njema kabisa ni kwamba anataka posho hizi zisipewe msamaha. Sasa pamoja na wachangiaji wote waliozungumza na namheshimu sana Mtoa Hoja nia yake ni njema na wazungumzaji wote nia zao ni njema. Ila kila mmoja anajaribu ku-*reflect* kwa mazingira anayoyajua kama hilo litafanyika. Jambo hili kwa kuwa lilikuwepo katika Mpango wa Serikali kwa miaka mitano juu ya kuangalia mfumo mzima wa namna ya posho zilivyo na mambo mengine yanayohusiana na posho.

Nadhani mtoa hoja akubaliane tu na wazungumzaji wengi waliosema lakini hasa upande wa Serikali kwamba tusikurupuke na jambo hili tunahitaji kufanya utafiti wa kutosha nani na nani, watu gani, makundi gani? Tukishaweka hiyo *classification*, ndiyo tunaweza tuka-*set* Sheria vizuri inayosamehe au kutokusamehe. Kwa sasa tukikurupuka, tukaweka hiyo Sheria sasa hivi kwa kadri Mtoa Hoja anavyotaka, hakika kesho tukitoka nje ni vilio kwa makundi mengine. Nadhani tukubaliane na naamini mtoa hoja atakubaliana na michango yetu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nadhani waliozungumza kwa kweli wamesaidia sana. Katika mambo haya nadhani tuwe tunaongea na viwango kwa sababu nikiangalia muda ambao tumeuchukua kuzungumzia suala hili kiasi chenye ukiambiwa ni kidogo mno, hicho ambacho tunakizungumzia, ambacho kitafutwa kama kodi. Nafikiri kama tuna hoja nyingine mahali pengine tuzizungumze lakini kama tunarudisha tu hoja ya posho na kodi naomba kwa kweli tukubali hoja ya Serikali, iwe kama ilivyo na kwa sababu kwenye Mpango wa Miaka Mitano tumesema tunaangalia posho, tunaangalia misamaha ya kodi ili tujue chochote ambacho sio cha lazima ama kifutwe au kirekebishwe. Sasa kwa hiki kidogo, nafikiri kwa kweli tungenema tu tukubali.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja za wachangiaji na naomba niseme tu kwa kifupi sana kwamba, hoja kwamba msamaha wa kodi ya posho inawahusu Madiwani iliyoanzishwa na Mheshimiwa Mkono na Mheshimiwa Mkono namheshimu sana lakini sijui ameyatoa wapi hayo maneno? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Diwani nchi hii anayelipwa *housing allowance*, hakuna Diwani nchi hii anayelipwa *responsibility allowance*, hakuna Diwani anayelipwa

extra duty allowance, anayelipwa *overtime*, anayelipwa *hardship*, anayelipwa *honorarium*, hakuna. Haya maneno kwamba tunataka kuwanyang'anya pesa Madiwani ni maneno ya kuokoteza tu na ya watu ambao hawana hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa maneno yale yale ya kuokoteza ndiyo tunayapigia kelele. Endelea Mheshimiwa Tundu Lissu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ambazo hazitozwi kodi, ambazo zinaombewa msamaha hapa ni posho za wakubwa. Ni posho, za hawa waliokaa humu, Wabunge, Mawaziri, Watendaji Wakuu wa Serikali wanalipwa mamilioni ya fedha, posho kila mwezi. Hizi zinatakiwa zikatwe kodi. (*Makofi*)

Mshahara wa Mheshimiwa Mbunge, milioni tatu na laki mbili.

WABUNGE: Aaaaah!

Ni kweli, aaaaaah nini? Lakini shilingi milioni tano ni posho, zitozwe kodi.

MWENYEKITI: Kwanza taarifa ya kwanza ni ya Mheshimiwa Mkono halafu Mheshimiwa Waziri.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Natoa taarifa Madiwani wanalipwa *sitting allowances* kama sisi Wabunge tunavyolipwa *sitting allowances*.

WABUNGE FULANI: *Responsibility!*

MWENYEKITI: Jamani mnaongea na kiti mbona mnajirusharusha huko kitu gani? Msikilize kila mtu atapata nafasi yake. Mheshimiwa Mkono malizia.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wanalipwa *responsibility allowance* wanapokwenda huko.

WABUNGE FULANI: Wapi?

MHE. NIMROD E. MKONO: Wanapokwenda kwenye vikao vya *LAAT* wanapewa posho, sawasawa kama Wabunge. Sasa kama sikueleweka vizuri ni kwamba *definition* ya posho haijaeleweka vizuri kwa hoja ya mtoa hoja. Kwa hiyo, nasema Madiwani wanapata posho sawasawa na Wabunge na hiyo pia imeorodheshwa kwamba hiyo kodi isamehewe.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 64(a) cha Kanuni yetu inasema: “*Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 10 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.*” Naomba nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba Wenyeviti wa Halmashauri wanalipwa *responsibility allowance* na hizi *responsibility allowance* *Mayors* wote wanalipwa. Wenyeviti wote wa Kamati ndogondogo za Halmashauri wanalipwa *responsibility allowance*.

WABUNGE FULANI: Madiwani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niendeleze kidogo kwamba, hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kuwa ana nia njema ya kuunga mkono Mpango wa Miaka Mitano ya Serikali, naichukua kama hoja *positive* kwa sababu lengo lake ni kuunga mkono kwa kazi ambayo mwisho wake itakuja tutaiona hapa Bungeni. Serikali imekwenda kwa mtazamo mpana, sio mtazamo finyu, tunataka kuangalia namna tutakavyoweza kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Alichosema Mheshimiwa Tundu Lissu ni kweli, Wabunge wanapata mshahara mkubwa wote tunajua ukilinganisha na mishahara ya watu wengine. Tunapata posho alizosema Jimbo *allowance*, baadhi yetu tunapata na *responsibility allowance*, mimi napata shilingi laki mbili na Wenyeviti wote wanapata. Kiongozi wa Upinzani ndiyo peke yake amependelewa katika Bunge zima anapewa na pesa ya kukirimu wageni, mwezi huu tumempa milioni mbili.

WABUNGE FULANI: Waziri Mkuu pia mtaje.

MWENYEKITI: Naomba tuongee kwa utaratibu. Waziri Mkuu anahusika vipi tena?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Nakubaliana na posho zote hizi zilizotolewa, mbona sisi tunawasikiliza sana.

MWENYEKITI: Muanze kusikilizana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Posho zote hizi ambazo amezisema Mheshimiwa Zitto hata sisi kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kabla hatujaandika tulijua zinatolewa na ndiyo maana tukakiri kwamba lazima tuangalie utaratibu mpya wa kupunguza gharama za Serikali za uendeshaji lakini pia kuongeza kipato kwa wafanyakazi. Lakini hatuwezi leo hii posho ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Ndugu Mbowe *Entertainment allowance* tukaitoza kodi kwa sababu imetungwa kwa kanuni nyingine. Tume ya Bunge ndiyo imehalalisha na posho hizi zote tunapata kihalali. Ninachopendekeza ni kwamba, jambo hili lirudi kwenye utaratibu, sisi Wabunge kama

tunataka kuonyesha mfano na ningefurahi kama Wabunge ndiyo tungeanza kwa mfano, tulirudishe hili jambo kwenye Tume yetu ambayo ilimpangia huyu na tulifanye hilo kama mfano, halafu ndiyo tuendeleo kwa watu wengine. Lakini hatuwezi kuliamulia hapa kwa wote.

Kwa hiyo pendekezo langu nasema, Mheshimiwa Tundu Lissu yuko sawa, lakini twende sasa kwa zile Kanuni zilizokokotoa kuwapa haki mmoja baada ya mwingine. Halafu tukubaliane na ningefurahi kabisa kama tungeanza sisi wenyewe Wabunge hapa ndani, lakini twende kwa utaratibu. Hatuwezi kukaa hapa Bunge tukawaondolea haki zote, watumishi wote. Hapa ndani ya Kanuni yako ingawa si kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu, Kanuni ya 95 kinasema: “Bunge halitashughulikia Muswada, hoja au ombi lolote endapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atathibitisha kwamba matokeo ya Muswada, hoja au ombi hilo yatakuwa ni:-

(a)...

(b) Kubadilisha mishahara, marupurupu, au masharti ya utumishi, ikiwa ni pamoja na likizo, usafiri, marupurupu...” Hayo ni mambo ambayo kanuni hii inatukataza Bunge hili kushughulikia. (*Makofi*)

Kwa sababu kwa kweli tutakuwa hatutendi haki kwa sababu baadhi ya marupurupu mengine ambayo yanatolewa yana Sheria ambazo tumezitunga hapa. Kwa hiyo, napendekeza Waheshimiwa Wabunge wakubali hoja hii kama ilivyoletwa kwenye Mpango na imeungwa mkono na Mheshimiwa Tundu Lissu kuwa ni sahihi, lakini twende kwa utaratibu. Kwa hiyo, yale ya Wabunge tuyalete kwenye Tume, mimi ni Mjumbe na baadhi ya Wabunge wenzangu ni Wajumbe tuyaamulie halafu tuangalie na Kanuni nyingine, tupendekeze kama sehemu ya kutekeleza Mpango wetu.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Hakuna taarifa nyingine, Mheshimiwa Tundu Lissu endelea.

MBUNGE FULANI: Tunadhulumiwa mishahara, kumbe ni milioni tatu. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Naomba Mheshimiwa Tundu Lissu ajibu na nyie wote mkae chini.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa haya maneno yanayozungumzwa hapa, hoja yangu sio kufuta posho, hoja yangu ni kuomba Bunge hili likatae pendekezo la kufuta kodi ya posho. (*Makofi*)

Sheria ya sasa hivi kwa wasiofahamu Sheria ya Kodi ya sasa hivi inasema posho yoyote inayozidi shilingi laki moja lazima itozwe kodi ya mapato. Muswada huu unapendekeza kuondoa hiyo kodi, sijaomba kuondoa posho. Nasema hivi, hawa wanaopata posho ya zaidi ya shilingi laki moja ambayo kwa Sheria ya sasa hivi

wanapaswa kutozwa kodi waendeleo kutozwa kodi. Hii kodi itatozwa kwa wenye vipato vikubwa kama nilivyosema Wabunge, Mawaziri, Watendaji Wakuu wa Serikali, Mameneja na watu wa aina hii. Si kufuta posho, ni kuondoa hili pendekezo la kuwafutia kodi hawa wanaopata vipato vikubwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima pamoja na kwamba maneno ambayo yamezungumzwa kwa kweli hayahitaji kujibiwa jinsi ambavyo yalivyo na upofu wa Sheria za sasa hivi. Ni kweli mtu anayesema tunafuta posho za Madiwani wakati posho zinazofutiwa kodi hapa hazitaji Diwani, hazitaji *sitting*, hazitaji nini ni kukosa kuelewa Sheria tu. Sasa hoja yangu ndiyo hiyo, nashukuru sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Nafanya uamuzi hakuna ruhusa ya Mwongozo wa Spika.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DR. HAMIS A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a), ambapo inasomeka kama ifuatavyo kwamba:

“Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:

(a) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli’.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Tundu Lissu akitoa hoja yake alisema mshahara wa Mbunge ni milioni tatu na laki nne. Lakini kwa mujibu wa *salary slip* yangu, mshahara wangu ni milioni mbili na laki tatu. Naomba mwongozo wako endapo Mheshimiwa Mbunge ametoa taarifa zisizo na ukweli katika Bunge lako.

MWENYEKITI: Mwongozo gani? Wabunge wanalipwa mshahara shilingi milioni mbili na laki tatu kabla ya kodi. Tunaendelea, hoja hapa si mshahara wa Wabunge. Tunaendelea na kazi, Katibu.

Kifungu cha 15

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 16

Kina Marekebisho ya Mheshimiwa Tundu Lissu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 16 kinapendekeza misamaha ya kodi *on flight charges* za ndege kubeba samaki Tanzania na kuzipeleka nje. Inazungumzia kwamba hizo “*exemptions shall not apply to payment received in respect of carriage of fish by a foreign aircraft*” na kama yanavyosema madhumuni na sababu za Muswada hii *exemption* itaruhusu vyombo zaidi vya usafirishaji mizigo kutoka nje ya nchi kutua Tanzania na kuendeleza uwekezaji katika maeneo hayo *and so on and so forth*. Hoja yangu hapa ni rahisi sana, nchi hii tumetoa misamaha ya kodi mingi sana. Umefika wakati kwa Serikali yetu kwa kupitia Bunge hili kutunga Sheria zitakazoiwezesha Serikali kupata mapato kutokana na kodi. Kwa hiyo, hili pendekezo la kutoa misamaha mingine tena ya kodi kwa hawa wanaokuja kubeba au kuchukua samaki wetu si vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti pendekezo langu ni kwamba hili pendekezo la Kifungu cha 16 likataliwe ili hayo malipo yanayopaswa kufanywa kwa sheria ya sasa hivi, kwa ndege zinazobeba minofu ya samaki kutoka Mwanza, kutoka Dar es Salaam au kutoka mahali popote kwenye viwanja vyetu vya ndege, zitozwe kodi kama ilivyo sasa hivi. Tumesema katika Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwamba misamaha ya kodi ni mikubwa mno tuanze kuipunguza, tuanze kwa kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukazungumza ulimi mmoja unasema tutapunguza misamaha ya kodi, ulimi mwingine unasema tutaongeza misamaha ya kodi. *We can not speak with the forked tongue, the only animal with forked tongue is a snake.* Hatuwezi tukazungumza na ndimi mbili kama za nyoka, ni lazima kama tunasema tunafuta misamaha ya kodi, tufute misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni hilo la kwenda sambamba na mpango wa maendeleo ya miaka mitano, unaosema misamaha ya kodi ni mikubwa tuanze kupunguza na tuanze kwa kukataa pendekezo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha wa minofu ya samaki, Ziwa Victoria limezungukwa na nchi tano, zote zile zinatoa misamaha. Kwa miaka kadhaa ndege zimeacha kwenda Mwanza kubeba samaki kwa sababu ya kodi ndogo ambayo tunatoza. Samaki wanajulikana kwamba wapo Kenya wakati robo tatu ya Ziwa Victoria lipo Tanzania. samaki wote wa Mwanza pale wanakwenda kwa magari mpaka Kisumu au Nairobi na wanasafirishwa kwenda Ulaya kwa kupitia Kenya na kwa maana hiyo wanajulikana kwamba wanatoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya sasa ni kufanya kama wenzetu walivyofanya, kwamba samaki wote wanaotoka kwenye viwanja vyao vya ndege

hawatozwi kodi. Sasa tukiendelea kufanya hivyo ndege hazitakuja, Wasukuma wale hawatapata chochote, sasa sijui hata tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali halisi ilivyo, hili lina faida kwa nchi, napendekeza kwamba tulikubali. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri wa Fedha na hoja yake, lakini naomba niijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kweli anachosema Waziri kwamba ndege zimeacha kutua kwa sababu ya kutokuwepo msamaha huu unaopendekezwa sasa hivi, tujiulize zamani wakati zilikuwa zinatua na hapakuwa na msamaha zilikuwa zinatua kwa nini? Kwa sababu zimekuwa zinatua miaka mingi nimekuwa nikienda Mwanza. Zimeacha kwa sababu ya kutokuwepo msamaha wakati zamani zilikuwa zinatua, wakati vile vile hakukuwa na msamaha, hii hoja ya aina gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hoja kwamba Kenya wana msamaha ni hoja sawa na kusema hivi, kwa sababu kwa jirani nyumba inawaka moto, basi na sisi tuwashe moto nyumba yetu, ni hoja ya aina gani hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inatoa misamaha ya kodi kwa asilimia 2.5 ya pato ya Taifa, Kenya wanatoa asilimia moja tu. Kwa nini kama tunataka kuwaiga Kenya tusipunguze misamaha yetu ya kodi ifikie kiwango cha Kenya cha asilimia moja ya pato la Taifa. Misamaha ya kodi ya aina hii lengo lake ni lile lile la siku zote la kuwatajirisha walio matajiri, kuwawezesha walio nacho kuwa nacho zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuanze mwaka huu *either we are serious or not*, kama tupo *serious* juu ya kupunguza misamaha ya kodi tuanze na hili. Kama hatupo tuendelee kuzungumza na hizo ndimi mbili kama nyoka.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi samaki wanavuliwa Ziwa Victoria na wanapelekwa kwa malori mpaka Kenya kwa ajili ya kusafirisha, kwa hiyo tukiondoa hii kodi, itawezesha ndege kutua Mwanza na kuchukua samaki na kupeleka moja kwa moja Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaunga mkono mapendekezo ya Serikali. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana tukaongeze na tukasisitiza, ili nchi yetu ifanikiwe katika kuongeza viwanda vinavyohusika na minofu ya samaki, ni lazima wale samaki wawe *processed* hapa Tanzania. Wakati tunaendelea kujibizana juu ya kuondoa huu msamaha wa kodi, ndege ambazo zinaingia Kenya kwa siku kuchukua samaki na wale samaki wote wakitoka katika Ziwa Victoria upande wa Tanzania kama alivyosema Waziri. Ndege zinazoondoka Jomo Kenyatta kwa siku zikichukua maua ambayo yamelimwa eneo la Kilimanjaro ni nyingi sana. Ni wajibu wa Serikali hii kuhakikisha kwamba tumeweka

mazingira ambayo tunaweza tuka-attract hizi ndege zikaweza kutua hapa na zikachukua mizigo hapa Tanzania. (Makofi)

MWENYEKITI: Wanaosema pendekezo lililoletwa na Mheshimiwa Tundu Lissu likubaliwe waseme ndiyo.

WABUNGE FULANI: Ndiyooo.

MWENYEKITI: Wanaofikiria pendekezo hili lisikubaliwe waseme siyo.

WABUNGE FULANI: Siyooo.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 17

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na maelezo ya Serikali.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, mapendekezo yangu yapo mahsusi kwenye ukurasa wa 14 wa Muswada huu wa Sheria, hiki ni Kifungu cha sheria namba 17(w), napendekeza kibandilike *in the clause 17 by deleting and substituting for it following new clause; “the principle acting amended in the paragraph one of the second schedule by deleting item (w) and substitute for it with following:*

(w) Payment of withholding tax on dividend arising from investment in the export processing zone and special economic zone during economic zone during initial period of five years.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijaeleza sababu ya jambo hili, niseme tu kwamba, mimi ni mdau katika hoja hii, kwa sababu Jimbo walilonituma kuwawakilisha kuna maeneo matatu ya kibiashara ya namna hii. Kuna eneo kubwa sana la ekari sitini na tano la Benjamin Mkapa *Special Economic Zone* na kuna *Millennium Business Park*, lakini vile vile kuna *EPZ ya NSSF*, kwa hiyo, ni jambo ambalo tunaishi nalo kila siku kule Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu linakusudia kupendekeza kwamba kuna kitu kinachoitwa *withholding tax on dividend*. Kwa lugha ya Kiswahili ningeweza kusema kodi ya zuiyo kwenye gawio. Kwa lugha rahisi ni kwamba wale wafanyabiashara wakishapata mapato, wakigawana mapato yale, wale wenye hisa ya ile kampuni, faida waliyoipata au gawio lao litozwe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Serikali ni kwamba hawa jamaa wapewe msamaha wa miaka kumi, *regardless* wanapata faida, wanazalisha au wanafanyaje waendeleo kupewa msamaha kwa miaka kumi mfululizo. Sasa pamoja na hoja ambazo amezitoa Naibu Waziri wakati anaelezea, niseme tu kwanza Naibu Waziri alitumia mifano mingi sana ya Uwekezaji mwingine ambao hauhusiani kabisa na hoja iliyopo mbele yetu kuonesha kwamba Taifa linapata tija sana na uwekezaji wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nijikite kwenye hoja hii iliyopo hapa sasa hivi ya *withholding tax*. Mifano iliyotumiwa ya nchi nyingine nashukuru Naibu Waziri amekiri kwamba nchi kama Malyasia inatoa msamaha kwa miaka mitano peke yake. Nchi kama Philippines ni miaka nane peke yake, Tanzania tumeamua kumi. Sababu ya kuamua miaka kumi inaelezwa kwamba ni kwa sababu Kenya wameamua kutoa misamaha kwa miaka kumi. Lakini ukiingia kwenye sheria ya Kenya, kuna misamaha unampa mtu ili aweze kuingiza mtaji wakati anapowekeza miundombinu na kadhalika. Kuna misamaha ya faida ya kampuni kama anakusudia kuwekeza mtaji tena kwenye kampuni kwa maana ya *cooperate tax*, huu ni msamaha mahsusni ambao hata wenzetu wa Kenya wameweka *limitation ya exemption* kwenye *withholding tax on dividend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna vivutio vingi sana ambavyo tumekwishavikubali, sioni sababu kwa nini tuwape faida hii ya msamaha huu wa miaka kumi, badala yake tupunguze ili tuweze kupata faida mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokieleza sisi, kwa maana ya misamaha ya kodi ambayo Serikali inatoa kwa miaka kumi na tulizungumzia *specific* kwamba katika viwanda vinavyowekeza katika *EPZ*. Jambo linalofanyika ni kwamba, kwanza, wawekezaji hawa wanaleta mtaji na mtaji huu kama usingekuwepo kusingekuwa na ajira, kusingekuwa na hicho ambacho kinafanyika, tunachotegemea baadaye kitozwe kodi. Tulisema vile vile kwamba katika utaratibu wa kawaida wa kuwekeza katika uwekezaji mkubwa, kwa mfano, Viwanda vya Chuma, tangu mchakato unapoanza wa kuwa na hiyo *feasibility study*, kuwa na mtaji, kuwa na ujengaji wa hiyo miundombinu, kutengeneza kile kiwanda, kukamilisha ujenzi na kuanza uzalishaji, kawaida unachukua miaka nane. Mtu aliyepewa fursa hiyo inakuwa ni miaka miwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba azma ya Serikali tunaposema tunaondoa au tunatoa nafuu ya kodi kwa wawekezaji wakubwa walete tija, walete mitaji, walete wawekezaji, ni kwa sababu ya kuhuisha uchumi wa nchi, ni kwa sababu ya kuongeza ajira kwa vijana waliopo Vyuho Vikuu ambayo wanategemea Serikali hii itengeneze ajira kwa wingi, na ni kwa sababu kwa kufanya hivyo, ongezeko la kodi linaendelea kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hawa watu wote ambao wataajiriwa katika viwanda hivi, wanaendelea kulipa *pay as you earn*, kodi zingine zote zinaendelea

kulipwa wakati kodi ya *cooperate tax* ndiyo ambayo peke yake inakuwa imesamehewa kwa kile kipindi na baada ya hapo inaendelea kulipwa kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyeiti, ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingekuwa na tatizo kama hapa tungekuwa tunazungumza kodi ambazo ni kwa ajili ya kumvutia mtu kuweka mtaji ama ni katika hatua za mwanzoni za uendelezaji. Hapa tunazungumzia mtu ambaye tayari amekwishaanza kutengeneza faida na siyo tu *exemption* kwenye faida ya kampuni *cooperate tax*, tunam-*exempt* kodi hata akigawia *dividends* wale wafanyabiashara wenzake ambao wako huko lakini wanapewa misamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, tuzungumze kwa *logic* moja kwa moja, Dar es Salaam kuna uhaba mkubwa sana wa ardhi. Makuburi pale limechukuliwa eneo la ekari 65, ni eneo kubwa kweli. Mmachinga akipewa eneo hata dogo tu, mfanyabiashara wa kawaida, kesho yake anatozwa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ekari 65 kwenye *prime land, ten years* mtu asilipe kodi, *it doesn't make sense* na ameshapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa, Naibu Waziri amesema kwamba mpaka sasa uwekezaji umegharimu trilioni moja, lakini umezalisha ajira elfu kumi na tatu. Mahesabu ya haraka haraka tu *per unit cost* ya kuzalisha ajira moja ni zaidi ya milioni mia moja kwa ajira moja. Ningemwelewa Naibu Waziri na hoja ya Serikali kama tungesema maana hapa tunazungumzia kuhusu *FDI (Foreign Direct Investment)*. Kuna vitu viwili hapa kuna *SEZ* na *EPZ*, *SEZ* ni mitaji mikubwa, dola milioni tano ambayo ni bilioni saba, *EPZ* ni mtaji mdogo sana dola mia tano ama dola laki moja na hamsini. Hii ni mitaji ambayo hata *domestic investors* wangeweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kubwa zaidi nimalizie kidogo, *EPZ* asilimia 80 ya bidhaa zinaruhusiwa kuuzwa soko la ndani, kama hawa wanakuwa *tax exempted* kwa muda mrefu hivyo wataathiri soko la ndani na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tufuate muda. Waziri kwa kifupi tumalize.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji amekubaliana na hoja ya Serikali kwamba, ni lazima uwekezaji wenye tija uweze kupewa msamaha wa kodi. Ninachotaka kusema hapa, Serikali itaendelea na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba tunawavutia wawekezaji wenye mitaji mikubwa mikubwa na tunahakikisha kwamba katika kufanya hivyo hizi *FDI's* anazosisema ni lazima ziende sambamba na ushindani wa Mataifa mbalimbali. (*Makofi*)

Kila nchi, mitaji duniani ni michache na nchi zote zilizopo unazoweza kuzifikiria zote zinafuata mitaji hiyo hiyo. Kama kuna uwekezaji wa dola za Kimarekani milioni,

nchi ya Rwanda inazitafuta, wameweka vivutio vingi. Kuna nchi nyingine duniani ambako wanasema mwekezaji ukifika siku hiyo hiyo una kampuni, siku hiyo hiyo una ofisi, siku hiyo hiyo umeanza kufanya kazi na hulipi kodi milele.

Sisi katika Tanzania tumesema kila biashara, kila kampuni ni sharti mwisho wa siku walipe kodi zote za Serikali na katika utaratibu wa kufanya hivyo tumesisitiza kwamba katika kuwekeza, uwekezaji mkubwa mkubwa na uwekezaji mdogo mdogo na nasisitiza utaratibu wa sisi kutoa nafasi ya *EPZA*, wawekezaji wenye mitaji midogo wawekeze ni kwa sababu Serikali iliona ni lazima wananchi wapewe fursa ya kuweza kushiriki katika uwekezaji katika *EPZA* na tunafanya hivyo kwa kuhakikisha kwamba tunapoendelea kukuza maeneo ya uwekezaji katika Miji mikubwa na Miji midogo na katika Halmashauri za Wilaya tunahakikisha kwamba, wawekezaji wetu wa ndani wanapata fursa ya kuendelea kukua ili baadaye na wao wawe wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kusema kwamba, Serikali kama tulivyorudia kusema itaendelea kuhimiza, itaendelea kusisitiza uwekezaji mkubwa na kama nilivyosema nchi yetu inahitaji *Marshal plan*, sisi wote tunahitaji kutengeneza ajira, tunahitaji kutengeneza miundombinu ambayo tunaitegemea, tunahitaji kutengeneza reli, bandari, tunahitaji kutengeneza haya mambo yote ili wakulima wetu huko waliko waweze kupitisha mazao yao yaweze kufika kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa wanaofikiria hoja ya Mheshimiwa John Mnyika ikubaliwe waseme ndiyo

WABUNGE FULANI: Ndiyoo!

MWENYEKITI: Wale wanaofikiri kwamba hoja ya Mheshimiwa John Mnyika isikubaliwe, waseme siyoo.

WABUNGE FULANI: Siyoo!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Mheshimiwa John Mnyika ilikataliwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Sasa tunakwenda kwenye hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kufuta misamaha yote ya kodi inayopendekezwa katika Kifungu cha 17 cha Muswada huu. *Paragraph* (a) inapendekeza msamaha wa kodi ya mapato inayotokana na uwekezaji au biashara inayofanyika katika *EPZ*, *paragraph* (b) inazungumzia misamaha ya kodi kwenye kozi ya zuio, *paragraph* (c) inahusu misamaha ya kodi kwenye kodi ya zuio kwa

gawio na vile vile inahusu misamaha ya kodi ya zuio kwa kodi inayolipwa kwa mwekezaji kutokana na leseni na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna swali la kujibu hapa, kama nchi hii lengo la Serikali ni kufanya mazingira mazuri kwa wawekezaji ili kuwafanya waendeleo kutajirika na rasilimali zetu, waendeleo kutumia nchi yetu na ardhi yake na mali zake bila kulipa kodi basi *paragraph* hii ipite. Lakini kama lengo la Serikali ni kuongeza mapato ili Serikali ipate uwezo wa kuwatumikia wananchi basi kifungu hiki cha 17 kikataliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia hoja juu ya ajira katika maeneo maalum ya kiuchumi. Nina ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ya mwaka 2007, *ILO Database on Export Processing Zones* na *ILO* katika ripoti yao ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri aliitaja bila kusema walisema nini, walisema *ILO* imesema *EPZ* - maeneo maalum ya kiuchumi katika nchi za Afrika hayajatengeneza ajira zozote za maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi tatu (3) tu maeneo haya yametengeneza zaidi ya kazi 35,000, nchi nyingine zote zaidi ya 18 ni kazi elfu kumi (10,000) au kwenda chini.

Kwa hiyo, hii hoja kwamba walete mtaji, watengeneze ajira, kodi ya mishahara ni hoja tulizosikia mwaka 1997/1998 wakati tunapitisha misamaha ya kodi ya madini. Leo hii waliopigia debe misamaha hiyo hawathubutu kusema sekta ya madini inatusaidia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kama tuko *serious* lazima tujifunze kutokana na makosa yetu. Tulikosea kwenye misamaha ya kodi ya madini, tumekosea katika maeneo mengi ya uwekezaji, tusikosee kwenye maeneo maalum ya kiuchumi.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Labda mimi naomba ni-*share* uzoefu wangu na Mheshimiwa Tundu Lissu, kuhusiana na uwekezaji na misamaha ambayo inatolewa wakati tunakwenda kutengeneza hiki kipengele cha kusamehe kodi kwenye maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Mheshimiwa Mbunge analiangalia hili suala kwa upande mmoja tu kwamba tu-*charge* kodi na mwisho wa siku tuongeze mapato kwenye Serikali yetu. Lakini kazi ya Serikali siyo kuongeza tu mapato kila siku kwenye shughuli zake.

Pia ni lazima tuangalie fursa ambazo zitajitokeza kwa sisi kupata uwekezaji wa kutosha kutoka kwa *foreign direct investors* ambao wanaleta *capital* ndani ya nchi yetu, wanaleta *transfer of knowledge* ambapo watalaam wa ndani ya nchi yetu, wafanyakazi watapata *knowledge* kutoka kwa wawekezaji na mwisho wa siku bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo haya zitapelekwa kuuzwa nje ya nchi na zitatingizia fedha za kigeni. Hii

pengine ingeweza kuwa ni faida kubwa zaidi kuliko hata ile faida moja ambayo tunaianalia kwa kodi ambayo tungeipata kwenye *withholding tax on dividend*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza sana muda wako, naomba niunge mkono hoja ya Serikali kwamba tuna kila sababu ya kupunguza kodi ili kuweza kuwavutia wawekezaji kwa kila jinsi ambayo tunaweza katika nchi yetu ili kuweza kukuza uzalishaji ndani ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu. Sasa nitatumia mtu mmoja kwa sababu muda hauruhusu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena katika ripoti ya Benki ya Dunia nchi ya China imefikia kuwa na uchumi wa pili duniani kwa sababu ya wawekezaji wa *EPZ* na *SEZ*. Katika ripoti hii ya Benki ya Dunia nchi ya China hadi kufikia sasa hivi watu walioajiriwa katika haya maeneo maalum ya wawekezaji wamefika milioni 30. Katika Tanzania *EPZ* na *SEZ* zina miaka minne ya kufanya kazi. Uwekezaji ambao niliuzungumzia kama sehemu moja tu. Uwekezaji mkubwa katika nchi hii umefikia zaidi ya trilioni moja. Narudia tena kusema hiyo haija-include uwekezaji wote unaopitia *Tanzania Investment Centre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu utakuwa mpana zaidi, wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Taifa kwa maana ya kodi utakuwa mpana zaidi kama tukiweza na tukiunga mkono uwekezaji wa ndani na uwekezaji wa nje kama nchi hii itakuwa tayari kuhakikisha kwamba watu wanaokuja kuwekeza, wawekezaji ambao siyo wababaishaji, wawekezaji ambao Serikali hii inawa-*vet* na kuhakikisha kwamba mitaji wanayoleta inakwenda sambamba na azma ya Taifa ya kukuza uchumi na dira yetu ya miaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu watatusaidia, naomba niseme pia kwamba hili siyo suala la kujipatia umaarufu wa kisiasa kwa kusema kwamba kodi hazilipwi. Sera ya Chama cha Mapinduzi kwanza ni kuhakikisha kwamba kila mtu kuanzia sisi tuliokaa hapa wote tunalipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na sera ya pili ni kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa kodi, utapanua wigo wa kodi kwa kuhakikisha kwamba unahuisha na unaboresha njia zote za uwekezaji, mitaji katika dunia hii inatafutwa, sisi tunatafuta wawekezaji tuweze kuboresha reli yetu kutoka Dar es Salaam ifike Kigoma kwa Mheshimiwa Kabwe Zitto. Reli hii ifike Rwanda na Burundi, reli hii itumiwe na nchi ya Congo na nchi zingine zote zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Uganda imesema iko tayari kutumia bandari ya Mwambani pale Tanga kama tukiweza kujenga reli. Uchumi wa Tanzania kama nilivyosema sasa hivi sisi tuna makontena 400,000 yanayotoka Dar es Salaam kwa uwekezaji zaidi ya milioni 500 ambazo tunahitaji kuvutia wawekezaji, tutasogeza na kuongeza idadi ya makontena 1,400,000 yanaweza yakatoka pale Bandari ya Dar es Salaam yaka-*flow*, yakaenda nchi zingine zote wanatutegemea. Bandari ya Mombasa

inatoa makontena 600,000 kwa mwaka, tuna uwezo wa kufanya mara mbili yao. Ninachotaka kusema na naomba mtu yeyote asibeze nia ya dhati ya Serikali ya kuvutia uwekezaji ya kuhakikisha kwamba uwekezaji huu unakuwa na tija, ya kuhakikisha kwamba uwekezaji huu hata baada ya wao kukamilisha kitu kinachoitwa *return on investors* wanaweza sasa wakaendelea kuchangia katika uchumi wa Taifa kwa kodi watakazozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Mauritius ambayo nilikuwepo wiki iliyopita wamefanikiwa katika miaka 10 kujenga kijiji cha teknolojia na teknolojia ile ya Mauritius imeweza kuwa ni *centre* kubwa ya uwekezaji wa dunia watu wote wanaokuja kuwekeza Afrika kuanzia akina *microsoft* na wengine wanaanzia Mauritius. Tunaweza tukafanya haya mambo hapa Tanzania. Nilichokisema ni kwamba tusijenge ukuta. Tukubaliane yale mambo ya msingi na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kodi ambazo ni lazima zihuishwe, zitahuishwa maeneo ambayo Serikali itabidi kuangalia misamaha ambayo haina sababu, tutaendelea kuiangalia na hatusemi kwamba kila msamaha upo sawa. Ndio maana Serikali hii ipo kuipitia misamaha yote ya kodi ikiwa ni pamoja na hii ya uwekezaji kuhakikisha kwamba inakwenda sambamba na ushindani, sambamba na uwekezaji, sambamba na kuhakikisha nchi hii inasogea mbele. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu hitimisha.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nijibu hoja mbili zilizotolewa na Mheshimiwa Kigwangalla na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Kigwangalla miezi michache iliyopita aliongoza maandamano ya wananchi wake dhidi ya Mgodhi wa Dhahabu wa Lusu, Nzega kwa madai kwamba huo mradi umeangamiza uchumi wa wananchi wake. Anataka kutuambia nini? Anataka kutuambia nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijibu hoja za Mheshimiwa Waziri, wala sitakwenda kwenye Benki ya Dunia. Niende kwenye maneno ya Serikali ya Tanzania kuhusiana na misamaha ya kodi. Kamati ya Dkt. Kipokola, Kamati ya Masha, Kamati ya Jaji Bomani, Kamati ya Bunge hili ya Fedha za Mashirika ya Umma (*POAC*) mwaka 2007 juu ya misamaha ya kodi. Serikali kwa kupitia Kamati zote hizi imesema kwamba *there is no win - win situation* kwa sababu misamaha ya kodi inatajirisha wageni, haiipatii Serikali mapato yake. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia habari za Kenya, za wapi, za China. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Malizia Waziri tupige kura.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Hakuna Taarifa, tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee tena kusema hili suala lisiingiziwe siasa kabisa. Tunachokuwa tunakizungumzia hapa ni rahisi, mtu kusema kwamba Serikali hii inasamehe kodi zote. Mtu anapoiingiza gari lake la kifahari halipi kodi, mtu anapofanya mambo ya nyumbani kwake halipi kodi. Tunachokizungumzia hapa ni suala la kusamehe kodi mahususi kabisa kwa wawekezaji ambao uwekezaji wao utaikomboa nchi hii. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo imepiga hatua bila kuwa na vivutio kwa wawekezaji. Katika nchi ya Amerika na naomba nimpe mifano, kwa mifano wanadamu tunaelewa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Amerika zile *states 50*, majimbo yote yale yanapambana kwa kupunguza kodi. Katika majimbo mengine yameondoa *income tax* ili wananchi na wawekezaji wa ndani wakawekeze kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Afrika zaidi ya 50 tunashindana kuvutia wawekezaji. Tunavutia wawekezaji wa ndani kwa sababu katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kama kodi za Tanzania zitakuwa juu kuliko za Uganda wawekezaji wenyewe wa Tanzania hapa wataondoka watakwenda kuwekeza Uganda na huna namna yoyote ya kuweza kumzuia. Tunapomzuia, idadi ya wanafunzi walioko pale *UDOM* wanaomaliza Chuo Kikuu mwaka huu na mwaka ujao hawa watu wote wanategemea wakute ajira ziko tayari. Viwanda hivi ambavyo tunawavutia watu wawekeze ni kwa sababu ya kuhakikisha kwamba tunajenga mazingira yaliyotayari ya kuhakikisha kwamba nchi yetu siyo tu kwamba inakuwa kwa uchumi, lakini tunaongeza uwezo wa Taifa kuweza kuajiri watu.

Mwaka huu tunao watu siyo zaidi ya 500,000 ambao wanalipa *pay as you earn*, nchi hii mwaka jana kwa takwimu zilizopo zaidi ya wananchi wa Tanzania milioni 20 walikuwa na simu za mkononi. Ni nafasi kubwa sana na ni fursa kubwa ya kuwapa hawa watu ajira mbalimbali za kilimo, za viwanda mbalimbali vya kuboresha, kuongeza thamani ili tuweze kuipeleka nchi yetu mbele.

Tuna uwezo wa kuifanya Tanzania iwe nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki kwa kuongeza ajira, iwe nchi ya kwanza kwa uchumi, iwe nchi ya kwanza kwa *GDP*, iwe nchi ya kwanza kwa *per capital income*, kipato cha mtu mmoja mmoja ndio azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaanza kufanya uamuzi.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyonayo natumia kifungu cha 28(5) kuongeza muda usiozidi nusu saa. Tukimaliza hizo dakika kama shughuli zitakuwa bado kutakuwa hakuna cha mapendekezo ya mtu yeyote tutapitisha vifungu kama vilivyo.

Kifungu cha 18

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 21

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu asubuhi nilisema kwamba tunajitahidi kugatua madaraka kupeleka kwenye Serikali za Halmashauri zetu za Wilaya. Lakini hapa tumesema katika maeneo yote ya uwekezaji ambayo yatakuwa yako kwenye mamlaka ya Halmashauri hizo na kwa maana ya mazao yote yatakayozalishwa katika maeneo hayo maana yake Halmashauri hizo zisitoze kodi kabisa.

Sasa tukasema tuna dhana ya *Devolution by Decentralization (D by D)*. Sasa tunachofanya ni kama tena tunazinyang'anya Halmashauri za Wilaya madaraka. Lakini wakati huo huo kumekuwa pia na tatizo la Serikali Kuu wakati mwingine kushindwa kupeleka fedha kwenye Halmashauri za Wilaya ili zifanye kazi sawa sawa. Sasa hapa tunataka, tena tunaondoa kodi za aina zote kwa mazao yanayozalishwa katika maeneo hayo. Sasa ndio sababu nikapendekeza kwamba kifungu hiki kiondoke ili sasa Serikali Kuu isionekane kama inaziingilia mno kiutendaji Halmashauri hizi za Wilaya. Naomba maelezo ya Serikali. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kweli kwa heshima yote niungane mkono na Mheshimiwa Zambi na niombe sana Serikali yetu, historia katika nchi yetu inaonyesha kwamba katika kipindi cha nyuma Halmashauri zetu za Wilaya zimekuwa zikikidhi haja ya kujitegemea kwa kuruhusiwa Halmashauri hizo kutengeneza vyanzo vyake vya mapato kupitia kodi mbalimbali. Lakini baada ya muda vile vyanzo vyote ambavyo ni laini ambavyo vilikuwa vikitumiwa na Halmashauri zetu vilichukuliwa na Serikali Kuu kwa nia njema kabisa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Nilikuwa naomba sana katika utaratibu huu wa kukusanya kodi za mazao Halmashauri ziachiwe mamlaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano halisi katika Jimbo letu la Peramiho na Halmashauri ya Wilaya ya Songea hatuna zao la biashara. Zao kubwa tunalolilima kwenye Halmashauri ile ni mahindi kwa ajili ya chakula. Mahindi hayo ushuru unaopatikana kwenye yale mahindi umesaidia sana kutoa mchango wa Halmashauri katika miradi ya maendeleo kwa mujibu wa taratibu za kifedha za Serikali yetu. Kwa

hiyo, naomba sana niombe Serikali yetu katika kukusanya mapato kwenye vyanzo vya mazao mamlaka hizo tuziachie Serikali zetu za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hiyo ya Mheshimiwa Zamboni.
(*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni huruma imetoshwa. Lengo la msingi la Serikali yetu ni kuhakikisha ustawi wa Watanzania unapatikana. Tumetoa misamaha mingi kwa wawekezaji kwa kiwango ambacho sasa kinatisha. Tumefanya hivyo kwenye sekta ya madini na uchumi wa nchi tunadanganywa kwamba unakua lakini kumbe kinachokua ni mitaji ya wageni iliyowekezwa nchini. Rai yangu ni kwamba lazima sasa tufike mahali, hakuna maana mimi kuwa na *EPZ* Mererani, hakuna maana mimi kuwa na *SES* mahali popote katika nchi hii kama Serikali Kuu haikusanyi chochote na wenyeji nao Serikali za Mitaa hazikusanyi chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Zamboni na hili lingefaa hata katika sekta ya madini, huko tunakwenda tuhakikishe kwamba sasa migodi mikubwa inafutiwa kodi ili tuhakikishe kwamba Serikali inakusanya kodi na kuleta ustawi kwa watu maskini na kuepusha sasa utajiri wote kuhamishwa kupelekwa nje. Hiyo ndio rai yangu. (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili ni sawa sawa na pendekezo ambalo limetolewa kwenye kifungu cha 17 cha Muswada. Kinachozungumzwa hapa ni zile kodi kwenye *EPZ* na *SEZ for initial period of ten years*. Nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, alitoa maelezo mazuri. Jambo hili ni jambo la *project* na *project* ina *project cycle*.

Sasa katika *initial* ya *ten years* tunasema kwamba kwenye *local government* wasikusanye hizo kodi kwa msingi kwamba kama utachora mstari utakapoanzisha hicho kiwanda ili uje upate faida baada ya kuwa umeanza *production* ni muda mrefu. Tumepewa *data* ya *eight years*. Wale ambao wamesoma uchumi juu ya *project circle particularly* kwenye *project* za *World Bank* utafahamu kwamba una kipindi cha kupumua kabla hujaanza kupata faida utozwe kodi na utoe gawio.

Sasa hapa pia ndio mapendekezo hayo, naomba Mheshimiwa Wabunge pamoja na hisia kali tuelewe tunachopendekeza. Serikali inapendekeza kwamba *there shall be exempted all taxes and levies imposed by local government authorities for products produced in the Export Processing Zones and Special Economic Zones during initial period of ten years*. Kwa hiyo, siyo kwamba kuna msamaha *completely* ni *initial period of ten years*. Baada ya miaka kumi zile kodi za Halmashauri zitatozwa kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri nitoe maelezo hayo kusudi twende kwa pamoja kwa sababu nimeona kwamba labda kuna mchanganyiko kidogo.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Tukishafika hapo tunafuata utaratibu, sana sana ataruhusiwa Mheshimiwa Zambi tu. Halafu mkumbuke pia kwamba kifungu cha 17 mmeamua vinginevyo kinalingana karibu na hicho hicho. Mheshimiwa Zambi endelea.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani tatizo la msingi la mahusiano kati ya Serikali Kuu na *local governments*. Uhusiano uliopo ni kwamba Serikali Kuu inajiona kama baba na *local government* kama mtoto, ndiyo tatizo lililopo hapa maana vyanzo vingi kama nilivyosema mwanzoni ambavyo ni vizuri zaidi vinayang'anywa au vinabaki Serikali Kuu na vyanzo vyote ambavyo ni hafifu ndivyo vinavyobaki kwenye *local government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *local government* ndiyo inayofanya kazi zote katika nchi hii pamoja na ustawi wa wananchi wetu, sasa kila tunapokwenda maana yake tunyanganywe vyanzo vyote vya mapato hata kama ni kwa mwanzo kama alivyosema AG miaka kumi sio muda mdogo kama mtoto anazaliwa yuko darasa la tatu, la nne huyu. (*Makofi*)

Mimi nadhani tumezidi kuwa wapole mno, kwa hiyo, Serikali wakati mwingine itusikilize na mimi naomba niseme na Serikali itusikilize Wabunge wa CCM pia tunaposema sio kila jambo linalozungumzwa na Wabunge wa CCM likaonekana halipewi maanani. Mimi naomba Serikali katika hili nalo kama linafanana na kifungu cha nyuma, lakini hapa Serikali itusikilize. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Bwana Zitto mbona unasimama kabla hujaitwa? Sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, *finalise* tukafanye maamuzi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezaliwa kwenye Halmashauri hizo hizo na kinachosemekana hapa jamani ni sawasawa na maamuzi tuliofanya kwenye kifungu cha 17 na kama tumefanya vile, hapa pia tunasema kwa njia yaku-*attract*, kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji kwenye Halmashauri zetu hizo ni kwamba...

TAARIFA

MHE. TINDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Ngoja amalize kusema Taarifa tutawapeni, kama nyie mnaelewa sisi inabidi tusikilize kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kwanza nafikiri umjulishe huyo kwamba mimi pia ni Mkuu wa *bar*. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Hayo ya kwenu huko huko, lakini tuendele. (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, ilikuwa ni kwamba sababu ni ile ile kwamba hatuzuii Halmashauri kutoza kodi baada ya kile kipindi cha miaka kumi, huo ndiyo msimamo tu wa pendekezo hili. Naomba pendekezo la Serikali likubaliwe.

TAARIFA

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa kabla hujafanya maamuzi.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupe Taarifa kwamba kifungu cha 17 hakifanani na kifungu hiki. Kifungu hiki kinahusu kodi za *local government*, kifungu cha 17 kinahusu mitaji yaani kinahusu kodi ambazo zinakusanywa na TRA. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili liweze kuwa *clear* kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu amejichanganya, nilikuwa naomba hoja ambayo Mheshimiwa Zambi ameitoa ijadiliwe kwa lengo hilo kwamba haya ni mambo mawili tofauti. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kifungu kikubaliwe kwa sababu moja kuu, Serikali Kuu inatoa karibu asilimia 95 ya matumizi yote ya *local government*, kwa hiyo, hakuna *local government* yoyote ambayo itakuwa haina mapato kwa sababu pesa zinatoka Serikali Kuu. Lakini la pili hawa tunaowasema, watakuja kwenye Wilaya yako kama kuna *incentive*, kama hakuna *incentive* hawatakuja na kwa hivyo hakutakuwa na ajira wala hakutakuwa na chochote. Kwa hiyo, hakuna sababu ya gombania kitu ambacho hakipo, kwa hiyo, hakuna kitakachokosekana, Serikali Kuu mpaka sasa hivi inazipa Halmashauri kati ya asilimia 90 mpaka asilimia 95. Naomba kifungu hiki kikubaliwe.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kura zihesabiwe.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika na rekebisho lake.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kilikuwa na marekebisho ya Mheshimiwa Zambi na kilikuwa na marekebisho yangu.

MWENYEKITI: *Actually* ngoja nieleze kwamba marekebisho yako yanakubalika ya Mheshimiwa Tundu Lissu hayakubaliki kwa sababu naye pia alitaka kifutike. Kwa hiyo, ya kwako yanakubalika. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mapendekezo ninayowasilisha yanahusu kifungu cha 21 kinaanzia ukurasa wa 14 mpaka ukurasa wa 15.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Hakuna utaratibu tuendele tumsikilize kwanza.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakijapitishwa, kuna *amendment*.

MWENYEKITI: Yeye huyu ana *amendment* yake ndiyo maana nimemruhusu aseme.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hiyo, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kifungu gani cha utaratibu?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuhusu utaratibu kwa sababu Mheshimiwa Zitto aliposimama hapo, Kanuni ya 68...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Sendeka naomba ukae chini tafadhali, tukishapita hatua fulani, haturudi nyuma, sasa hivi huyu Mheshimiwa Mnyika ndiyo nimempa nafasi. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naamini maamuzi yalifanyika yalihusu *wording* ya Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Lissu ambayo ilikuwa inahusu kuondoa kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni tofauti na ninaiwasilisha hoja hii kwa sababu nilipata hisia pamoja na kuwa nilikuwa naungana na Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Lissu kwamba Serikali ingekataa katakata kukibadili hiki kifungu kama ambavyo wenzangu walikipendekeza.

Sasa mimi naomba nipendekeze *a win-win situation*, hoja ya Serikali ni kwamba huu msamaha utolewe kwa miaka kumi, mabadiliko ninayoyapendekeza mimi ni *“the last sentence is amended by deleting the word ten before years and substituting it with the word five to read during initial period of five years.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya mabadiliko haya ninayoyapendekeza ni kwamba dhamira ya Serikali ni kwamba kifungu kiendele kubaki, kifungu kibaki, lakini

kipunguzwe idadi ya muda badala ya msamaha wa miaka kumi, uwe msamaha wa miaka mitano pekee yake kwa maana ya *initial stages*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme tu pamoja na yote hayo yaliyoelezwa na Serikali kuhusu *exemptions* na kadhalika na visingizio vyote vilivyotolewa vya Serikali, tutofautishe mambo mawili, kuna kitu kitu kinachoitwa, *Special Economic Zones*, hizi zinahusisha mitaji mikubwa dola milioni tano ambayo ni kama bilioni sana na kuendelea. *EPZ category* yake ni mitaji midogo, dola laki tano, wazawa dola laki moja na hamisi, dola laki moja.

Hoja inayotolewa na Serikali ya *incubation period* kwamba ili uwekezaji ukue mpaka upate faida unahitaji miaka kumi, unahusu uwekezaji mkubwa sana. Huwezi kuniambia mtu anayewekeza dola laki moja ambayo ni kama milioni mia moja na hamisi sawasawa na wafanyabiashara wengi sana wazawa ambao wakiwekeza tu wanalipishwa kodi papo papo, mfanyabiashara naamini unasema unampa *exemption* ya miaka kumi, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ina *public interest*. Sisi kule Ubungo, mimi natoka Manispaa ya Kinondoni tunalalamikiwa kwamba barabara kipande kidogo tu kutoka Ubungo Maziwa mpaka *External* kilomita mia kibovu kweli kweli, Halmashauri inalalamikiwa kwamba inashindwa kukisawazisha, matokeo yake kuna foleni, Halmashauri hii sehemu ambayo ingepatia mapato inaambiwa *stop* kwa sababu ya sheria iliyotungwa na Bunge sio Halmashauri, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii haihusu Bunge pekee yake, inawezakana Wabunge wengine humu naomba mfuatilie kwenye maeneo yenu. Mpango huu wa *EPZ* ama *SEZ* unakwenda sambamba na mimi nitumie neno la moja kwa moja tu, uporaji mkubwa wa haja, kuna Mikoa ambayo maeneo yatachukuliwa ndani ya kijiji ekari elfu moja ni zaidi ya kijiji ni eneo kubwa kweli kweli, watu wachukue ekari elfu moja, wakae miaka kumi wafanye kazi, uzalishaji bila kulipa kodi, haiwezekani. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi muhimu sana kwa niaba ya Watanzania, *win-win situation* anayosema Mheshimiwa Mnyika, ukiziangalia Halmashauri zetu na huu uwekezaji kwa wengine, Halmashauri zingine ndiyo utakuwa unaanza, hakika miaka kumi ni mingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ataanza biashara, atawekeza, atapata faida mpaka atafilisika Halmashauri haijapata kitu. Mimi naunga mkono hoja ya Mnyika ya miaka mitano, *win-win situation*. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Hakuna cha Mwongozo, Waziri wa Viwanda.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni suala la ufafanuzi tu. Katika Afrika Mashariki, tumeingia katika Itifaki ya Soko la Pamoja. Kuna mambo ambayo tunakubaliana kama nchi zote tano tuyafanye, tumeweka mpango wa *common external tariff* na hadi sasa hivi *VAT structure* katika Afrika Mashariki imefanana nchi zote, kasoro Kenya wakaenda wakarudisha chini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji ambao Serikali inajaribu kuuvutia, jambo la kwanza naomba ieleweke kwamba wale wawekezaji mpaka tunavyozungumza sasa hivi hawapo, hizo kodi ambazo tunazungumza mpaka sasa hivi si sifuri, mwekezaji atakapokuja katika Halmashauri husika chini ya mpango huu wa miaka kumi ambao unawavutia wawekezaji ambao unawapa fursa sawasawa na Wilaya zingine zote za nchi zote tano za Afrika Mashariki, mwekezaji huyu jambo la kwanza anaanza kulipa mishahara na kodi zinazotokana na ajira kuanzia siku ya kwanza. Kwa hiyo, sio kweli kwamba kodi hazilipwi zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mwekezaji huyu analeta teknolojia, sio tu kwamba watu wanapata ajira, wanapata na teknolojia ambayo inaendelea kurithishwa miongoni mwa watu wetu wanaoajiriwa.

Kwa hali halisi, kama Bunge hili halitaridhia kuhakikisha kwamba upunguzaji wa kodi hii na kuruhusu wawekezaji ambao tunawaomba, tunawasihi, tunawabembeleza waje katika Halmashauri zetu na tumesema sio tu waje katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Mbeya, tunataka waje Singida waende Tandahimba, waende katika Mikoa mbalimbali ambayo hawaendi, hali hii mpaka kule Karagwe, hali hii itawezekana kama sisi wote hapa tukikubaliana kwamba tunawapa wawekezaji hawa miaka kumi, wawekeze na katika kuwekeza wafanikiwe na katika kufanikiwa ajira tunazotaka kuzitengeneza kwa mamilioni ziweze kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutahadharisha katika hali tulionayo sasa hivi ya ushindani ya nchi tano, ambazo zinapambana kama ambavyo Wilaya zetu nchi hii na zenyewe zinapambana kuvutia wawekezaji waanze kuchajiwa kodi kinyume na mapendekezo ya Serikali yatahatarisha kabisa wawekezaji ambao tungetegemea waje katika Halmashauri zetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri analipotosha Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri anazungumzia *East African Common External Tariff*. Hii ni *internal tariff*, hii ni kodi ya ndani tena ya *level* ya Halmashauri, kazi ya Serikali za Mitaa. Mimi niseme tu kwamba jambo hili lina maslahi sana kwa Taifa na ninaamini kabisa na hii ni imani yangu kwamba Bunge lako Tukufu litachukua mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 64(2) na (3), kazi ya Bunge ni kutunga sheria, sio kazi ya Serikali. Serikali inaleta mapendekezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hizi za Wabunge wote wa pande zote mbili, tukikubali pendekezo la Serikali kama lilivyo, tutakuwa tumekuwa kama *rubber stamp*. Huo ndiyo ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwenye sheria kuna kitu kinachoitwa *consequential amendments*, unabadili sheria moja mabadiliko yake yanasababisha kubadilika kwa sheria nyingine, naamini tukipitisha hii itafanya *consequential amendments* ya sheria zingine zozote ambazo Naibu Waziri anazizungumza, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, someni Kanuni, akishajibu wengine hamuingii, wanakuwa wawili tu, ndivyo inavyokuwa.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimsahihishe mdogo wangu Mnyika, suala la *Common External Tariff* nililolitolea mfano, lilikuwa ni mfano wa jinsi nchi za Afrika Mashariki zinavyofanya kazi pamoja. Katika uchumi ambao sasa ni uchumi mmoja na *point* yangu katika msamaha wa kodi juu ya uwekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ*, nchi zote za Afrika Mashariki zimekubaliana kwamba ni miaka kumi. Kwa hiyo, kuna uwiano kabisa kwamba nchi zetu zote za Afrika Mashariki zinatoa fursa hizi kwa wawekezaji kwa miaka kumi na kwa sababu Serikali Kuu inatoa fursa hii kwa miaka kumi, Serikali imeona ni busara, Halmashauri vilevile zisubiri kipindi hiki hiki cha miaka kumi ili kodi hizi zinapoanza kulipwa kwa Halmashauri ziweze ku-*apply* kwa Serikali nzima. Huu ni utaratibu ambao unatumika kote, utaratibu wa ushindani, utaratibu wa uwezeshaji wa watu ambao tunawahitaji waje na kama sisi tutawakatalia na kama Halmashauri yako ingepewa nafasi ya ku- *impose* hiyo *tax* ya miaka mitano, naomba ujue kwamba wawekezaji wengi watairuka hiyo Halmashauri, waende Halmashauri nyingine.

Naomba niwahakikishie Wabunge wenzangu wa CCM ambao walikuwa wanahoji juu ya hili suala. Azma ya Serikali na nia ya Serikali hapa ni nzuri, tungependa tuongeze fursa hizi za uwekezaji mahali ambapo hakuna na kwa sababu katika kufanya hiyo kazi ni lazima tuziweke fursa hizi wazi, wawekezaji waweze kuziona na waone faida kiushindani, sisi na nchi zingine zote ambazo zitatuzunguka na kama nilivyosema awali nimesema nchi Nigeria na Ghana zinafuata utaratibu huu huu wa Tanzania na utaratibu huu umefanikiwa sana katika nchi nyingi kuweza kuwavutia wawekezaji wengi. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Sawa wanaofikiri, tunaendela kufanya maamuzi...

TAARIFA

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya kimaamuzi.

MWENYEKITI: Taarifa ya nini?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu unisikilize.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza, Mheshimiwa Zitto na Waheshimiwa mliosimama naomba mkae kwanza, hoja hii ni ya Mheshimiwa John Mnyika, kwa hiyo, nasema wanaofikiri kwamba mapendekezo aliyoleta Mheshimiwa Mnyika yakubalike waseme ndiyo na wasiyakubali waseme siyo.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 22

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 23

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hiki cha 23 lipo tatizo la kimsingi ambalo jana katika maelezo ya kutathmini au kuiangusha thamani fedha ya Tanzania. Kifungu hiki kinataja na huu ndiyo mtindo ambao pamoja na kwamba tuko katika umoja wa *custom* wa dunia, lakini suala la kutunga sheria, tukachukua pesa ya kigeni tukaiwekea thamani, halafu jambo lolote tukakokotoa kutoka pesa ya kigeni kuja kwa pesa ya Kitanzania, hilo ni tatizo. Hapa kama tunatunga sheria itajwe pesa ya Tanzania *or equivalent to other currencies*. Lakini siyo kutaja pesa za kigeni halafu ya Tanzania ikawa ya mwisho, *or Tanzania shilling*. Hiyo ni katika zile njia ambazo nasema siku zote tunaiangusha thamani shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikubaliki sisi, hata hizo nchi nyingine hawawezi kutunga sheria, wakaweka pesa ya kigeni, lazima tuweke shilingi ya Tanzania. Tukokotoe kitu chote kutoka shilingi ya Tanzania, sisi ndiyo wa ku-*dictate*. Lakini kuweka fedha ya kigeni halafu ukakokotoa kwa hesabu kwa kubadilisha shilingi ya Tanzania, hiyo ni *wrong*. Kuithamini shilingi yetu ni kuiweka shilingi ya *Tanzania or other currencies equivalent to other currency* lakini ya Tanzania ndiyo iwe msingi. Ahsante. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nalikubali pendekezo la Mheshimiwa Mnyaa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ninakupongeza sana. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 24

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 25

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Nimetoa ya kwangu Mwenyekiti.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijatoa ya kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 25 kinapendekeza adhabu ya faini kwa makosa ya usalama barabarani iongezwe kufikia shilingi 30,000/=. Katika Bajeti ya Serikali inaonyesha kwamba mapato yanayotokana na faini hizo za makosa ya barabarani yatapungua kutoka kipindi cha mwaka uliopita ya shilingi bilioni 10 hadi shilingi bilioni nane, pamoja na kuongeza hizi adhabu kufikia shilingi 30,000/=. Sasa kama mapato ya Serikali yatapungua pamoja na adhabu kuongezeka. Lengo la kuongeza faini ni nini kama siyo kutengeneza ulaji na rushwa barabarani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kwa sheria ilivyo sasa hivi faini ya makosa ya barabarani ni shilingi 20,000/= napendekeza ibaki kama ilivyo. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni rahisi kwamba ukiweka *deterrent punishment* wachache watafanya makosa na ndiyo maana fedha zitakuwa kidogo.

MWENYEKITI: Sijakusikia, umesemaje?

WAZIRI WA FEDHA: Tulisema tumeweka *8 billion* kwa sababu ukiweka adhabu kali zaidi mwelekeo ni kwamba wengi watakuwa waangalifu hawatafanya makosa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo?

WAZIRI WA FEDHA: Kibaki kama Serikali ilivyopendekeza.

MWENYEKITI: Nauliza ni shilingi ngapi? Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa marekebisho ambayo *Schedule of Amendments* ya Serikali ukurasa wa nne, ni shilingi 30,000/=.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu kwa ufupi sana hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kama anaamini kwamba adhabu kali inaondoa makosa, adhabu ya kwanza waliyokuwa wamependekeza ilikuwa faini ya shilingi 300,000/= . Sasa wameondoa kutoka shilingi 300,000/= wameleta mpaka shilingi 30,000/= kwa sababu hawaamini kwamba adhabu kubwa itaondoa makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema adhabu ya sasa hivi inatosha shilingi 20,000/= hujafunga mkanda, unaongeza *speed* ya kilomita 50 inatosha. Hatuhitaji kuongeza faini kila wakati tunapojifikiria hivyo kwamba inapendeza kuongeza adhabu. Adhabu iliyopo sasa hivi katika sheria ya sasa hivi faini shilingi 20,000/= inatosha kabisa. Tunaendelea ku-*improve* barabra zetu. Haya makosa yatapungua kwa sababu watu wetu wanazidi kuelimika zaidi. Hatuhitaji kuwatia umaskini zaidi kwa kuongeza faini hizi ambazo Serikali yenyewe inakiri kwamba wala hazitaongeza mapato ya Serikali. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *process* ya mambo haya yamepitia sehemu nyingi. Niliposoma *speech* yangu nilimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa ushauri ambao anatupatia. Tulipokaa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tulipata ushauri mwingi sana. Tukakubali ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na ndiyo maana tukapunguza kufikia hiyo shilingi 30,000/= . (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 26

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 27

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu tunajaribu kukimbia na muda, ikifika muda fulani, natakiwa nipitische tu sasa.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na sitakuchukulia muda wako mwingi. Mapendekezo yangu kuhusiana na kifungu cha 27 ni kuondoa yote. Kinachopendekezwa ni misamaha ya kodi tena na tumeshazungumza sana juu ya madhara makubwa ambayo tumeyapata na tunaendelea kuyapata na tutaendelea kuyapata kama tusipoanza kutekeleza Mpango wa Taifa wa miaka mitano unaosema; “Misamaha ya kodi ipunguzwe ifikie angalau asilimia moja ya Pato la Taifa.” Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Serikali mna maelezo ya ziada? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuendelea kuangalia utaratibu wote unaohusika na misamaha hii ya kodi na Serikali kama tulivyosema hapo mwanzo misamaha ambayo tunaisamehe ni misamaha tu ambayo ina tija. Ni misamaha tu ambayo kwa kuwepo kwake kunaongeza tija kwa wananchi wa Tanzania kwa mambo yanayohusiana na uwekezaji, mambo yanayohusiana na kuwapa ajira watu wasio na ajira. Mambo yanayohusiana na kuongeza thamani bidhaa za wakulima wa vijijini ambao sasa hivi faida yake ni kidogo. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba misamaha hii ni misamaha tu ambayo ina tija na ningeomba kusema kwamba watu ambao wanaweza wakapinga kila kitu, wakapinga kupitisha Bajeti ambayo kesho yake watapokea posho na mshahara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kabisa wasipinge kila kitu, hata jambo ambalo lina tija na naomba nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi wa Tanzania wafahamu kwamba azma ya Serikali, nia ya Serikali ni kuhakikisha tunaongeza tija, tunakuza uchumi kwa kasi ambayo imeahidiwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu nusu dakika.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika tatu, lakini sitazitumia zote. Haya maneno kwamba misamaha ya kodi yenye tija, yenye tija, yenye tija, si maneno ya kweli. Ushahidi wangu ni Kamati ya Dkt. Kipokola iliyoundwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye, Kamati ya Mheshimiwa Lau Masha iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, Kamati ya Mheshimiwa Mark Bomani iliyoundwa na Mheshimiwa Rais na zote zilisema misamaha ya kodi haijawa na tija, hakuajawa na *win-win situation*. Huyu Waziri Mdogo hatuambii chochote kipya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, wenyewe mmekataa maneno ya kudhalilishana. Sasa mnafanya nini?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, dharau hiyo, afute kauli yake.

MWENYEKITI: Kwanza hakuna Waziri Mdogo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaelewa maneno yapi ndiyo niyafute. Si Waziri Mdogo huyu! *(Makofi)*

Aaah, aaah, aaah, kumbe ni Naibu Waziri. Aaah, samahani Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Naomba msikilize, acheni kusimama bila sababu. Mheshimiwa Tundu Lissu hebu malizia.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kwamba nilisahau kwamba Mawaziri Wadogo kama walivyokuwa wanaitwa zamani imebadilika, siku hizi wanaitwa Naibu Mawaziri. Nafuta usemi wangu. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, natumia Kifungu cha 88(10) sasa nitapitisha kwa *parts*. Hakuna cha *amendment* za mtu, basi naendelea kwa *parts* kwa sababu nina dakika tano tu. Tuendelea.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Hakuna Mwongozo, sina muda. Tunaendelea.

Sehemu ya 11

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Sehemu ya 12

Kifungu cha 34
Kifungu cha 35

(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa mtoa hoja Taarifa.

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011
(The Finance Bill, 2011)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa taarifa kwamba

Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 (*The Finance Act, 2011*) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Kwa hiyo, Muswada huu umepita halafu utangojea *signature* ya Mheshimiwa Rais, nadhani atafanya mapema kwa sababu utanzisha kazi ya kukusanya kodi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ngumu ambayo imekamiliika, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni kwa mujibu wa Kifungu cha 150(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la 2007.

Kwa kuwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge unaoendelea pamoja na shughuli nyingine zilizopangwa, Wabunge wanatakiwa kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu kufuatana na masharti ya Kanuni ya 99 na kwa kuwa Kanuni ya 38 imeweka utaratibu wa kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu Maswali ya Papo kwa Papo kila siku ya Alhamisi kwa muda usiozidi dakika 30 na kwa kuwa uwasilishaji wa mjadala wa hotuba ya Waziri Mkuu umepangwa kuanza kesho siku ya Alhamisi, tarehe 23 Juni hadi tarehe 29 Juni, 2011.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kujiandaa kikamilifu na kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Ofisi yake kwa mwaka wa 2011/2012 na kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano Mkuu wa Nne, Kanuni ya 38 itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 38 ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba kutakuwa na kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kila siku ya Alhamisi kisichozidi dakika 30 itenguliwe na badala yake Mheshimiwa Waziri Mkuu apewe muda huo ili ajiandae na uwasilishaji wa hotuba ya Bajeti ya Wizara yake hiyo kesho. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hii hoja inatenguliwa kwa ajili ya kesho tu, siyo kwamba ndiyo imeondoka. Sasa nitawahoji wanaokubali kwamba hii Kanuni ya 38 itenguliwe kwa ajili ya kesho kwa sababu Waziri Mkuu anawasilisha hotuba yake kesho hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Kanuni husika zilitenguliwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda tuliomba uongezwe dakika 30 umeshamalizika, kama nilivyosema hatuna matangazo. Kesho tunaingia na hotuba ya Waziri Mkuu. Mwingine aliuliza kwamba niliifunga orodha, mimi sikufunga orodha, mnaweza kujaza. Lakini tunaweza tusipate nafasi wote. Lakini jazeni kama inavyokuwa kawaida. Kama nilivyosema kesho tutakuwa na tafrija ya Balozzi wa Canada, haitakuwa kwenye viwanja vyetu itakuwa *St. Gasper*. Maelezo tuliyopata na *Foreign Affairs* wanasema siku ya Taifa ya nchi ilitakiwa wafanyie kwenye eneo ambalo ilikuwa ni nchi yake kama pale Ubalozini. Sasa huyu akija kufanyia hapa Bungeni siyo sahihi, kwa hiyo, tutafanyia *St. Gasper*. Kwa hiyo, naomba Wabunge mjiandae kwenda kwenye hiyo tafrija kesho, msifanye kuondoka kwa sababu Balozzi ameleta hapa kwa ajili yetu sisi. Kwa hiyo, naomba wote mjiandae kesho hiyo jioni tutawaarifu tena vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi mliyofanya kwa siku ya leo. Naomba niwatakie jioni njema. Naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.16 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 23 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*